**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**
**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Hamad Masoud Hamad | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa. |
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi |
| 18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |

| | |
|---|---|
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 30.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 31.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 32 Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 36.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 37.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 38.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 42.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 43.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 44.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 47.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |
| 51.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

**Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Pili – Tarehe 18 Juni, 2012**

*Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti):** Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika leo hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Maoni ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 31**

**Kero za Muungano**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** – aliuliza:-

Moja kat ya Kero za Muungano ni kutokuwepo uwiano katika kushika nafasi za Uongozi au nafasi za Utumishi wa Umma za Jamhuri ya Muungano na zile za vyombo vya Ulinzi baina ya wananchi wa nchi mbili hizi, Mfano: Mkuu wa Jeshi la Ulinzi (*CDF*) na Mkuu wa Jeshi la Polisi (*IGP*).

Je, ni sababu gani zilizosababisha kusiwepo uwiano au *fomular* maalum baina ya wananchi wa pande mbili hizi za Muungano katika kushikilia nafasi hizo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake Nam, 31 kwa heshima na taadhima.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa mamlaka Mhe. Rais aliyepo madarakani kufanya uteuzi wa viongozi na wakuu wa taasisi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiwemo Mkuu wa Jeshi la Ulinzi na Mkuu wa Polisi. Katika uteuzi wa nafasi zote hizi, katiba haikuweka vigezo, uwiano wala *fomular* maalum katika uteuzi huo, uteuzi huo ni mamlaka aliyonayo Mhe. Rais ambaye pia ni Jemedari Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Mhe. Spika, hata hivyo, kutokana na mchakato wa marekebisho ya Katiba hivi sasa ni wakati muafaka wa kutoa maoni yetu kwenye Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba Mpya itakapopita katika maeneo yetu. Sote tuamini kwamba, maoni yetu ni muhimu na yanahitajika kwenye marekebisho ya kuandaa katiba mpya, tutoe maoni yetu ili kuweza kutatua matatizo yaliyopo na yanayojitokeza kwenye Muungano wetu. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba katiba haikuweka vigezo maalum katika kugawa nafasi hizi, na kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, *CDF*, *IGP* na Mkuu wa Usalama wa Taifa wote ni kutoka Tanzania Bara, na kwa kuwa Zanzibar haina uwezo wa kujiunga na taasisi yoyote ya Umoja wa Kimataifa bila ya idhini ya Tanzania Bara (Tanganyika).

Je, atakubaliana nami kwamba Zanzibar ni koloni la Tanganyika. Hilo moja.

Pili, Mhe. Spika, kwa kuwa viongozi wetu wakubwa na waasisi wa Muungano huu akina Mzee Aboud Jumbe Mwinyi, Mzee wetu Ramadhan Haji Faki, Maalim Seif Sharif Hamad aliyekuwa Waziri Kiongozi wa nchi hii walihangaika sana katika kutatua kero za Muungano na kujiondosha katika jinamizi hili la Muungano uliopo sasa.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba Tanzania haifuati utawala bora na demokrasia.

**Mhe. Spika:** Hivi hili swali la mwanzo linakwenda sambamba na hili swali mama la ugawaji wa nafasi hizi za *IGP* na *CDF*? Nadhani haliendi, jibu hilo la pili.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza nakushukuru wewe kwa kutoa maelekezo ya busara katika kutuelekeza uli tuweze kufuata utaratibu wetu tuliojiwekea katika Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Spika, sote hapa tumeapa kutii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi zinaendeshwa kwa katiba na sheria, tunachokizungumzia hapa ni maelezo yaliyomo ndani ya katiba yetu na katiba hii tumeitunga sote kwa pamoja na ndio maana serikali zote mbili zilipoona kuna mapungufu ndani ya katiba yetu, na kwa kuwa kunahitajika maslahi ya Zanzibar yalindwe kwa ukamilifu wake. Vile vile na maslahi ya ndugu zetu wa Tanzania Bara nayo yalindwe kwa ukamilifu wake, ndio maana Mhe. Spika, ukaja huu mpango maalumu wa kisheria kwa wananchi kutoa maoni yao, ili pale ambapo pana kasoro katika katiba hii basi kasoro hizo tuziondoshe na tuwe na katiba iliyo bora zaidi.

Haya mapungufu yote ambayo Mhe. Saleh Nassor anayasema na wananchi wengine wanayasema, huu ni wakati muafaka wa kujipanga kwa mujibu wa sheria tukatoa maoni yetu bila ya woga kwa kufuata taratibu zilizowekwa, ili tuweze kuwa na katiba ambayo itakidhi haja na matakwa ya wananchi wetu na itaweka utaratibu mzuri kwa waendeshao nchi yetu na kuondoa kila kasoro iliyopo katika nchi yetu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipa rufsa asubuhi hii. Serikali inachukua juhudi gani za kuzungumzia kero hizi za uongozi wa ngazi za juu kupitia kamati ya usuluhishi wa kero za Muungano.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, jitihada za serikali ni hizi ambazo Waheshimiwa Wajumbe wanazielewa na wananchi wote wanazielewa kupitia kikao cha pamoja cha kuzungumzia kero za Muungano ili kuondoa kero hizo, zipo baadhi ya kero ambazo sasa zimepata ufumbuzi wake.

Lakini kutokana na kwamba serikali imeona upo umuhimu wa kutafuta suluhu yenye muafaka ya kuyaondoa matatizo hayo kwa ukamilifu na kuondoa kero hizi ndio maana tukaleta sheria ya kusikiliza ama ya kutoa maoni ili kufanya katiba mpya, wananchi nao wana haki ya kutoa maoni yao wanavyoona wao inafaa hakuna aliyewakataza, cha msingi ni kufuata taratibu za sheria zilizopo.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza ambalo litakuwa na vifungu viwili a na b.

(a) Mhe. Waziri katika kutoa maelezo yake mazuri alisema kuwa tuitumie fursa hii kwenye Tume ya Kukusanya Maoni ili kupeleka kero zetu, kaelekeza kuwa yatazingatiwa na kupatiwa ufumbuzi. Lakini Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi hili likiwa ni chombo cha wananchi tunawakilisha wananchi wote, katika kipindi kilichopita kwa pamoja kabisa tulipitisha kuwa mafuta si jambo la Muungano. Kwa bahati mbaya na masikitiko juzi nimesoma gazeti kuwa ile *CPDC* ambacho si chombo cha Muungano kimetoa idhini ya kuchimba na kutafuta mafuta katika eneo la Zanzibar ambalo wamesema kuwa kuna mafuta mengi sana. Kwa hivyo, ikiwa kauli yetu ya Baraza haifuatwi kwenye chombo cha Muungano itakuwa au wana ushahidi gani kuwa hawa watu binafsi kero zao zitafuatwa.

(b) Mhe. Waziri kasema kuwa tumeshirikiana katika kuitunga hii Katiba ya Muungano, Zanzibar imeshiriki vipi katika kuitunga katiba hii.

**Mhe. Spika:** Suala la mafuta na ugawaji wa madaraka ya *IGP* na *CDF* nadhani kidogo hapa hapalingani na swali mama, angalau ingekuwa ni madaraka mengine ugawaji ule basi kidogo ingekuwa inalingana na hilo. Sasa hili Mhe. Waziri liache na hilo la (b) hebu tusaidie.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, tuna utaratibu katika nchi yetu wa kutunga katiba na utaratibu huo umewekwa kisheria. Serikali zetu mbili zinapopata mawazo kutoka kwa wananchi wake juu ya suala ambalo linahitaji kufanyiwa mabadiliko ya katiba ama kuundwa kwa katiba basi serikali hizi hukaa pamoja na kuzungumzia mambo hayo. Lakini kwa upande wa Zanzibar kuwa ni vipi imeshiriki katika kuundwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwanza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshiriki kikamilifu katika kutoa maoni yake katika katiba iliyopo sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapa ieleweke Mhe. Spika, kwamba serikali ni endelevu, hao waliopo wakati huo waliwakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wakafanya wajibu wao wa kutoa maoni yao kwa upande wa Zanzibar.

Lakini hata hivyo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo lilipitisha kauli ile ya katiba ile, lina uwakilishi wa pande mbili za Muungano wetu. Pia katika katiba yenyewe inaonesha utaratibu wa namna ya kupitisha maamuzi yale ya katiba. Kwa hivyo, Mhe. Spika, na kabla ya kufikia hatua hiyo wadau mbali mbali kwa upande wa Tanzania Bara na upande wa Zanzibar walitoa maoni yao kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyopo sasa.

Lakini hata hivyo, kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika katiba yetu ndio maana serikali zetu mbili zimekaa na kuona umuhimu wa kufanya katiba mpya ambayo inawashirikisha wananchi wake wote kutoa maoni yao, mawazo yao waamue ni katiba gani wanayoitaka kwa maslahi ya nchi yao. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe maswali haya ambayo sikumpa nafasi waziri kuyajibu sio kwamba hayawezi kuulizwa Barazani, lakini hayaendani na swali mama. Kwa hivyo, tukitaka kuyauliza tutafute utaratibu wa kuuliza kwenye swali la msingi. Tunaendelea.

**Nam. 10**

**Uchakavu wa Chelezo cha Kibweni KMKM**

**Mhe. Ali Salum Haji** – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu chelezo cha Kibweni KMKM kimeshindwa kufanya kazi kwa uchakavu.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kufufua chelezo hicho.

(b) Je, wizara haioni kuzifanyia ukarabati boti za vikosi vya ulinzi kwenye chelezo nyengine ni kutoa siri kuhusiana na uwezo wa boti hizo kwa raia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 10 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Kikosi cha KMKM imo katika jitihada kubwa za kukijenga upya Chelezo cha Kibweni. Aidha, katika kufanikisha azma hiyo, mawasiliano ya awali yamekwishafanyika na mkandarasi kutoka Uholanzi anayeitwa “Damen Shipyard”, ambaye alitoa makisio ya gharama za kutengeneza chelezo hicho. Hata hivyo, Mhe. Spika, jitihada pia zinaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa kushirikiana na Kampuni hiyo ili kutoa muono halisi wa faida itakayoweza kupatikana kutokana na mradi huo wa mradi wa chelezo pamoja na kufahamu gharama halisi.

**(b)** Nakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba upo umuhimu mkubwa wa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) kuwa na chelezo chake yenyewe, ndio maana juhudi zinachukuliwa ili kuhakikisha kwamba chelezo cha kikosi hiki kinatengenezwa upya na kuwa cha kisasa. Naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba wakati wowote ambapo kikosi kinafanya ukarabati wa boti zake katika chelezo chengine basi kunakuwa na uangalizi mkubwa tena unaofanywa na askari wenyewe mpaka kazi inapokamilika. Hata baadhi ya kazi huwa wanasaidiana panapofanywa hiyo kazi kwa kushirikiana na hawa askari.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwanza nikupongeze Mhe. Waziri kwa kuleta mkandarasi mwelekezi katika hatua hii ya Mwanzo, lakini nataka kujua ni kiasi gani zitagharimu katika ujenzi huo utakaoendelea.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, katika *proposal* aliyoleta mwanzoni hii kampuni wameikisia kwamba ujenzi utagharimu Euro 9, 250,000/- na wametarajia kwamba ujenzi ungefanywa kwa miezi 23 mpaka kukamilika kwake.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa sheria ya manunuzi ya mwaka 2005 ina taratibu zake na sifa zake juu ya kumpata mkandarasi, na kwa kuwa tumekuwa tukigundua hasa katika ofisi yake Mhe. Waziri taratibu za manunuzi hazifuatwi. Je, kwa mkandarasi huyu wamefuata? Kama wamefuata atwambie ni wangapi walioomba hadi wakafikia kuamua kumpata huyu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, kwanza naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba taratibu za manunuzi kwa sheria za mwaka 2005 zimefuatwa. Kwa sababu ile Kamati ya Tenda ya Kikosi chenyewe ambayo inayo imeipitia hiyo *proposal* na imeipitisha. Lakini kama tunavyosema na ninarudia tena, tunaangalia ule muono wenyewe kwamba hii kampuni kweli, kwa sababu bado hatujatiliana saini ni haya mazungumzo tu na sisi tunaendelea na kufanya upembuzi yakinifu. Kwa hivyo, baada ya kutangaza na kutafuta hizo kampuni basi tukaipata hii, lakini kama tunavyosema kuwa bado ujenzi haujaanza tumo katika upembuzi yakinifu kuangalia *cost benefit analysis* na namna gani tutafaidika, hivyo bado tuko katika hatua ya kujitayarisha.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri katika maelezo yake ametaja kampuni hiyo ni kampuni elekezi, namuuliza Mhe. Waziri ni sheria gani iliyotumika kwa kampuni hiyo elekezi kuwa sasa wanageuka wanakuwa ndio wajenzi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, naomba kumafahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba kidogo nataka afahamu kuna tofauti kati ya mambo ya kijeshi na mambo ya kiraia, si kampuni zote tukaichukue tukajenge chelezo cha kijeshi, kule kuna taratibu zetu, kuna siri zetu, kuna mambo ya kuyalinda. Kwa hivyo, hata tunapotangaza tunatangaza lakini *short listing* tunajua tumchukue nani sio kila raia tu akajenge kituo cha kijeshi. Ahsante sana.

**Nam. 187**

**Kutembea na Bendera**

**Mhe. Mohammed Said Mohammed** – Aliuliza:-

Hivi karibuni katika mji wa Zanzibar na vitongoji vyake pametokea mfumko mkubwa wa wananchi kutembea na bendera za serikali katika gari zao pamoja na ofisi mbalimbali kwa watumishi.

(a) Je, kuna uhalali wowote wa wananchi wa kutembea na kuweka ndani ya gari bendera ya Taifa.

(b) Na kama sio, serikali imechukua hatua gani za kisheria mpaka sasa.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye Nam. 187 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali haimzuii mwananchi wake kutembea na bendera ndogo ya Tanzania au hata ya Zanzibar, kama ataiweka ndani ya gari yake au kwa wale wenye vyombo vya Maringi mawili mbele kwenye sehemu ya usukani wake au hata kwenye ofisi zao.

Mhe. Spika, hii ni *fair* kwetu kuona wananchi hao wanaipenda nchi yao, haya takriban hufanywa kila pahala ulimwenguni hasa pale ambapo wanasherehekea kitu fulani kama vile mpira, siku ya kitaifa na kadhalika kwa sababu hakuna tatizo lolote kisheria.

Mhe. Spika, serikali haijachukua hatua yoyote ile na wala si busara kuchukua hatua hizo kwa sababu watu hawa hawajafanya kosa ila wanaonesha dhahiri kuwa wanaipenda nchi yao kwa moyo wao wote.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nimuulize swali dogo tu la nyongeza Mhe. Waziri kutokana na majibu yake. Mhe. Spika, kwa sababu hivi sasa hapa Zanzibar kumejitokeza hamasa kubwa za uzalendo za kuipenda nchi yao, na kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri katika majibu yake, bendera ni moja katika kielelezo cha kuthibitishwa uzalendo na mapenzi kwa nchi, lakini kwa Zanzibar kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa bendera za Zanzibar ambazo kwa wananchi wa Zanzibar zina umuhimu mkubwa kuliko bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sijui serikali inachukua hatua gani ya kuona inachapisha kwa wingi bendera za Zanzibar ili wananchi wa Zanzibar wanapotaka kuzitumia kuthibitisha uzalendo wao waweze kuzitumia kama wanavyotumia wenzetu wa Jamhuri ya Muungano ambao kwao bado ina umuhimu mkubwa zaidi kuliko bendera yetu ya Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba bendera za Zanzibar ni kidogo na wazo lake ni zuri nakubaliana nalo. Mimi binafsi nitashirikiana na wizara inayohusika ili kuhakikisha kwamba bendera nyingi za Zanzibar zinapatikana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ndogo kuongezea majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, suala la bendera liko chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, lakini namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba katika Idara yetu ya Bohari Kuu bendera za Zanzibar zipo za kutosha na kama anazo fedha aende akanunue na bendera moja inauzwa kwa shilingi arobaini elfu. Kwa hivyo, namthibitishia yeye pamoja na Baraza lako tukufu kwamba bendera za Zanzibar zipo na zinatosha aende akanunue tu pale.

**Nam. 4**

**Ujenzi wa Barabara ya Uzi Ng'ambwa kwa Kiwango cha Lami**

**Mhe. Mussa Ali Hassan -** Aliuliza:

(a) Kwa kuwa Barabara ya Uzi/Ng'ambwa haijawahi kujengwa kwa kiwango cha lami, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango hicho.

(b) Je, serikali haioni kwamba hali hii inawapa usumbufu mkubwa wananchi wanaotumia barabara hiyo.

(c) Kwa kiasi gani kukosekana kwa barabara bora kunazorotesha maendeleo ya kiuchumi ya wananchi wanaoishi Uzi /Ng'ambwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 4 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(b Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara hiyo haijawahi kujengwa kwa kiwango cha lami, ila barabara hii inahitaji taaluma na utaalamu maalum wa kuweza kuijenga kwa lami, kwa kutambua kwamba ina urefu usiopungua kilomita 2 lililopitiwa na bahari. Imani yangu kwamba pamoja na utaalamu huo serikali yetu ikipata uwezo wa fedha suala hilo litazingatiwa.

Jibu (a) na (c) kwa pamoja Mhe. Spika, serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Uzi- Ng'ambwa na barabara nyengine kama hiyo kwa Maendeleo ya Jamii inayoishi kwenye kisiwa cha Uzi, kwa kutambua umuhimu huo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imekuwa ikishirikiana na uongozi wa Jimbo la Koani pamoja na wananchi wa Uzi, kwa kutoa vifaa na gari kwa kila siku ya Jumapili ili kuifanyia matengenezo barabara hiyo hadi pale Serikali itakapopata fedha za ujenzi wa barabara kwa kiwango kinachostahiki cha lami.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji barabara itatenga fedha maalum kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya kawaida *(routine maintenance)* barabara hiyo, ili iweze kupitika kwa urahisi wakati serikali ikiendelea kufanya jitihada ya kutafuta fedha kuweza kujenga kwa kiwango cha lami.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Spika, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, nataka kumuuliza swali la nyongeza.

Ni lini kwa vile barabara ya Uzi-Ng'ambwa ni kivuko ni lini barabara hiyo itajengwa madaraja makubwa ili ziweze kupita gari zote nzito za kuweza kufika Uzi-Ng'ambwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, ni kweli natambua kwamba Mhe. Mwakilishi kwamba ana kiu ya kutaka kuona watu wa Uzi wanajengewa daraja. Naamini kwamba dhamira ya serikali, lakini kwa wakati huu suala la ujenzi wa daraja kwa watu wa Uzi ni jambo ambalo haliwezekani. Hadi pale serikali itakapokuwa na uwezo wa fedha na utaalamu kwa kutambua tu kwamba eneo linalohitaji kujengwa daraja hilo ni eneo refu lisilopungua mita 2000. Mategemeo yetu ni kwamba pale fedha zitakapopatikana utaalamu wa serikali ukawa unakidhi hakuna sababu ya kutofanya ujenzi huo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Waziri utakubaliana nami kwamba tokea Mapinduzi ya Mwaka 1964 barabara ile haijafikiriwa hata kwa jicho la huruma. Umekiri katika suala la msingi hapa serikali inafikia suala hilo, lakini nataka nikwambie kwamba serikali haina nia ya kufikia suala hilo, je utakubaliana nami.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, sikubaliani na Mhe. Mwakilishi kwa kusema kwamba serikali haina nia ya kujenga barabara hiyo. Katika maelezo ya jibu langu mama tumeeleza kwamba barabara hii imekuwa ina kawaida ya kufanyiwa matengenezo kwa kila mwaka. Katika mwaka huu wizara yetu chini ya usimamizi wa UUB na ushirikiano mzuri tunaoupata kwa viongozi husika wa jimbo, tumeendelea na utaratibu huo wa kujenga katika kiwango kile cha kuweka mawe na kifusi. Ni jambo ambalo serikali imekuwa ikitoa vifaa, wataalamu, pamoja na gari kwa kila wiki katika kuona tu tunapunguza changamoto hiyo.

Uwezekano wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kunahitaji gharama na ni gharama kubwa. Kwa kutambua kwamba kuna eneo linalopitisha maji ya chumvi, kwa hiyo dhamira ya serikali ni kujenga barabara. Kikwazo kilichopo sasa hivi ni uwezo, lakini nia ya serikali ni kuona kwamba wananchi hawa wanasaidiwa.

**Nam. 34**

**Umuhimu wa Madini Joto Katika Uzalishaji wa Chumvi**

**Mhe. Saleh Nassor Juma –** Aliuliza:-

Kwa kuwa wataalamu wa Afya wamekuwa mara nyingi wakitueleza na kusisitiza umuhimu wa madini joto katika mwili wa binaadamu. Na kwa kuwa wataalamu hutushauri kuwa chumvi tunazotumia lazima ziwe na Madini Joto. Na kwa kuwa katika maeneo mengi ya Kisiwa cha Pemba wananchi wameanzisha mashamba ya chumvi ili kujipatia kipato pamoja na kupunguza umasikini.

Je, ni utaratibu gani unatumiwa na serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhakikisha kuwa kila mkulima wa chumvi anapata Iodine kwa ajili ya shamba lake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya –** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako tukufu swali lake Nam. 34 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba wawakilishi nyote na wananchi mnatambua umuhimu wa madini joto katika mwili wa binaadamu na athari zake yanapokosekana. Kwa mantiki hiyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Afya imeziimarisha sheria ndogo ndogo zinazosimamia matumizi ya madini joto kwenye chumvi.

Wizara ya Afya kwa kupitia Kitengo cha Lishe pamoja na UNICEF wametoa mafunzo kwa vikundi vya uzalishaji pamoja na vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya uchanganyaji wa chumvi na madini joto. Pia imetoa mafunzo kwa Maafisa wa Afya kuwasimamia, na wamepewa vifaa vya kupimia madini katika chumvi.

Serikali ya Mapinduzi imeshirikisha Jumuiya ya Wazalishaji Chumvi Pemba, *Association of Zanzibar Salt Processing Organization (AZASPO)* kwa msaada wa UNICEF iliwanunulia madini joto *(potassium iodate)* na kuwakabidhi wao kama ni wadhamini na wasimamizi wa vikundi hivi. Lengo la kufanya hivyo wao *(AZASPO)* wanatakiwa wawauzie wazalishaji na pesa wanazozikusanya waziendeleze kwa kununulia madini hayo kwa mzunguko *(revolving fund)*. Katika kutekeleza hilo vikundi mbali mbali vilipatiwa madini hayo katika kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2010.

Wizara ya Afya kupitia Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi itaendelea kusimamia na kufanya uchunguzi wa viwango vya madini joto katika chumvi.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza niishukuru serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuwapa taaluma wadau wa uzalishaji chumvi na kuwapatia hayo madini joto. Mhe. Naibu Waziri amesema kwa kushirikiana na UNICEF wamepeleka iodine kwa wazalishaji lakini hadi leo hii tatizo la *iodine* kwa wazalishaji chumvi ni kubwa. Kwa sababu ukosefu wa *iodine* katika lishe husababisha *mental retardation.* Kwa hivyo kuna uwezekano hapo mbele ikiwa serikali haikuwa *serious* tukapata kizazi kilichokuwa *retarded mental*, kuachia hivi na kuwaachia UNICEF bila ya kushirikisha serikali kwenda kwa wadau wenyewe kuhakikisha kwamba chumvi inakuwa *iodised* si kutuongezea idadi ya watu ambao akili zao ni taahira.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, (AZASPO) ni Jumuiya ya Wazalishaji Chumvi nao walipewa elimu na wakapewa iodine, wakaambiwa kwamba mzungushe ili muweze kupata fedha wazalishaji wapate iodine. Kilichoendelea kwa (AZASPO) sikifahamu ikawa kwa nini wameshindwa hilo. Lakini walipewa mtaji wa kutosha na iodine ya kutosha. Lakini hata hivyo baada ya kuonekana kwamba *iodine* hakuna, kuna wauzaji ambao wamejitokeza, kwa hivyo kuna mawakala wawili Pemba wanauza iodine. Kwa hivyo hawa wazalisha chumvi ni kiasi tu cha kwenda kununua wakachanganya kwenye chumvi yao. Kwa hivyo sioni tatizo liko wapi hapa. Kwa sababu *iodine* ipo, wauzaji wapo, AZASPO walishirikishwa, wananchi walishirikishwa.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kutoa mafunzo na kutoa elimu kubwa kwa wazalishaji wetu wa chumvi hii.

Mhe. Spika, lakini kwa kuwa chumvi tunazotumia ni lazima ziwe na madini joto ni vizuri sana kwa sababu ya Afya za binaadamu. Pia kwa kuwa wananchi wetu hawawezi kuitambua chumvi iliyokuwa na madini joto na chumvi iliyokuwa haina madini joto.

Je, Mhe. Waziri huoni kwamba ipo haja ya wizara yako kutoa mafunzo kwa njia ya vyombo vya habari ili wananchi waweze kuitambua hiyo chumvi na kama chumvi haikutiwa madini joto wasinunue.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nataka nikubaliane na wewe kwamba si kila mtu anafahamu hilo, hilo ni sadakta. Lakini kwa kadiri ya uelewa wangu nafahamu kwamba Wizara ya Biashara huwa inakagua viwango na chumvi za madini joto huwa ina alama ambayo imewekwa kwenye pakti ya kile kifuko kinachojazwa chumvi. Chumvi hizo ndizo zinazotakiwa zipitishwe kwa sababu si kila mtu anaweza kujua kwamba hii ina madini joto au haina. Kwa hivyo hiyo alama iliyokuwepo hapo ndiyo inayoonesha kwamba hichi kifuko chumvi iliyokuwemo ndani ina madini joto. Watu wetu wa Chakula na Vipodozi wanavyopita kucheki wanayaangalia haya. Ni matumaini yangu kwamba chumvi inayotumiwa ipo salama.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri suali moja la nyongeza.

Kwanza na mimi niungane na wenzangu kuishukuru sana Wizara ya Afya kwa kuitoa elimu kwa wajasiri amali wazalishaji wa chumvi katika kuingiza madini joto katika chumvi. Lakini kwa kuwa Wizara ya Afya ndiye msimamizi mkuu wa afya za wananchi wake katika nchi. Na kwa kuwa wametoa elimu ya kuingiza hayo madini joto katika chumvi.

Je, Mhe. Waziri umeunda kitengo maalum cha kuwakagua hao wazalishaji wa chumvi kuangalia kama hiyo kazi wanaifanya? Kama hakuna ni lini Wizara yako itaunda wakaguzi maalum wa kuwapitia na kuwakagua. Na kama kimeundwa ni mara ngapi wanapita na kuwakagua na kuangalia wakajua kama kweli wanayatumia hayo madini joto.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, katika jibu mama nilisema kwamba wakati wa mafunzo kuna maafisa wa Afya ambao wapo hapo karibu na hao wazalishaji chumvi ambao na wao walifundishwa pamoja na hao wazalishaji chumvi wenyewe. Kazi yao kubwa ni kuhakikisha kwamba wanasimamia hilo, kuona kwamba matumizi ya iodine katika chumvi yanayotiwa yanakubaliana na viwango vilivyokubalika. Wana vifaa vya kuchekia hayo. Inapotoka kule chumvi inakuwa tayari imeshakaguliwa na maafisa wa afya. Inapofika madukani

nimesema kwamba Bodi ya Chakula ya Dawa na Vipodozi inasimamia kuhakiki hizo chumvi zilizokuwemo katika maduka zina madini joto. Kwa hivyo, hivyo viwili vinahakikisha hilo na hiyo ndiyo kazi yake.

**Nam. 132**

**Mfuko wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo**

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa -** Aliuliza:-

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2008/2010 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Kikwete na Rais wa Zanzibar na Mhe. Amani Abeid Karume walianzisha utaratibu mzuri wa kuwa na mfuko wa kuwasaidia wajasiriamali wadogo wadogo ambao kwa upande wa Zanzibar ulijulikana kwa jina la JK na AK. Mfuko huo ulitoa matumaini makubwa kwa wajasiriamali hao.

(a) Wananchi wangapi waliokopeshwa fedha hizo na kiasi gani cha fedha kilitolewa.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kimesharejeshwa.

(c) Je, ni wanawake wangapi katika Mkoa wa Mjini Magharibi wamepata mkopo huo.

(d) Je, Mhe. Waziri waanzilishi wa mfuko huo wana dhamira ya kuendelea na mfuko huo na kama ndio ni lini mfuko huo utaanza tena.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika -** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 132 lenye vifungu a,b, c na d kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, jumla ya mikopo ambayo imetolewa ni 750. Mikopo hiyo imetolewa kwa watu binafsi/wajasiriamali mmoja mmoja 676, SACCOS 10 na vikundi vya kiuchumi 64 vyenye idadi tofauti ya wanachama, Jumla ya TShs. 1,529,884,831.55 zilitolewa kupitia mikopo hiyo.

b) Mhe. Spika, fedha zilizorejeshwa ni T.Shs. 765,587,363.75 hadi kufikia Mwezi wa Aprili 2012, ambayo ni sawa na asilimia 50.04

c) Mhe. Spika, jumla ya wanawake 170 katika Mkoa wa Mjini Magharibi waliofaidika na mkopo huo kati ya wanawake 276 waliopewa mkopo wa Mikoa yote kwa Zanzibar.

d) Mhe. Spika, waanzilishi wa Mfuko huo pamoja na Rais wetu Dokta Ali Mohammed Shein, wana dhamira ya kuendeleza mfuko huo na tunatarajia utaanza tena mara tu yatakapokamilika mazungumzo baina ya Benki Kuu na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Aidha kupitia Mfuko wa Uwezeshaji uliozinduliwa na Dokta Ali Mohammed Shein utaongeza nguvu katika mpango wa Mikopo hapa nchini.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana.

Mhe. Spika, katika utafiti wangu nimegundua kuwa katika Mfuko wa Kujitegemea watu wanakwenda vizuri sana lakini katika Mfuko wa AK JK una ugumu mkubwa sana kwa wanaokopeshwa kurejesha fedha hiyo, kiasi ambacho Benki ambao ndio wahusika wakuu wa mfuko huu nasikia wameshaanza hata kusita kutoa tena fedha zao wa kuwakopesha wananchi.

(a) Je, Mhe. Waziri kalichukulia uzito gani suala hili la Mfuko wa AK JK.

(b) Kuna utaratibu gani wa kuchanganyisha huu mfuko ili kuondoa matatizo yanayojitokeza hivi sasa.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Spika, napenda kumtoa wasi wasi Mheshimiwa kuanzia kipindi cha Bajeti hii ambayo imeshaanza sasa hivi kipindi hichi na kuendelea, mifuko hii yote tuna nia ya kuikusanya pamoja na kuifanyia kuwa na management ya aina moja, ili kuondokana

na hayo matatizo ambayo Mheshimiwa ameyaeleza. Lakini pia napenda nitoe taarifa ambayo nimewahi kuitoa huko nyuma kwamba Mifuko ya AK JK hii ilikuwa inasimamiwa zaidi na Benki ya Watu wa Zanzibar.

Hivi sasa kama nilivyosema katika jibu langu mama ni kwamba sasa hivi tuna makubaliano kati yetu sisi na Benki ya Watu wa Zanzibar kwamba mfuko huu sasa usimamiwe na Wizara yetu moja kwa moja, na ndio tutakaoratibu kutoa mikopo hiyo. Naomba asiwe na wasi wasi Mheshimiwa tutaisimamia vizuri mifuko hii ili kuweza kutolewa vizuri.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Waziri kuna wengine hawajalipa mpaka leo fedha hizo. Je, wizara yako inachukua sheria gani hao watu ambao hawajalipa ili kuweza kuwanufaisha na wengine waweze kuendelea kupata mkopo huo.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Spika, ni kweli kama nilivyosema kati ya bilioni 1.5 zilizolipwa ni milioni 765 kwa hivyo zaidi ya asilimia 50 bado hazijalipwa, lakini pesa hizi ambazo hazijalipwa haina maana kwamba hazilipwi lakini ulipaji wake unakuja kwa kila mwezi. Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa kwamba tutazidisha juhudi za kufuatilia. Mhe. Spika, tumefanya juhudi nyingi kwa wakopaji hawa ambao wamechukua mikopo hii kwa siku nyingi, tumetumia njia mbalimbali kupitia kwa Masheha hata Mashekhe na viongozi wa kidini ili kuwaeleza hatari za kukopa na kutokulipa.

Kusema kweli mikutano ile imezaa matunda kwa sababu sasa hivi ulipaji speed yake inakwenda vizuri zaidi kuliko huko nyuma. Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa ajidhatiti vizuri na kuhakikisha kwamba wale wote wanaodaiwa wote wanalipa, na kupitia chombo hichi ambacho leo natoa taarifa hii naomba wajitahidi kulipa kwa sababu wakilipa wao na wengine ndio watafaidika.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Kwanza namshuru sana Mhe. Waziri kwa kujibu maswali yake vizuri na naamini kama amejipanga vizuri kwa ajili ya kujibu haya maswali.

Napenda nimuulize kwa sababu ametwambia kwamba kuna fedha kiasi cha milioni mia sita na zaidi zimesharudishwa kwa wale waliokopa na wameshazirudisha. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri

(a) Jee, wakati huu kwa sababu fedha zile zimesharudishwa huu utaratibu wa kuwakopesha wengine unaendelea au wamesitisha mpaka zirudishwe zote.

(b) Kama wamesitisha je, ile dhima ya kuwa wanakopeshwa wananchi ili kuwakwamua kiuchumi itakuwa inaendelea au itakuwa imesita.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika**: Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia mikopo hii itaendelea kutolewa hilo la kwanza. Lakini la pili kwenye jibu langu (d) nilisema kwamba sasa hivi tunakamilisha taratibu na Benki Kuu ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ili zile fedha za AK JK zije huku kwetu, ili tuziratibu sisi ili ziweze kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi, na waweze kuzifanyia kazi kwa mujibu ambavyo sisi tumepanga mipango yetu.

Mhe. Spika, lengo la serikali hii ni kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi. Napenda nimuhakikishie kuanzia mwezi wa Julai mikopo hii itaendelea kutolewa. Kwa sababu tayari tumeanzisha na Mfuko wa Uwezeshaji ili kuwarahisishia wananchi kutatua matatizo yao.

**Nam. 92**

**Mkataba wa Udhamini wa Mchezo wa Soka Kutoka TBL**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:

Mhe. Spika. mnamo mwezi wa Aprili mwaka huu Chama cha Soka Zanzibar kimeripotiwa kusaini Mkataba wa miaka 3 kwa udhamini wa Mchezo wa Soka kutoka Kampuni ya TBL kupitia kinywaji chake cha Grand Malta.

(a) Je, Serikali imejitayarisha vipi kuhakikisha vilabu vinanufaika na fedha hizo.

(b) Kwa kuwa Sera ya Michezo Zanzibar inakataza Udhamini wa Pombe, Je, ZFA imezingatia vipi Sera hiyo kwa vile kinywaji cha Grand Malt kinatengenezwa na kampuni Mama inayotengeneza Pombe ya TBL Tanzania.

(c) Kukubali Udhamini huo kabla ya kubadilisha Sera ya Michezo, Serikali haioni ni sawa na kukataa kula nguruwe na kukubali kunywa mchuzi wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo -** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nikubali kwamba Chama cha Soka cha Zanzibar (ZFA) kimetiliana saini na kampuni ya TBL kupitia kinywaji chake kisichokuwa na ulevi Grand Malta mkataba wa miaka mitatu (3) wa udhamini wa ligi kuu ya soka Zanzibar. Baada ya kutoa uthibitisho huo sasa naomba kumjibu swali hilo kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika kupata udhamini huu serikali kupitia Baraza la Taifa la Michezo imekuwa karibu sana na ZFA tokea hatua ya awali ya ushughulikiaji wa maombi ya udhamini huo. Pia kufanya jitihada za kuweka wazi udhamini huo, ili kila mdau vikiwemo vilabu vitavyoshiriki ligi kuu ya Zanzibar. Vilevile haki na fursa wanazostahiki na hivyo kuondosha utata usijitokeze miongoni mwa wadau wa udhamini huu.

   Mhe. Spika, serikali kupitia Baraza la Taifa la Michezo imejidhatiti kuhakikisha fedha zitakazotolewa na wadhamini zinanufaisha vilabu vya Zanzibar vilivyokusudiwa. Kwa kuwa mkataba uliofungwa unazungumzia kasma itakavyotolewa kwa kila timu itakavyoshiriki kwenye ligi Kuu ya Zanzibar, kitakachotekelezwa na Baraza la Michezo ni kuhakikisha mkataba huo unatekelezwa ipasavyo kwa timu kupata haki inayostahiki. Hivyo ni kusema kwamba Baraza la Taifa la Michezo kupitia kamati husika litakuwa karibu wakati wote wa utekelezaji wa udhamini huu hadi msimu wa ligi kuu kukamilika.

b) Mhe. Spika, lengo la Serikali kukataa udhamini wa Pombe ni kuwaepusha vijana kutumbukia katika athari zinazotokana na ulevi. Ndio maana ikapigwa marufuku udhamini wa pombe ili kuepusha matangazo ya ulevi michezoni. Hivyo, kukubali udhamini huo ZFA haikwenda kinyume na Sera iliyopo ya michezo.
   Mhe. Spika, kinachokatazwa michezoni si jina la kampuni bali ni matangazo ya ulevi. Kwa kuwa kitakachotangazwa katika udhamini huo ni kinywaji cha Grand Malta ambacho hakileweshi, uamuzi huo hauwezi kulinganishwa kabisa na dhana ya kukataa kula nguruwe na kukubali kunywa mchuzi wake.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kusikitisha ya Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa serikali imeruhusu udhamini wa pombe kupitia mlango wa nyuma. Utakubaliana nami Mhe. Naibu Waziri suali langu namba ( c) lililosema kwamba serikali haioni sawa kukataa kula nguruwe na kukubali kula mchuzi wake. Kampuni ya TBL ni Kampuni Mama iuzayo Grand Malta.

(a) Je, una uhakika gani pesa hizo watakazopewa wachezaji zinatoka kwenye Kampuni ya Grand Malta. Tumezowea hapa kuna Kampuni ya Cocacola inazalisha Sprite na Fanta lakini Kampuni mama ni Cocacola. Kwa hivyo utakubaliana na mimi msemo wangu wa kula nguruwe na kukataa mchuzi.

(b) Mhe. Naibu Waziri kuna msemo unasema mgeni fika mwenyeji apone, kuna timu zimeshuka daraja nazo zinalia kilio hichi. Je, kuna msamaha gani juu ya timu hizi Kikwajuni, Polisi na Mundu.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): :** Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa idhini hii na mimi kujibu suali la nyongeza. Kwanza Waheshimiwa Wajumbe kuelewa kwamba hii Kampuni ya TBL ni kampuni tanzu, kwa maana ina mambo mengi, inazalisha vinywaji ambavyo vina kilevi na vinywaji ambavyo havina kilevi. Sawa sawa na baba ambae ana watoto wengine Waislamu wengine Wakristo. Sasa sisi tulichokifanya tumeamua kumuoa yule ambae kasilimu ambaye ni Muislamu. Nafikiri hakuna ubaya, tena unaambiwa mtu kama huyo muoe haraka sana.

Sasa sera inasema kuimarisha michezo na michezo tunaiimarisha kwa kuwatafuta wafadhili, yaani wadhamini wa *league* yetu. Hatuwezi, lazima tuseme ukweli kwamba kwa bajeti zetu, hatuwezi kudhamini michezo au *league* zetu ndio maana tukenda kutafuta TBL.

Mhe. Spika, mimi nilipokuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nilikwenda mimi mwenyewe binafsi kwenda kuiomba kampuni ile, baada ya kuona kwamba baba yule kumbe ana watoto Waislamu. Kwa hivyo, mimi nilimtaka yule Muislamu nikamuowa, kwa hivyo nafikiri sio kosa. Tulifanya hivyo, hata timu yetu ya Baraza la Wawakilishi tulidhaminiwa na hao hao TBL, kinywaji ambacho hakina *alcohol* ndani yake, kwa hivyo hakuna ubaya wowote. Yeye Mhe. Mjumbe alikuwa golikipa huyu.

Suala la timu ya Kikwajuni. Mimi nafikiri angekaa akazungumza na ZFA, kwa sababu bila shaka watakuwa wamefuata taratibu ambazo wenyewe wanazo. Ajaribu kukaa na ZFA ili aone ni vipi anaweza kuirejesha timu ya Kikwajuni katika hadhi yake, ahsante sana.

**Mhe. Spika**: Hivi udakaji wa Mhe. Jaku siku ile ulikuwa mzuri kutokana na msaada wa hawa ndugu zetu.

**Mhe. Hija Hassan Hija**: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize maswali mawili yafuatayo.

Mhe. Spika, mimi naomba serikali itusaidie hasa inakataa nini? Inakataa michezo kudhaminiwa na kampuni ambazo zinazozalisha bia au inakataa michezo kudhaminiwa na wanywa bia.

Swali la Pili katika mechi ambazo tulifungwa magoli matano ambapo golikipa alikuwa ni Mhe. Jaku na nambari sita alikuwa ni Mhe. Jihad kwa Baraza la Wawakilishi, sote tulivaa fulana ambazo zimedhaminiwa na kampuni hiyo na bahati mbaya nembo yake hasa ilikuwa ni ile ya bia ingawa jina lilikuwa ni Grant Malt.

Sasa serikali haioni na kwa kuwa wizara hii ni wizara ya michezo, utamaduni na utalii, na utalii huko kuna mambo makubwa zaidi kuliko hayo ya bia. Kweli serikali inafanya hadaa mbele ya kisheria.

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hija Hassan Hija.

Kwa kweli kinachokatazwa hapa ni michezo yetu kudhaminiwa na vinywaji vyenye ulevi. Ninafikiri nilitoa mfano huo kwamba kweli hii kampuni hii inazalisha ulevi lakini wakati huo huo inazalisha vinywaji vilivyokuwa baridi na si vibaya kwenda kutafuta kile kinywaji baridi ambacho hicho kitakachotumika kutudhamini katika michezo yetu. Kwa hivyo ninafikiri hilo si tatizo kabisa.

Jengine ni kwamba tulivaa jezi ambazo zimeandikwa alama hiyo, ni kweli lakini tulichosema ni hapa ndani ya visiwa vya Zanzíbar, ile mechi tulicheza Tanzania Bara na sio hapa.

**Nam. 7**

**Ufutwaji wa Matokeo ya Kidato cha IV Kwa Skuli Za Zanzibar**

**Mhe. Ali Salum Haji** - Aliuliza:-

Baada ya kutangazwa matokeo ya Kidato cha Nne (*Form Four*) kwa mwaka wa 2011, imeonekana skuli nyingi zimefutiwa matokeo.

(a) Je, ni skuli ngapi za Tanzania zilizofutiwa matokeo.
(b) Je, ni skuli ngapi za Tanzania Bara, Unguja, na ngapi za Pemba zimehusika na kufutiwa matokeo hayo.
(c) Je, ni kigezo gani kilichotumika kufuta matokeo ya skuli hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 7 lenye sehemu (a), (b) na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

Ni kweli kuwa baadhi ya watahiniwa wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne iliyofanyika mwezi wa Oktoba 2011 wa skuli mbali mbali za Tanzania walifutiwa matokeo yao ya mitihani baada ya kubainika kufanya udanganyifu katika mitihani hiyo, Jumla ya watahiniwa 3,303 walifutiwa matokeo yao. Kati ya waliofutiwa matokeo, watahiniwa wawili (02) ni wa mtihani wa Maarifa na watahiniwa 3,301 wa mtihani wa kidato cha nne.

Kwa upande wa Zanzibar watahiniwa 1,010 wa skuli za serikali na za binafsi walifutiwa matokeo hayo.

Baada ya maelezo hayo sasa Mhe. Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

a) Watahiniwa katika skuli 83 za Tanzania ndio waliofutiwa matokeo yao.
b) Watahiniwa waliofutiwa matokeo yao wametoka katika skuli 53 za Tanzania Bara na 30 za Zanzibar. Kati ya Skuli za Zanzibar skuli 24 ni za Unguja na 6 za Pemba. Kati ya skuli 24 za Unguja zimo skuli 6 za binafsi.

c) Watahiniwa waliofutiwa matokeo yao walibainika na makosa mbali mbali ikiwemo watahiniwa kuwa na mfanano mkubwa wa majibu usio wa kawaida na *notes*", kukamatwa na simu ndani ya chumba cha Mtihani, kufanyiwa mtihani na watu wengine, Watahiniwa kubainika wamesajiliwa kufanya mtihani kwa kutumia majina ya watu wengine, kubainika kuwa na *script* zenye miandiko tofauti au kuwa na miandiko tofauti katika *script* ya somo moja.

Vile vile baadhi ya watahiniwa kukamatwa wakibadilishana karatasi za maswali/vijitabu vya kujibia mtihani ili kuandikia majibu ili kuandikiana ndani ya chumba cha mtihani, watahiniwa kukamatwa na *booklet* zaidi ya moja ambapo *booklet* moja hakupewa na msimamizi, watahiniwa kubainika kuwa na kesi mbili tofauti; kama vile mfanano wa majibu, *notes*, kijitabu cha kujibia zaidi ya kimoja na kubadilishana karatasi ya majibu au kijitabu cha kujibia ndani ya chumba ya mtihani.

**Mhe. Ali Salim Haji:** Ahsante sana Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Spika, mimi nina maswali madogo tu ya nyongeza.

Kuna fununu kuwa baadhi ya wanafunzi ambao mwanzo walifutiwa matokeo yao baadae kwamba kulitokea marekebisho ya kufanyiwa na matokeo yao kupata upya. Jee, hili ni kweli na kama ni kweli ni kigezo gani kilichotumika mwanzo kufutiwa na baadae kupatiwa matokeo yao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali**: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi anachokizungumza ni kweli, kuna wanafunzi wa *form six* na sio *form four* kama swali lake la msingi liliuliza, wamefutiwa matokeo yao na baada ya Baraza wanaita Baraza la Wakuu wa Skuli za Kiislamu kule Bara wana Baraza lao, kukata rufaa katika Baraza la Mitihani ikabainika kwamba ni kweli wanafunzi hao kuna makosa ambayo ya matokeo.

Na moja ya makosa ambayo Mhe. Spika, yametokea mara nyingi mitihani hii ilikuwa ikitolewa kwa *papers* tatu, wanajibu *papers* tatu wanafunzi. *Process* zao za kutiwa maksi zilikuwa zinagaiwa kwa *papers* tatu vile vile.

Mara hii wakaja na mfumo mpya ambao ulikuwa bado hawajaubadilisha katika system, wakaleta *papers* mbili, matokeo yake wakagawa *papers* mbili kwenye *system* ya *papers* tatu. Kwa hivyo bila shaka mparaganyiko hapo ukaanza na maksi za wanafunzi zinarudi chini. Baada ya Kamati hii wanaita Baraza la Wakuu wa Skuli za Kiislamu kukaa na kukata rufaa, wakenda kwa Katibu Mkuu wa NECTA ikaonekana kama makosa yamefanywa na Mhe. Spika, marekebisho yakafanywa na maksi za wanafunzi zimepanda baada ya marekebisho hayo kufanywa.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.
Mhe. Naibu Waziri katika kadhia hii bila shaka kuna watu ambao watahusika kwa njia moja au nyengine. Jee, wizara yako inachukua hatua gani kwa watu hao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ninakushukuru sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Shadya kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli Mhe. Spika, katika kadhia hii ni lazima kutakuwa kuna watu watakuwa wamehusika na kama ambavyo nimejibu swali katika kipindi kilichopita. Mara tu Mhe. Spika, baada ya matokeo haya kutokea kama wizara yangu sisi wenyewe tuliunda kamati yetu ya ndani ambayo ilikuwa na wajumbe sita, kuhakikisha kuwa yale matokeo ambayo yametolewa ni kweli wanafunzi walikopi, wizara tukajiridhisha kwamba ni kweli matokeo ambapo yamatokea watoto wetu kufutiwa mitihani ilikuwa ni halali kufutiwa.

Lakini vile vile Baraza la Mitihani (NECTA) waliunda kamati na kamati hiyo tayari imemaliza kazi yake na ripoti kama wizara tumewasilishiwa juzi.

Mhe. Spika, ninachotaka kuahidi ndani ya Baraza lako tukufu, kwanza tulitoa barua kwa wale wote ambao NECTA walituletea wanahusika na kadhia hii ili wajieleze. Baada ya hapo Mhe. Spika, kuna hatua ambazo tutazichukua. Hizo hatua Mhe. Spika, zitakuwa ni tofauti.

Kuna wale ambao tutawanyang'anya madaraka ambayo walikuwa wanayo. Kwa mfano wasimamizi wa mitihani ni mara nyingi ni walimu wetu wakuu, wale ambao tumebaini wameshiriki kwa njia moja au nyengine basi tutawaondoa katika dhamana ya walimu wakuu. Kwa sababu kama wewe ni mwalimu mkuu umeaminiwa na hujiaminishi, huwezi kutufaa.

Mhe. Spika. Lakini la pili, hatutowaruhusu tena yeyote atakayekutikana na kadhia kusimamia tena mitihani yetu. Lakini la tatu ambao Mhe. Spika tunalichukulia hatua, mitihani hii ilikuwa haihusishwi moja kwa moja na wizara yetu ya elimu. Ilikuwa ikipelekwa mikoani, kamati za mikoani ndizo zilizokuwa zikisimamia mitihani ile.

Sasa Mhe. Spika, kwa kuona kadhia hii tumezungumza na wenzetu wa Baraza la Mitihani kuwa sasa mitihani yote tusimamie wenyewe wizara ya elimu na isiende tena kule mikoani. Kwa hivyo jengine ambalo tunalichukua hatua ni kuhakikisha Mhe. Spika, mitihani hii tunaisimamia sisi wenyewe wizara ya elimu.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali (a) na (b) la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Utakubaliana na mimi kuwa wapo baadhi ya watoto ambao hali zao ni duni na wazee wao ni hivyo hivyo, wamewasomesha kwa muda wa miaka 12 na hatimaye kufutiwa matokeo yao. Na kuna watoto ambao hadi hii leo wamepatwa na mshtuko wa maradhi kukosa kusoma na kuendelea. Jee, Mhe. Naibu Waziri unawaeleza nini wazee na wanafunzi hao.

Lakini pili, jee wale ambao wamefutiwa matokeo yao kuna utaratibu gani wa kiserikali au wizara kuwaonea huruma alau kuwapatia vyeti vyao ili waweze kujiendeleza.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali**: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeze lenye (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, mimi ninataka nikubaliane na yeye kama kuna wazee na wanafunzi ambao wameathirika na hili, kwa sababu tokeo limetokea na wanafunzi wamefutiwa mitihani yao. Lakini ninataka nimuhakikishie sio wazee na wanafunzi tu na hata sisi wizara ya elimu tumeathirika na matokeo haya.

Lakini Mhe. Spika, tungefanya nini wakati jambo limefanyika na tumethibitisha kama wizara ya elimu kuwa jambo limefanyika. Mhe. Spika, hili naomba nitoe wito kwa wazazi, jamani siku hizo kumekuwa na utapeli wa mitihani. Mitihani imekuwa ni biashara ndani ya nchi yetu.

Kwa hivyo wazee wasishiriki kuwapa nguvu hawa matapeli ambao matokeo yake mwisho wa siku hawasaidii watoto wetu wanawaangusha kimitihani. Kwa sababu Mhe. Spika, hili jambo lina pande nyingi na hata wazee wenyewe wanashiriki kwa sababu katika kununua hii mitihani ambayo ni feki. Moja ni hilo.

Lakini suala la pili ambalo amelizungumza Mhe. Spika, sheria ya NECTA mwanafunzi akifutiwa mtihani miaka mitatu anatakiwa asifanye mtihani. Lakini wizara ya elimu kwa kuliona hilo wakaona kwa kweli itakuwa ni mzigo mkubwa na itakuwa ni *crisis* ndani ya nchi. Kwa sababu miaka mitatu hasa kwa mwanafunzi mwanamke basi si rahisi kuweza kukaa miaka mitatu akasubiri kufanya tena mitihani.

Matokeo yake mwanafunzi yule anaweza akaolewa au akaingia katika gengi lolote halitomletea maslahi. Kwa hivyo tulikaa na wenzetu tukazungumza nao na matokeo yake tumekubaliana badala ya miaka mitatu basi ile adhabu iondolewe na sasa imeekewa mwaka mmoja, utakapomaliza mwaka mmoja watakuwa tayari wanaweza kufanya mtihani Mhe. Spika.

**Nam. 77**

**Nyumba za Kuishi Viongozi wa Kitaifa**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa miaka mingi ilikuwa na nyumba zake za kuishi viongozi wakiwemo wa Kitaifa.

(a) Sababu gani zilizopelekea wasiishi katika nyumba za Serikali na kuanza kuishi katika nyumba za kukodi kwa watu binafsi.

(b) Serikali inatumia kiasi gani kwa mwaka kulipia gharama za nyumba za kukodi wanazoishi viongozi wake.

(c) Serikali ina mpango gani wa kuzitengeneza nyumba za viongozi zikiwemo za Mazizini, Migombani na Chake Chake ambazo zinakabiliwa na uchakavu mkubwa na nyengine zimo katika hatari ya kuanguka.

(d) Je, ni nyumba ngapi za Serikali ambazo wameuziwa viongozi mbali mbali na sababu gani zilizopelekea kuuzwa na kusababisha viongozi kuishi katika nyumba za kupanga.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 77 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Ni kweli kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa miaka mingi ilikuwa na nyumba zake za kuishi viongozi wakiwemo wa Kitaifa, lakini matatizo yaliyojitokeza ni mawili, la kwanza ni kuwa baadhi ya viongozi wamekuwa na tabia ya kutokuhama katika nyumba za Serikali baada ya muda wao wa uongozi kumalizika na la pili ni kuwa nyingi katika nyumba hizo za viongozi ziko katika hali mbaya. Kwa hivyo Serikali inafanya utaratibu wa kuwahamisha viongozi hao ili kuzifanyia matengenezo nyumba hizo.

b) Gharama kamili za nyumba za kukodi kwa viongozi hili si jibu la kujibiwa moja kwa moja kwa sababu kila Wizara huwa inawagharimia kuwalipia gharama viongozi wao wenyewe.

c) Kama tulivyoelezea kuwa hivi sasa Serikali inaandaa mpango maalum wa kuzifanyia matengenezo nyumba zote za viongozi ambazo ziko katika hali nzuri na zile zipo katika hali ya mbaya kuzibomoa na kutoa nafasi ya kujenga nyumba nyengine katika maeneo hayo.

**(d)** Mhe. Spika**,** swali hili tunalifanyia marekebisho na tutalijibu kama linavyostahiki hapo baadae.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, mimi nina maswali manne (a), (b), (c) na (d)

Maswali niliyopata ni mawili jee nikupe muda zaidi pamoja na hayo sababu zilizopelekea nyumba aliyokuwa akiishi Makamu wa Kwanza wa Rais hapo Maisara na kuhamishwa na kupelekwa katika nyumba ya kukodi.

(a) Huoni serikali inatumia matumizi yasiyokuwa ya lazima.

(b) Ni viongozi wangapi wa kitaifa ambao hawana nyumba wanalazimika kupangishwa nyumba na lini tatizo hilo litamalizika.

(c) Kwa kuwa serikali imekiri nyumba nyingi ni chakavu, nani dhamana wa nyumba hizo na viongozi wangapi ambao waliomaliza muda wao mpaka hivi sasa hawajahama katika nyumba hizo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati**: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama hivi ifuatavyo.
Kwanza ninaeleza kwa masikitiko kwamba maswali ambayo mimi nimeyapata yalikuwemo matatu, lakini katika *order paper* tumeyakuta manne, sasa swali la (d) hatukuwa nalo na kwa maana hiyo hatukutengeneza jibu.

Lakini hata hivyo tunachukua nafasi hii kwamba tutamjibu hili swali lake kwa maandishi kama alivyosema mwenyewe atatupa muda wa kutosha tutamjibu vizuri kwa maandishi.

Swali jengine ni kwamba Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alikuwa akikaa *Bosnia* hapa Mnazi Mmoja-Maisara. Lakini unapokuwa una nafasi kubwa kama ya Makamu wa Kwanza wa Rais unatakiwa muda mrefu upate nafasi ya kutosha ya kutafakari kazi zako. Tatizo ambalo lipo *Bosnia* ni kwamba pale kuna wapiga mziki wanaanza saa tatu usiku mpaka liamba na kelele zinakuwa kubwa sana pale pahala. Kwa hivyo tunashukuru mwenzetu yule alistahamili kwa muda mrefu mpaka hatimaye ikabidi tutamtafutie nyumba aende akakae aondoke katika mazingira yale ambayo kidogo pale kuna matatizo.

Ni eneo lile ukitazama kuanzia pale *Bosnia* mpaka ukaja huku Kilimani kwa huyu Raju kuna makelele mengi sana. Kwa hivyo kwa kweli tumeamua kumuhamisha na tumemueka huko ambapo tulikomueka hivi sasa.

Swali jengine ni kwamba nani ni mwenye dhamana ya kutengeneza nyumba za serikali. Mhe. Spika, nyumba za serikali ambazo wanakaa mawaziri zipo katika makundi mawili kwa matatu. Kuna nyumba zipo chini ya dhamana ya Mji Mkongwe, Idara ya Ardhi na kuna nyumba zipo chini ya dhamana ya wizara zenyewe.

Kwa hivyo hili swali la nne alilouliza hili ndio tutajua nani anakaa katika nyumba ya Mji Mkongwe, katika nyumba ya dhamana ya serikali yenyewe na nani anakaa katika nyumba inayomilikiwa na Idara ya Nyumba.

Kwa hivyo nyumba anayokaa katika Idara ya Nyumba mtengenezaji ni Idara ya Nyumba, nyumba iliyokuwa dhamana ni wizara wenyewe ni wizara yenyewe na nyumba iliopo katika Mji Mkongwe mtengenezaji ni Mji Mkongwe mwenyewe.

Halafu swali lake la nne ni kwamba baada ya kumjibu swali lake la nne ndio tutajua ni nani anaishi katika yake na nani anaishi katika nyumba ya serikali.
Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub**: Mhe. Spika, ninataka kujua ni viongozi wangapi wanaishi katika nyumba za kupanga na lini tatizo hili litamalizika.

**Mhe. Spika:** Yaani hili lilikuwa halijajibiwa.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati**: Mhe. Spika, tumeshalijibu kama angelisikiliza vizuri ni kwamba swali lake la nne linazungumzia suala hilo kuwa nitalijibu kwa maandishi.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk**: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kumuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwa majibu ambayo amejibu Mhe. Waziri hapa ametufafanulia kuwa kuna idara tofauti ambazo zinamiliki mawaziri hao. Lakini Mhe. Naibu Waziri amejibu swali amesema kuwa wanatambua kuwa kuna waheshimiwa huku wameshastaafu kazi lakini bado wanang'ang'ania nyumba hizo kukaa. Jee, Mhe. Waziri katika hao ambao wamo katika uwezo wako wa wizara na kama wamo jee una hatua gani ya kuchukua ya kuwaondoa mara moja ili kuokoa kodi ya mapato ya wavuja jasho.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli kuna baadhi ya wenzetu ambao tulikuwa tukifanya kazi kwa pamoja lakini sasa si mawaziri tena wamebakia katika nyumba zile za serikali. Tulichokifanya ni kuwasiliana nao watupishe katika zile nyumba kwa madhumuni ya kuwapa mawaziri wengine au kama inahitaji kufanyiwa matengenezo tufanye matengenezo, hilo ndilo tunalolifanya.

Tunataka tuweke mkazo zaidi na kwa sababu tunajua wao ni watu wazima hawatategemea mpaka tupeleke Polisi kutoa vyombo nje na nini, hilo hatolifanya. Lakini ninajua. Wajumbe wameuliza maswali basi na wenyewe wanasikia huko basi ni bora watupishe ili tuendelee na kazi vizuri. Ahsante.

**Mhe. Salmin Awadhi Salmin**: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema sababu ya kumuhamisha Makamu wa Kwanza wa Rais pale alipokuwa akikaa *Bosnia* ni kwa sababu hapana utulivu.

Sasa swali ninataka kumuuliza hapa alipohamia sasa hivi Makamu wa Kwanza wa Rais yeye anapafahamu.

Lakini la pili, atakubaliana na mimi hapo alipohamia hivi sasa hapana utulivu kuliko hapo alipohama.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati**: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Niseme kwamba anapoishi Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Waziri anapafahamu na ni pahali ambapo pana utulivu na pahali pazuri sana ambapo hapana tatizo lolote.

**Mhe. Spika:** Kabla ya kuendelea tulichelewa kuwakaribisha vijana wetu lakini hii leo tuna wageni ambao ni wanafunzi jumla yao ni 26 kutoka Skuli ya SOS hapa Zanzíbar.
Wamefuatana pamoja na mwalimu wao wapo pale juu naomba wasimame.

Hawa ndio wageni wetu kwa leo wamekuja kuona wazee wao wanafanya nini kwa ajili yao. Karibuni sana.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tunafungua mjadala leo, baada ya hoja iliyowasilishwa siku ya Jumatano tarehe 13/06/2012 kuungwa mkono kumaanisha kwamba sasa tujadili. Nimuombe basi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, kuja ili kutoa hotuba kwa niaba ya Wenyeviti wenzake. Baadae Mhe. Rashid Seif.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti):** Mhe Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti, naomba kusimama mbele yako kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Wenyeviti, kuhusu mapitio ya hali ya uchumi na mipango ya maendeleo ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, kwanza sote hatuna budi kumshukuru M/Mungu kwa kutujaalia kukutana tena hapa tukiwa wazima kabisa na wenye afya njema, kuja kuwatumikia wananchi wetu waliotuchagua.

Pili, nikushukuru na wewe mwenyewe binafsi Spika wetu mpendwa kwa kunipa nafasi ya mwanzo kuwasilisha ripoti yetu ya kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Baraza lako tukufu la Wawakilishi hapa Zanzibar. Ili kuichangia Hotuba ya Bajeti ya SMZ iliyowasilishwa na kipenzi chetu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar, Mhe. Omar Yussuf Mzee.

Tatu, nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi kwa kutupa dhamana ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati za Wenyeviti, na leo nawasilisha ripoti hii kwa niaba yao wote.

Nne, nawashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kutuamini na kutupa dhamana ya kuwatumikia ndani ya chombo hiki ili kulinda maslahi yao hapa Zanzibar.

Pia tunawashukuru wafanyakazi wote wa Baraza lako la Wawakilishi hapa Zanzibar kwa msaada mkubwa wanaotupa na wanatupatia wakati wote tunapohitajia, tunaomba waendelee na moyo huo huo.

Mwisho kabisa, shukurani zangu kubwa zaidi nazitoa kwa waandishi wote wa Habari, wa TV, Magazeti, Radio, pamoja na Wapigapicha wote kwa kutuwezesha kufikisha habari zetu kwa wananchi wote tunawashukuru sana kwa hilo**.**

Mhe. Spika, kamati yangu ilipitia Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ilitoa maoni mbali mbali kwa Serikali, ili kuiboresha na leo pia tutaongeza michango zaidi kama itakavyofuata muda huu. Aidha, naomba niwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa michango yao ya kina waliyoitoa kwa serikali wakati Kamati yetu ilipokuwa inaijadili hoja hii.

Lakini Mhe. Spika, naomba uniruhusu niwataje Wajumbe wa kamati hii, walioijadili bajeti ya serikali.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Ali Abdalla Ali | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Asha Bakari Makame | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Amina Idd Mabrouk | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Omar Ali Shehe | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Salmin Awadh Salmin | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Nassra Awadh Salmin | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Ramadhan Kh. Masoud | - | Katibu |

Mhe Spika, kwa kuanzia, tunaungana na kauli ya Mhe Waziri, kwa Serikali kutimiza matakwa ya katiba (Kif. 105) kwa kuwasilisha Bajeti kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na huu ndio utekelezaji wa utawala bora, kama MKUZA Klasta ya tatu inavyoeleza suala la Utawala Bora, kwani sote tunatakiwa kufuata katiba. Kwa hiyo, pia tunaitaka serikali kutekeleza (kif.61 (2) cha katiba ya Zanzibar, kinachotaka kuteuliwa kwa Wakuu wa Mikoa na kabla ya kuanza kazi zao ni lazima wale kiapo cha kuitii katiba inayoiongoza nchi, kwa kuwa leo tunapitisha matumizi ya Serikali na wao wakiwamo katika Utumishi wa Umma, basi ni vyema Katiba itekelezwe kama inavyo taka, vinginevyo hata wananchi wetu watashindwa na wao kuitii hii katiba yetu ya Zanzibar, kwani hakuna aliye juu ya sheria.

Mhe Spika, kamati yangu inampongeza sana Mhe Rais wa Zanzibar, D.k Mohammed Ali Shein kwa kuendelea kutuongoza kwa amani na utulivu hapa nchini. Pia tunampongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa kuwa muelewa na msikivu kwa hoja zetu nyingi tunapoishauri Serikali, katika mianya ya ukwepaji kodi na uvujaji wa mapato ya Serikali na matunda yake tumeanza kuyaona, ingawa kwa kasi ndogo kwani taasisi za kodi zimevuka malengo waliojiwekea lakini bado kuna baadhi ya maeneo yanahitaji kuwekewa mkazo ili kuziba kabisa uvujaji wa mapato ya Serikali. Lakini pia bado kuna maeneo machache Serikali yetu haikusanyi mapato kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano inavyosema, mapato ambayo yangelisaidia katika uchumi wetu.

Mhe Spika, leo kwa mshangao mkubwa tumekuja hapa kuidhinisha ukusanyaji na kuruhusu matumizi ya pesa nyingine za Umma, kwa shughuli za uendeshaji na maendeleo ya wananchi wakati baadhi ya wasimamizi wa pesa hizi tayari kupitia ripoti za kamati ulizoziunda wewe mwenyewe zimegundua usimamizi mbovu na uvujaji wa mapato wakiwa wao ndio wasimamizi wakuu katika sehemu zao, na taarifa zao tumekuletea wewe Mhe Spika, na tayari umeziwasilisha Serikalini zikiwa na ushahidi kamili. Leo hatujapokea taarifa yeyote na wala hatujaona hatua zozote zilizochukuliwa na Serikali.

Sasa nikuulize Mhe Spika, Je, zile taarifa tulizokuletea wewe hukuziamini? Au Serikali haikuziamini? Kwa kuwa kanuni zetu hapa Baraza la Wawakilishi, zinatukataza kusema uongo. Je, ni maelezo gani tuliyoletewa toka Serikalini kuwa tumelidanganya Baraza?

Mhe Spika, sisi wajumbe wako kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 88, Baraza la Wawakilishi limepewa dhamana ya kuisimamia Serikali, kuihoji na kuielekeza, lakini sasa inaonesha ni kinyume chake kuwa sasa Serikali ndio inalisimia Baraza la Wawakilishi, wanaweza kufanya lolote kwa kuamini kuwa hatuna uwezo wa kufanya chochote, hii inawapa watendaji wa Serikali jeuri na kibri kwani hawajali chochote na wanaweza kufanya lolote dhidi ya Baraza kwani Serikali inawalinda.
Mhe Spika, mimi nasikitika sana kuwa ulimega sehemu ya fedha ulizotengewa na Serikali katika bajeti yako na kuwalipa wajumbe wako, ili wakachunguze uzembe na ubadhirifu unaofanyika ndani ya taasisi za Serikali na wamegundua mambo mengi tena kwa ushahidi wa vielelezo vya maandishi na kinasa sauti ili kulinda uadilifu na fedha walizotumia wajumbe hao ikiwa ni sehemu ya kodi ya wananchi, na leo tuko hapa tena tunaendelea kutumia kodi za wavujajasho hao hao wa Zanzibar. Lakini mawazo, fikra na maamuzi tunayoyafikia, hadi sasa hatujaona dalili ya uwajibikaji kwa wahusika.

Mhe Spika, tunaomba sana Serikali yetu kuifuata katiba na Sheria tulizozitunga sisi wenyewe, na sote tulikula kiapo kwa kukamata msahafu, naomba sana Mhe Spika, tuwajibike kwa pamoja, tuache muhali, kuoneana haya kila mmoja awajibike kwa nafasi yake kwa uadilifu vinginevyo tutaendelea kutambaa badala ya kutembea.

Mhe Spika, hii ndio Bajeti ya Serikali tunaidhinisha tena matumizi kwa baadhi ya watendaji ambao hatuna imani nao, na kuendelea kusimamia taasisi walizoshindwa kuzisimamia. Aidha, kwa kukiuka maadili ya dhamana walizopewa, au ubadhirifu katika taasisi zao, tunaiomba Serikali kuchukua hatua za dharura kuhusu

suala hili ili na sisi tuamini kuwa kweli sote nia yetu kuijenga nchi yetu na sio kuwalinda watu. Vinginevyo itakuwa ni sawa na kutia maji kwenye pakacha.

Mhe Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya matumizi hasa ya maendeleo na mengine ya kawaida, tayari kunabaadhi ya wizara aidha wametumia kinyume na walivyotuahidi, na baadhi yao pia tumegundua wamekusanya pesa za umma na kuzitia mifukoni mwao. Sasa leo bado tena Serikali inataka tuendelee kuwaamini watu wao hao wakakusanye nyingine na kama kawaida yao wakazitafune tena, ah! Nadhani hata wananchi wetu watakosa imani na sisi. Sasa Mhe. Spika, naomba utumie busara zako kuilekeza Serikali ipasavyo ili tutekeleze matakwa ya katiba ya Zanzibar kuhusu ubadhirifu wa mali za Umma na nini kifanyike kabla ya kuipitisha Bajeti hii.

Mhe Spika, serikali yetu inaongozwa na CCM na chama chetu kinapiga vita kwa nguvu zote, ubadhirifu wa aina yeyote au ufujaji wa pesa za Umma, pamoja na Rushwa. Sasa siamini kama kuna mtu yeyote atakaekwenda kinyume na matakwa hayo ya Chama chetu cha Mapinduzi ambacho ndicho kinachoongoza nchi kwa sasa.

Mhe Spika, kamati yangu pia inaungana na Serikali kuwapa pole wananchi wetu wote, waliopatwa na janga la kuzama kwa meli ya MV SPICE ISLANDER iliyozama siku ya Tarehe 10/08/2012 kwa uzembe uliosababishwa na tamaa ya kutowajibika kwa viongozi wakuu wa Wizara ya Miundombinu, katika kusimamia majukumu yao kwa kujua kuwa chochote kitakachotokea wao hawatoathirika kwa lolote, *(BUSSINESS AS USUAL).*

Mhe Spika, kamati yangu inasikitika kwa wajumbe wako walipozuiwa na Serikali kuzungumzia tukio lile hapa Barazani baada ya kuzama kwa Meli ile eti kwa kwa sababu kumeundwa tume, wakati kanuni zetu hapa Barazani hazituzuii kuzungumzia jambo lolote, isipokuwa suala hilo liweko Mahakamani. Haya ndio baadhi ya yale niliyoyazungumza mwanzo kuwa Serikali ndio inayolisimamia Baraza la Wawakilishi badala ya Baraza kuisimimia Serikali. Kama kawaida na kwa hivi sasa wakati tume hiyo ilipomaliza kazi yake, haraka suala hilo likapelekwa Mahakamani kwa hiyo hivi sasa pia kwa mara nyingine tena hatuwezi kulijadili tena kwa kuwa suala hili liko Mahakamani. Lakini tukitaka tusitake wananchi wetu wengi wameathirika kutokana na tukio lile, wengi wao wamebaki Mayatima, Wajane, Wagonjwa, na wengine kupoteza mali zao na hakuna njia ya kuwarejeshea mali zao kwa fidia ya aina yeyote, ingawa waliohusika wanaendelea kupiga tai, wao na familia zao.

Mhe. Spika, lakini kwa taarifa tulizozipata ambazo Serikali haikututhibitishia kuwa tajiri mwenye meli yeye tayari alikwishakulipwa na Bima, nadhani hivi sasa anatafuta meli nyengine. Mhe Spika, hii inatupa fundisho sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuleta mswada wa sheria utakaowalinda wananchi wetu, pindi inapotokea ajali ili na wao waweze kupata fidia ya kisheria na sivyo kama ilivyo sasa kufikiriwa tena kama kipo hicho cha kufikiriwa, kwani sisi hapa wametuleta wao wananchi na tunapaswa kutunga sheria za kulinda maslahi yao na ni vyema kuwalipa fadhila zao.

Mhe Spika, pato la taifa, kweli tunakubali kuwa pato la taifa limekuwa kwa mwaka unaomalizika na kipato cha mwananchi kimekuwa, kama ilivyoelezwa na waziri, hasa kutokana na kupanda kwa bei ya karafuu na kuongezeka kwa watalii kumesaidia sekta ya huduma kuimarika kwani utalii unatija kwa njia tofauti, huongeza kipato na ajira kwa wananchi. Lakini pamoja na kipato cha mwananchi kukua hakiendani na kasi ya mfumko wa bei za bidhaa kuanzia chakula na vifaa vya ujenzi n.k.

Mhe Spika, pamoja na bei ya karafuu kupanda, sio watu wote ambao wana mikarafuu hapa Zanzibar, kwani ukiangalia hata hiyo mikarafuu iko zaidi katika baadhi ya mikoa tu ya Zanzibar. Wazanzibari mazingira yao ya kiuchumi yanatofautiana sana, kuhusu kuongezeka kwa watalii hapa tunapata fundisho sote Wazanzibari kulinda amani iliyopo, kwani tukianza kuvuruga amani hii hapa nchini, basi watalii hawatokuja na mapato ya serikali yetu yatapungua.

Mhe Spika, kukua kwa pato letu la taifa pia kunatokana na kuongezeka kwa uwekezaji, ikiwemo ujenzi wa barabara, viwanja vya ndege, ujenzi wa maskuli, mahoteli, viwanda n.k. Lakini bado haturidhiki na kasi ndogo ya ujenzi wa miundombinu hasa ya barabara, hatuelewi tatizo ni nini, kwani miradi yote kabla ya ujenzi hufanyiwa upembuzi yakinifu na zinapotolewa *tender* kila kitu kinajieleza. Kitu cha kushangaza kuna barabara tena za kilomita chache zimeanzwa kujengwa tangu mwaka 2008 hadi leo bado hazijakamilika, na zilitolewa ahadi kumalizika nyengine kabla ya uchaguzi mkuu uliopita, hasa barabara zinazosimamiwa na Kampuni ya MECO. Hivi sasa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar, unajengwa, unasimama, nao hatujui utamaliza lini, kwani tunaelewa mradi wowote ukisimama kuna mambo mengi yatatokea, ikiwemo upotevu wa vifaa, kuongezeka bei za vifaa na bei ya ujenzi vile vile gharama za ujenzi zitatofautiana.

Mhe Spika, mfumko wa bei kwa mwaka uliopita wa 14.7 unatishia amani ya uhai wa wananchi wetu. Tumeshuhudia bidhaa za chakula kupanda bei, waziri ametupa moyo kuwa kwa mwaka huu mfumko wa bei utashuka, lakini bado mimi sikubaliani nae sana, kwani tayari katika bajeti yake ametangaza kuongeza baadhi ya kodi ikiwemo kodi ya Mafuta. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa bei ya usafirishaji itaongezeka, na bei za bidhaa zitapanda. Lakini isitoshe kinachotutia hofu zaidi ni kuendelea kwa mvutano unaoendelea baina ya Marekani na Iran kuhusu uzalishaji wa Nyuklia na tishio la kuwekewa vikwazo Iran kuhusu kuuza mafuta yake, inatishia kupanda kwa mara nyengine bei ya mafuta duniani na kusababisha bidhaa nyingi kupanda bei ambapo suala hili liko nje ya uwezo wetu.

Mhe Spika, jengine ni kupanda kwa bei ya umeme ambalo limeongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wetu, wakiwemo wafanyakazi wa serikali na wanachi wengine, kwani umeme kwa hivi sasa ni jambo la lazima kwa maisha yetu na kutokana na Serikali yetu kuwa na uhaba wa vianzio vya mapato imeshindwa kufidia gharama hiyo, kwani vitu kama hivi vya maisha ya kila siku Serikali inabidi iangalie namna ya kuwapa wanachi unafuu ili kuweza kukabiliana na kasi ya maisha. Lakini hapa Serikali naomba iangalie upya ongezeko hilo kama kweli linasababishwa na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji au kufidia wizi na ubadhirifu usio na kificho unaofanywa na watendaji wachache wa Shirika la Umeme wasioitakia mema nchi yetu kwa maslahi yao binafsi,

Mhe Spika, kwa kua sisi wajumbe wako kama kawaida yetu tukiona wizi tunasema. Katika Shirika la Umeme kuna wizi tumeugundua na wakati huo huo Shirika limechukua hatua za kupandisha bei ya umeme kwa wananchi. Sasa sisi tunaamini wamechukua hatua hiyo ili kuziba pengo la pesa walizoziiba wao sio wananchi. Kwa hiyo, tunaitaka serikali kusitisha mara moja ongezeko hilo la bei ya umeme ili kwanza kupitisha uchunguzi wa kitaalam, atafutwe mtaalam nje ya Shirika la Umeme ili afanye tathmini ya kujua je ongezeko hilo la bei ya umeme ni sahihi au ni moja katika njia za kuziba pengo hilo la pesa zilizoibiwa.

Pili, wajumbe wako tumegundua kuwa kuna baadhi ya wafanya biashara wakubwa hapa nchini, wanakwepa au hawalipi umeme na wanadaiwa pesa nyingi je! kuna utaratibu gani wa kulipa pesa hizo kuanzia tangu siku waliyoungiwa umeme? Kwani imani yetu wao ndio wanaosababisha kuongezeka kwa bei ya umeme. Sisi tunasema hii sio haki kuwa ubadhirifu ufanywe na watu wengine na adhabu ya kulipa deni walipe watu wengine. Huko nje wananchi wetu wote wanapiga kelele kupandishwa bei ya umeme, wakati huku sisi tumekuja hapa na tunapitisha bajeti ili wakaendelee kuiibia nchi na hakuna hatua inayochukuliwa na serikali, kwani tumeshazoea kufanya hivyo. Lakini kwa hili Mhe Spika, sisi tunakuahidi hatutokuwa rahisi kukubali hata kidogo kwani mchezo wao ndio mauti yetu. Mhe. Spika, serikali tunaomba iwe makini katika suala hilo.

Mhe Spika, miongoni mwa mambo yaliyosababisha mfumko wa bei ni kushuka kwa thamani ya Tshs kwa USD na kwa kuzingatia chombo kinachodhibiti mfumko wa bei ni chombo kimoja yaani Benki Kuu ya Tanzania (B.O.T), inayosimamia serikali mbili zenye uchumi tofauti, lakini zinazotoza kodi za aina moja, bila ya kuangalia vianzio vya mapato ya nchi na rasilimali zilizopo katika nchi hizo na uhuru au vikwazo vya kuzitumia rasilimali hizo katika nchi hizo mbili, na ushahidi kama nilivyosema kwenye bajeti ya mwaka uliopita, kuwa chombo hicho kiliwahi kutoa msaada wa fedha taslim kwa makampuni karibu 90 ya Tanzania Bara, kutokana na mtikisiko wa kiuchumi duniani ili makampuni hayo yasitetereke, wakati hakuna hata kampuni moja ya Zanzibar iliyopata hata senti moja, eti kwa kisingizio kuwa Zanzibar hakuna kampuni iliyoathirika kwa mtikisiko huo.

Kwa hiyo Mhe Spika, tunaomba sana chombo hichi kiangalie sana uchumi wa Zanzibar na maisha ya watu wake, kwani kutokana idadi ya watu wake kuwa kidogo, hata soko la wafanya biashara walioko Zanzibar ni dogo kutokana na idadi ya watu wake kulinganisha na walioko Tanzania Bara. Kwa hivyo, hata mauzo kwa mfanyabiashara aliyeko Tanzania Bara yanakuwa ni makubwa ukilinganisha na mauzo ya mfanyabiashara aliyeko Zanzibar. Kwa tathmini ya utaalam wa Kikwamtipura, hata ukichukulia muuza maandazi aliyeko Tanzania Bara atakuwa na uwezo wa kuuza maandazi kwa wateja wengi zaidi, ukilinganisha na yule muuza mandazi aliyeko Zanzibar kutokana na idadi ya wateja waliopo hapa Zanzibar kuwa ni kidogo. Sasa tujiulize, inakuwaje kodi kwa nchi zetu hizi ziwe sawa?

Mfano mwengine ni hata kwa mkulima aliyeko Zanzibar na ardhi aliyonayo ni ndogo ukilinganisha na aliyeko Tanzania Bara, kwa hiyo hata mavuno atakayoyapata yatakuwa tofauti. Kwa hiyo, mkulima aliyeko Tanzania Bara anaweza kujikomboa na umasikini kwa asilimia 80, lakini mkulima aliyeko Zanzibar uwezekano wa kujikomboa na umasiskini ni asilimia 20 tu.

Mhe Spika kwa vigezo hivi hakuna haja ya kumtafuta mshauri muelekezi kutoka Ulaya, kwani huyu aliyetokea Kwamtipura anatosha kabisa. Mhe. Spika, haya nimeyasema ili kuwafahamisha wale wanaopanga Mipango ya Maendeleo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kujua hali ya maisha ya Zanzibar na Tanzania Bara ni tofauti sana, kwani hata ukiangalia bei ya bidhaa zote muhimu za maisha yote ya kila siku, hasa chakula kwa

Zanzibar iko juu ukilinganisha na Tanzania Bara. Kwani bidhaa nyingi sisi tunaagizia kutoka Tanzania Bara. Kwa hesabu za haraka haraka mtumishi wa Serikali ya Zanzibar anayepokea kima cha chini, ambao ndio wengi, anapokea mshahara ambao hauzidi Shs. 150,000/-, inamaana kwa siku atumie Shs.5, 000/-, kuanzia chakula, mavazi, matibabu, makaazi, Umeme, Maji, Usafiri, pamoja na kusomesha watoto.

Ukiangalia na sisi ndani ya Baraza hili tutapitisha Sheria ya marekebisho ya kodi mbali mbali ni vyema tukaangalia na ugumu wa maisha kwa wananchi wetu. Sasa hiyo nimeelezea kwa mfanyakazi wa Serikali tu, lakini wananchi wetu wa Zanzibar na wengi wao wanaishi katika majimbo yetu, likiwemo Jimbo langu la Kwamtipura, ambao hawana kazi za uhakika za kupata hata hiyo Shs. 150,000/- kwa mwezi. Je, maisha yao yatakuwa hali gani, kwa hiyo tunaiomba serikali yetu kutafuta namna yeyote ili kuweza kuzitumia rasilimali zilizoko nchini kwetu ili ziwanufaishe wananchi wetu, kwa kuwapa unafuu wa maisha yao.

Mhe Spika, sekta ya fedha ni kweli imeimarika lakini hebu tujiulize ni asilimia ngapi ya wananchi wetu wanaitumia na kufaidika na sekta hiyo? Kwa haraka utaona zaidi ni wafanyabiashara tena wachache ndio wanaofaidika na sekta hiyo ya fedha, ukiacha wengi wasiofaidika nayo moja kwa moja, kwani wengi wa wafanyabiashara wadogo wadogo hawafaidiki na mikopo kutokana kukosa dhamana, na hao ndio walio wengi na ndio maana wengi huwa hawaoni umuhimu wa kuweka fedha zao benki.

Ingawa wafanyakazi wa Serikali na Mashirika labda wao ndio hufaidika na mikopo ya Benki na wamesaidia sana Mabenki hapa nchini kutengeneza faida kubwa, lakini mabenki hayo bado yameshindwa kuwapunguzia riba kubwa inayowatoza kwani wao ni wateja wenye *Guarantee* ya waajiri wao, hakuna njia ya kukimbia kulipa madeni yao hayo. Kama mwaka uliopita tunakuomba Mhe. Waziri ukae na watendaji wakuu wa mabenki waliokuwepo hapa Zanzibar, ili kuwapa kilio cha wafanyakazi wetu cha kuwapunguzia riba kwa sababu na wao pia ni sehemu ya wabia wao kwa zile fedha zao wanazoziweka katika benki hizo.

Mhe Spika, pia tunaitaka serikali kuyashawishi Mashirika kujenga nyumba za kuwakodisha na kuwauzia wananchi pamoja na mabenki ya kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba ili kuwawezesha wananchi wetu kupata makaazi yaliyo bora. Kwani tumeona kwa sasa kwa wenzetu wa Tanzania Bara tayari Shirika la Nyumba limeanza kujenga Nyumba za Makazi ili kuwauzia au kuwakopesha watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania. Pia kuna mabenki nayo yameanza kutoa mikopo kwa ajili ya kuwakopesha wananchi kwa ajili ya kujenga nyumba.

Mhe Spika, waziri pia katika kuongeza mapato, ameeleza kuwa serikali imekusudia kurekebisha kodi ya *Lease* ya Ardhi, ili kuendana na thamani ya soko la ardhi ilivyo hivi sasa. Lakini kamati yangu haijaridhishwa na utaratibu wa utozwaji wa kodi za *Lease* za ardhi za serikali kwani kuna ubabaishaji mkubwa uliofanywa na Wizara ya Ardhi, kwanza kufuta ovyo *Lease* zilizotolewa na Serikali na baadhi yao kulipishwa kodi ndogo ikilinganishwa na ile iliyokuwa ikitolewa hapo mwanzo. Mhe Spika, tunaushahidi wa baadhi ya risiti za kodi zilizokuwa zikilipwa mwanzo kwa baadhi ya ardhi ambazo zilikuwa zikilipwa karibu Dola 11,000 na kupewa mtu mwengine ambae ametakiwa na wizara kulipia Dola 3,000 tu, hapo kuna tofauti ya karibu Dola 8,000, kwa pesa za Tanzania ni karibu milioni 12 kwa *lease* moja tu tunazikosa. Ukiangalia Mhe. Spika, huu kama sio ufisadi ni kitu gani. Kweli tunaamini mtu gani serikalini hivi sasa? Na ardhi hizi ziko nyingi ni lazima zifutwe mara moja na ardhi hizo zirudishwe serikalini mara moja ili ziwanufaishe wananchi. Leo kila siku serikali inaongezea kodi wananchi, wakati kodi za rasilimali za nchi zipo mnaziacha zinaliwa na watu wachache tena wenye dhamana kubwa seriliani, huku mnawakamua walalahoi wananchi wetu kulipa kodi hizo.

Mhe Spika, wakati umefika sasa rasilimali tulizojaaliwa na Mwenyezi Mungu hapa Zanzibar, kwanza tuzitumie hizo na kama hazitoshi kutuendesha nchi yetu ndio tuwakamue wananchi wetu. Leo wazee wetu wanaoishi Majumba ya Wazee Sebleni tunajisifu tunawalipa shs 40,000/= kwa mwezi wakati pesa za kuwalipa vizuri tunazo, lakini tunashindwa kujipangia matumizi vizuri kwa tamaa ya watu wachache.

Mhe Spika, vianzio vya mapato, tumeona mapato kwa mwaka uliopita yameongezeka kutokana na malengo ambayo yaliyojipangia. Kwa mfano ZRB kukusanya karibu bilioni 106.6 hadi kufikia bilioni 120.4. Sijaridhika sana na kima hicho kwani ninazo taarifa kuwa kuna baadhi ya watendaji wachache wa ZRB wanashirikiana na wafanyabiashara na wawekezaji wachache kuiibia na kuikosesha mapato Serikali. Suala hili nikishalithibitisha nitakuja kuliripoti Barazani ili kulifanyia kazi. Hivi sasa ni mapema mno kwani kanuni zako zinatutaka jambo tunaloliwasilisha hapa Barazani ni lazima liwe na uhakika na liwe na ushahidi kamili. Wakati nikishakamilisha ushahidi huo, sitasita kuja kukuomba kulifanyia kazi kama tunavyoendelea kufanyia kazi hivi sasa kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe Spika, kwa upande wa TRA-Zanzibar, kamati yangu inawataka watendaji kujitahidi kudhibiti uvujaji wa mapato, kwani hatujaridhika na utendaji kwa baadhi yao, kwani tunazo taarifa kuwa kuna baadhi ya watendaji kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania, hasa walioko Bandarini wanashirikiana na baadhi ya Wafanyabiashara wakubwa wanaoleta bidhaa hapa nchini na kukwepa kodi na kuibia Serikali na kuikosesha serikali mapato.

Mhe Spika, kwa mtindo huu uliokuwepo kwa serikali yetu kushindwa kuwachukulia hatua za kuwawajibisha wabadhirifu wanaogundulika kuiibia serikali. Mchezo huu utaendelea kila kukicha hasa ukizingatia hofu tuliyonayo sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kutokujiamini katika kutekeleza majukumu yetu, kwani tumeshindwa kujua kuwa sisi ndio tunaopaswa kuiwajibisha serikali kutokana na uzembe na wizi unaofanywa kwa mali za serikali au umma.

Mhe Spika, kamati yangu pia haikuridhika na kitendo kilichofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) hasa Tanzania Bara kwa kushindwa kutuletea fedha zetu karibu bilioni 18 kwa mwaka unaomalizika, fedha ambazo sisi tuliziidhinisha zikusanywe kutokana na kodi ya huduma wanazozipata watumishi wa Jamhuri ya Muungano wanaofanyakazi zao hapa Zanzibar. Fedha ambazo zingeliweza kutatua kero mbali mbali za wananchi hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe Spika, suala hili sio dogo kwani kwa kiasi kikubwa limerejesha nyuma jitihada za serikali yetu kuwaondolea wananchi wake shida za maisha. Shilingi bilioni 18 ni karibu bajeti za wizara tatu, kama tungelizipata tungeliweza kujenga miundombinu mingi, mfano mwaka uliopita Mhe. Waziri wa Afya alihitaji karibu shilingi bilioni 1 kwa ajili kuijenga *ICU*, lakini hadi leo sijui kama ameweza angalau kuimaliza kutokana na tatizo la fedha ndani ya serikali yetu. *(Makofi)*

Mfano mwengine hivi sasa serikali kutokuwa na meli ya uhakika kwa ajili ya kuwasafirisha wananchi wake, basi fedha hizo zingeliweza angalau kuisaidia serikali ikaweza kulipa fedha nusu, ili kununulia meli ya uhakika na wananchi wake kuweza kupata huduma ya usafiri wa uhakika.

Aidha, fedha hizo zingeliweza kutatua matatizo ya kununulia madeksi. Pia, fedha hizo zingeliweza kuchangia ujenzi wa barabara zetu za ndani karibu zote, hata kumalizia skuli zetu tulizozianzisha majimboni, na nyengine zingeliweza kuchimba visima ili kuondoa tatizo la maji majimboni mwetu. Kwa mifano hiyo michache, kila mtu ameona ni kiasi gani ukosefu wa fedha hizo zimerejesha nyuma Maendeleo ya Jamii yetu. Vile vile fedha hizi pia zingeliweza kuboresha Makaazi ya Wazee wetu Wasiojiweza pale Sebleni, na haya ndiyo mambo yanayopigiwa kelele na wananchi wetu kila siku. *(Makofi)*

Mhe Spika, naomba kumuuliza Mhe Waziri gawio tulilolipata kutoka *B.O.T* bado serikali imeridhika? Kwani mimi ninavyojua kuna madai ya Zanzibar ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kupatiwa 11.5% ya gawio badala ya 4.5% tunayoendelea kuipata hivi sasa kutokana na hisa zetu za uundwaji wa Benki ya Tanzania. Hesabu za haraka kwa asilimia 11.5 tunazodai tungeliweza kupata gawio si chini ya shilingi bilioni 15 kwa mwaka, ambapo kwa mwaka huu tumezikosa karibu shilingi bilioni 7. *(Makofi)*

Lakini kutokana na kimya kirefu na kwa kua na sisi tumeridhika na kupokea tunachopewa kutokana na unyonge wetu, inaonesha tumeridhika wakati kitu hicho sio sahihi hata kidogo, katika nchi zilizoungana kwa hiari kwa maslahi ya kiuchumi na kijamii lakini hadi leo tuna miaka karibu 48, suala hili halijapatiwa ufumbuzi. Nadhani tungelikuwa tunadai kwa mataifa ya kigeni tungelikuwa tumeshajua moja, mambo kama haya ndiyo yanayowafanya Wazanzibari kupiga kelele huko nje na kudai haki zao ndani ya Muungano. *(Makofi)*

Mhe Spika, tunaipongeza serikali yetu kutokana na mapato ya nchi kuongezeka imeweza kutenga karibu shilingi bilioni 8 kwa ajili ya Mfuko wa Elimu ya Juu, ambapo ni asilimia 200% ya bajeti ya mwaka uliopita. Hii imetokana na kilio chetu mwaka uliopita kwa vijana wetu wengi kukosa mikopo wa kuendelea na masomo yao ya Elimu ya juu. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ndio maana tunakusifu Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wetu mpendwa kuwa msikivu kwa kutekeleza ushauri tunaoutoa hapa Barazani. *(Makofi)*

Lakini pamoja na pongezi hizo kamati yangu inaitaka Wizara ya Elimu Zanzibar kuzitafuta fedha za wananchi zilizopotea karibu shilingi bilioni 8 wanazodai eti wamepewa wanafunzi wasiowajua (Wanafunzi Hewa). Kamati yangu inaagiza fedha hizo zirudishwe serikalini mara moja kabla ya Bajeti ya Wizara ya Elimu kuwasilishwa hapa Barazani au tupatiwe maelezo ya kina, vyenginevyo Mhe Spika itabidi askari wako shupavu, Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi *(Watch Dogs)* uwaagize wakazisake fedha hizo na naamini watazigundua na watazileta. *(Makofi)*

Mhe Spika, eneo jingine tulililoligundua tunaweza kuongeza mapato kwenye bajeti yetu ni kupitia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Nyongeza ya kwanza orodha ya Mambo ya Muungano, Orodha ya 18 Elimu ya juu ni jambo la Muungano. Kwa hiyo, tunahitaji kupata gawio letu kama tunavyopata kwenye mambo mengine ya hiyo ya asilimia 4.5 kwa hivi sasa.

Bajeti ya mwaka unaoishia mwezi huu Mhe. Spika, tungeliweza kupata karibu gawio shilingi bilioni 15 kutoka Mfuko wa Elimu ya Juu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo bajeti iliyopita Mhe. Spika, bajeti ya Elimu ya Juu ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania karibu bilioni 317 ukiangalia asilimia 4.5 utakuta karibu shilini bilioni 15 mpaka 18 tumeweza kuzikosa. Kwa hiyo, hili pia ni miongoni mwa Kero za Muungano.

Kutokana na hali hiyo, tunataka serikali yetu kuidai katika bajeti ya mwaka huu ujao tupatiwe asilimia yetu hii ya 4.5, ili tuweze kujipangia wenyewe matumizi yetu ya Elimu ya Juu, kwani tumepata taarifa kuwa kuna baadhi ya wanafunzi hivi sasa ambao ni wa Zanzibar waliopo nje ya nchi wanatishiwa kurejeshwa nchini kutokana na ukosefu wa kuweza kulipa fedha.

Mhe Spika, eneo jingine ambalo tunaloweza kuisaidia serikali yetu kuongeza mapato yetu ni kupitia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nyongeza ya kwanza orodha ya 15 suala la Mafuta na Gesi Asilia.

Katika mapato yanayoendelea kuvunwa na Wizara ya Nishati na Madini ya Tanzania Bara, ambayo sio Wizara ya Muungano ambapo inaendelea kuvuna mapato ya gesi kwa zaidi ya mwaka wa tisa hivi sasa, lakini Zanzibar hakuna tunachokipata kwa serikali yetu, labda serikali ituambie je katika mwaka huu uliokwisha tumepata kiasi ngapi? Kutokana na mavuno ya gesi kutoka katika Wizara ya Nishati ya Tanzania Bara, yaani zinazotokana na gesi iliyovunwa huko Bara?

Lakini sio hayo tu, hasa kwa hivi sasa kwa kuwa imegundulika gesi nyingi zaidi katika eneo la Mtwara. Vile vile tunayo taarifa ya kuwa kuna kampuni mbili, yaani *STAR ONE* na *BRITISH GAS* tayari zimepewa kazi hiyo na kuna baadhi karibu *Blocks* sita mpaka saba watapewa makampuni mengine, kwa ajili ya uzalishaji wa gesi na kila kampuni kabla ya kupewa kazi hiyo watatakiwa kulipa ada ya kilemba kabla ya kuanza kuvuna hiyo gesi, Mhe. Spika haya yote ni mapato ya Muungano.

Lakini sisi tukiwa wasimamizi wa maslahi ya wananchi wa Zanzibar, kwa serikali inabidi tuulize kuna nini? Tunaamini kama serikali itafuatilia, basi kuna mapato mengi ambayo tutaweza kuyapata, ili kuongeza uwezo katika Bajeti yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli bila ya hivyo tutakuwa tunawadanganya wananchi wetu tunapowambia suala la Gesi na Mafuta ni la Muungano, wakati wao hawapati kitu. *(Makofi)*

Mhe Spika, tunaipongeza serikali kwa kupiga marufuku uuzwaji wa mafuta huko baharini kwa njia ya meli kwa meli, kwani kuna mapato mengi ya serikali yalikuwa yakipotea, tunaamini sasa mapato hayo yataongeza mapato ya serikali.

Lakini katika eneo hili tunaitaka serikali kukaa na waletaji wa mafuta hapa Zanzibar, ili kulizungumzia suala la uletaji mafuta hapa nchini na ikiwa kuna kampuni yoyote itakayokuwa na uwezo wa kuleta mafuta moja kwa moja kutoka nje hadi hapa Zanzibar, basi waweze kuruhusiwa, kwani Tanzania Bara wao wameamua kuagiza mafuta kwa pamoja na kuyauza kwa kampuni nyengine. Kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa kampuni zinazoleta mafuta Zanzibar kutozwa ushuru mara mbili. *(Makofi)*

Mhe Spika, kwa upande wa utekelezaji wa *Programu* ya Mkuza II upande wa Huduma za Jamii, kamati yangu imeridhika na mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa miaka mitatu kwa kuamua kutumia fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi wa dawa hasa kutokana na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwani kutokana na hali za wananchi wetu uwezo wa kununua dawa za hospitali unakuwa mdogo.

Lakini kuna taarifa kwa hivi sasa kuna baadhi ya wafamasia huziiba dawa kutoka serikalini na kuziuza katika Maduka ya Watu Binafsi, tunawambia ole wao tabia hiyo waiache mara moja, vinginevyo adhabu kali itawashukia pindipo tukija kuwanasa. Kwa hiyo Kamati yangu inashauri serikali kurudisha ule utaratibu wa zamani wa serikali kuagizia dawa na kuyaandika au kuyapiga nembo ya SMZ, hili litaweza kukomesha wizi huo. *(Makofi)*

Mhe Spika, kamati yangu bado hairidhiki na utekelezaji wa mashirikiano na Sekta Binafsi (*PPP*), kwani bado kuna kazi nyingi ambazo serikali ingeliweza kushirikiana na Sekta Binafsi au kampuni za Zanzibar. Kwa mfano, kuna suala la kuuweka mji wetu safi, basi ni bora Mabaraza yetu ya Miji kuzitoa kazi hizo kwa kampuni

Binafsi, ili kuongeza wigo wa ajira katika Taasisi Binafsi. Tayari tumewashauri Mabaraza ya Miji kulitekeleza hilo na Mabaraza yabakie na kazi chache ambazo watazimudu kwa wepesi.

Mhe Spika, kamati yangu imegundua kwamba kuna miradi mingi hasa ya ujenzi imekuwa ikipewa kampuni zinazotoka nje ya Zanzibar na kuzikosesha kazi kampuni za ndani, kwani wao ndio walipaji wakubwa wa kodi na hata usajili wao wa kampuni zao umesajiliwa hapa Zanzibar, ambazo nyingi huwatumia vijana wa hapa Zanzibar kwa ajili ya kuongeza ajira.

Kwa nchi za wenzetu kodi za wananchi hupewa kipaumbele kampuni za ndani, ili kuwajenga uwezo, kwani kama hivi sasa tunazo taarifa kuwa hata madeski pia hutengenezwa na kampuni kutoka nje ya Zanzibar, ambapo kampuni za ndani hukoseshwa kazi hizo. Sasa je! hawa wananchi wetu watapewa kazi na nani au nchi gani?

Mhe Spika, hali ya ajira kwa vijana wetu ni mbaya sana hivi sasa vijana wetu wengi hawana ajira. Kwa hiyo, ninatofautiana na taarifa aliyotusomea Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwenye kitabu chake cha bajeti, alichotusomea na kutuambia kwamba katika kila vijana watano eti kijana mmoja tu ndiye ambaye hana ajira. *(Makofi)*

Mhe Waziri, takwimu hiyo haikufanyiwa utafiti wa kutosha, kwani vijana wengi hasa wa kike, ambao ndio wengi wakishamaliza skuli tu hubaki majumbani mwao bila ya ajira. Kwa mfano, kuna wengine wameshasomea ualimu ngazi ya Cheti na Diploma mpaka leo bado hawajaajiriwa, mbali waliofeli Kidato cha Pili na wengine walioacha masomo yao njiani kutokana na sababu mbali mbali.

Tunaelewa kuwa ajira sio tu kuajiriwa serikalini, bali shughuli yoyote nyengine inayompatia kipato pia ni ajira. Lakini ukweli vijana wengi hawana ajira na wanakuwa mzigo mkubwa kwa familia zao. Kwa hiyo, tunatoa wito kwa wizara zote kuweka kipaumbele kwa kuwapa kazi kampuni za ndani, kwani hata akiba zao karibu zote wanaziweka katika benki zilizopo hapa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa nchi za wenzetu hasa China tumegundua kampuni nyingi zinazopewa kazi na serikali aidha ni Kampuni za Serikali au kampuni ya ndani, ili kuongeza mzunguko wa fedha na ajira ndani ya nchi yao, kwani wanaamini kutoa kazi kwa kampuni za nje, basi hata fedha hazibakii nchini na wanaweza kuwekeza nje.

Kwa mfano mzuri hata kwa jirani zetu Tanzania Bara, hivi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania imezihamasisha kampuni kushirikiana kwa pamoja zaidi ya kampuni moja na kupewa mradi mmoja mkubwa, kwa pamoja mfano miradi ya ujenzi wa Barabara na Madaraja, ili kuunganisha nguvu zao za kuongeza mtaji, ubora wa utaalamu pamoja na kazi, ili kujenga Sekta Binafsi iweze kutoa ajira kwa wananchi wao.

Mhe Spika, tunatoa pongezi kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kutoa mikopo kupitia Mfuko wa AK na JK. Lakini bado haujakidhi haja ya kuwawezesha wananchi wetu, kwani fedha hizo ni kidogo sana, ambapo wananchi wengi mpaka leo wanazisubiri kwa muda mrefu, lakini mpaka leo wengi hawajazipata.

Mhe. Spika, hapa tunaishauri serikali yetu kuangalia uwezekano wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Vijana, ambayo tunaamini ndio itakuwa suluhisho la kusaida vijana kuwaondoa katika umasikini na kuleta maendeleo kwa vijana hapa nchini kwetu. Pia tunapongeza jitihada zinazofanywa na Waziri wa Kazi na Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kuwatafutia misaada mbali mbali ya fedha na ajira vijana na kinamama wetu, lakini bado anayo kazi kubwa kwani malengo yake ni makubwa lakini uwezo alionao wa uwezeshaji mpaka hivi sasa ni mdogo. *(Makofi)*

Mhe Spika, kupitia Wizara ya Kazi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, tunataka kuanzia mwaka huu Mhe. Waziri wakati wa bajeti yake kuja kutuhakikishia kwamba vijana wetu wote wanaofanya kazi kwenye hoteli za Kitalii pamoja na walinzi kwenye Minara ya *Zantel* tuhakikishe wanapatiwa Mikataba ya Ajira vinginevyo tutaikataa bajeti ya wizara. *(Makofi)*

Kwa kweli tunasikitika kuwa kampuni na Uwekezaji wao wanakuja kutengeza faida kwetu, lakini wanawatumia vijana wetu kuwafanyia kazi bila ya kuwapa mikataba, ambapo hupelekea kuwafukuza kazi kama kuku kwani hakuna mkataba unaowalinda Muajiri na Muajiriwa. *(Makofi)*

Kwa mfano, hivi sasa kuna walinzi wa Kampuni ya *Zantel* wameshatumikia karibu miaka mitano wanataka kuwaachisha kazi, na kwa kuwa hawana mikataba inaonesha wataondokea patupu bila haki zao za kustaafishwa kazi, hivi sasa wamekuwa kama manamba tu, sio waajiriwa. Suala hili ndilo linalosababisha vijana wetu kila siku kuwa na hali ngumu ya maisha, kwani hawana kinga ya hatma yao. *(Makofi)*

Mhe Spika, tunaishukuru Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweka utaratibu mzuri wa kutoa fedha taslim kwa Waheshimiwa Wawakilishi, kwa kuondolea matatizo madogomadogo majimboni mwao, kwani kwa muda mrefu tulikuwa tunawaangalia Wabunge wanavyotumia fedha zao na sisi tukiwa hatuna uhakika wa kuzipata. Kwa hivyo, naamini Waheshimiwa Wawakilishi wote watafanya matumizi vizuri kwa kufuata sheria na kurejesha matumizi, ili kila mwaka kuweza kupatiwa nyengine. *(Makofi)*

Lakini tunaiomba serikali kuangalia mfumo wa wenzetu Kenya jinsi walivyoweka utaratibu mzuri wa utoaji na usimamizi wa fedha hizo, ambapo hivi sasa kuna miradi mingi imejengwa na wananchi kupitia fedha hizo walizopewa Waheshimiwa Wajumbe kule Kenya.

Mhe. Spika, majimboni kwetu tuna matatizo mengi lakini uwezo wa kuyatatua ni mdogo sana, kwa hiyo kwa mfumko wa bei kwa vifaa vya ujenzi hivi sasa ulivyo shilingi milioni 10 sijui tutatatua jambo gani na tuache jambo lipi? Pamoja na hayo, tunaishukuru serikali yetu kwa kuanzia kima hicho na tunaamini kila tutakapozitumia vizuri, basi serikali itaweza kutuongezea fedha hizo kama alivyoahidi Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mhe Spika, kwa ujumla bajeti ya mwaka huu imejaribu kujikita zaidi kwa maendeleo ya wananchi, kwani karibu bilioni 341.1 sawa 53% ya mapato yanaelekezwa kwenye maendeleo na bilioni 307.8 sawa na 47% zimeelekezwa katika matumizi ya kawaida. Kamati yangu imeridhika na mgawanyo huo maalum wa fedha, lakini tatizo letu liko pale pale baadhi ya tunaokwenda kuwakabidhi kuzisimamia fedha hizo si waaminifu, sasa ni vigumu kuendelea kuwaamini kuwapa nyengine wakafanya watakavyo. Kitu hiki hakiwezekani hata kidogo.

Kamati yangu imeridhika na jinsi ya mgao ulivyofanywa kutokana na fedha zilizopo karibu shilingi bilioni mbili kwa maeneo maalum, ikiwemo Utunzaji na Uhifadhi Mazingira, Walemavu, Madeski, na Dawa. Lakini kamati yangu inatoa angalizo kuwa utekelezaji wa matumizi hayo tutaufuatilia kwa karibu, ili watu wachache wasije kujificha kwenye kichaka cha matumizi ya fedha hizo kwa matumizi yao binafsi.

Mhe Spika, kamati yangu inaipongeza serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kupanda mikarafuu zaidi na kuitoa kwa wakulima, lakini pia kwa kuimarisha kilimo hasa cha mpunga kwa kununua mbegu, mbolea na pembejeo za kilimo.

Lakini bado hatutakubali kuruhusu kuidhinisha fedha nyingine mpaka tujue fedha tulizotoa mwaka uliopita zimetumika vipi, kwani tunazo taarifa kuwa kuna baadhi ya watendaji waliopewa fedha hizo kwa ajili ya kununulia mbolea na pembejeo za kilimo hawakuzifikisha kwa wahusika na serikali inajua, lakini kama kawaida yao serikali hadi leo iko kimya hakuna hatua zilizochukuliwa kwa wahusika hadi leo watu hao wanapiga tai maofisini mwao.

Sasa nakuuliza Mhe Spika kwa hali hii kweli sisi tutapona na hayo maendeleo ndio yatapatikana? Kwa hivyo, wakati umefika kila mtu aliyejikubalisha kuwatumikia wananchi awajibike kwa upande wake, na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa haraka kwa yeyote atakayekiuka taratibu hizo.

Mhe Spika, serikali imetuomba ruhusa ya kuwaruhusu kuuzwa kwa majengo Machakavu ya Serikali. Suala hili kamati yangu haikubaliani nalo kwa sasa mpaka tupate jawabu kutoka serikalini ya hatua tuliyoitaka serikali kuyarudisha serikalini majengo tuliyoyataja kwenye Ripoti ya Kamati Teule, ambayo yaliuzwa kinyume cha sheria na watu wachache kujinufaisha kwa faida yao.

Mhe Spika, tumegundua kuwa pia kuna majengo mengine na mali nyengine za serikali zimeuzwa kwa bei ya kutupwa wakati kuna Agizo la Serikali kuzuia Mali za Serikali zisiuzwe. Kwa hivyo, majengo hayo kwanza yarudishwe serikalini na hapo ndipo tukubaliane utaratibu wa kuyauza majengo mengine.

Mhe Spika, serikali tushakukubalieni mambo mengi lakini kutokana na baadhi yenu kutokuwa waaminifu, sasa hatukubali vitu kiurahisi, kwa hili serikali itusikilize na sisi. Kwa baadaye tutapanga utaratibu mzuri wa uuzaji ambao hautaleta harufu ya rushwa.

Mhe Spika, tunaipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Saba kwa kuanzisha utaratibu wa kuyafufua majengo ya zamani yaliyokuwa yakitumiwa na serikali kama vile viwanda huko Maruhubi kwa ajili ya kujenga majengo ya serikali, ambapo baadhi yao si muda mrefu yataanza kutumika. Hongera sana Dkt. Shein kwa uono wako wa mbali. Kwa kuwa serikali yetu ina mipango mingi ya maendeleo, basi tunaamini na hayo majengo mengine yataweza kutumika kwa maslahi ya umma.

Mhe Spika, kwa kumalizia kamati yangu inaamini kama tutakuwa makini na kusimamia uchumi wetu, hasa kwa kuimarisha ukusanyaji kodi kuacha kudokoa tunachokipata na kuendelea kudai mapato yetu yaliyomo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa sasa bila ya kuambiwa tusubiri Katiba mpya kama tunavyoambiwa hivi sasa, basi tunaamini mapato yataongezeka sana kwa kipindi kifupi.

Mhe. Spika, isitoshe kwa maandalizi ya siku za baadaye, matayarisho ya uchimbaji wa Mafuta na Gesi, pia kuendelea kudai kwa Zanzibar kuwa ni Eneo Maalum Tengefu la Kiuchumi, ili kuvutia uwekezaji hasa wa viwanda pamoja na Bandari Huru na kutafuta ufadhili kwa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri tunaamini tukiweza kufanya hayo, basi Zanzibar itakuwa miongoni mwa nchi zitakazobadilika kwa haraka sana kimaendeleo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tufikie hatua hiyo kwa haraka sana.

Mhe Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuendelea kunipa moyo na imani ya kuwatumikia, na ninawaahidi nitajitahidi kuwatumikia kwa uwezo wangu wote, pia naishukukuru familia yangu, mama yangu, ndugu zangu pamoja na wake zangu wote kwa kunivumilia na kunipa moyo wakati wote ninapowaacha nikiwa katika majukumu ya kuwatumikia wananchi.

Mhe Spika, kwa mara nyengine tena nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kunisikiliza. Vile vile Mhe. Spika, nikushukuru wewe zaidi kwa kuweza kunipa nafasi ya mwanzo kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, nashukuru, ahsante sana.

Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru *Allah* kwa kutupa uhai, uzima na taufiki ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Pili kwa kuwa tuko katika kipindi cha bajeti, umepita mwaka mzima tokea tuondokane na bajeti iliyopita. Kwa hivyo, napenda kutoa shukurani maalum kwa wananchi wote wa Jimbo la Ziwani kwa uvumilivu pamoja na umahiri wao katika kunisaidia kwenye kazi hii walionikabidhi wao. Mhe. Spika, naamini nitaitekeleza kwa kadri ya uwezo atakaonijaalia Mwenyezi Mungu na ninawaahidi sitowaangusha wala kuwatelekeza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hapo napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa uwasilishaji mzuri wenye maneno matamu na fasaha wakati alipowasilisha bejeti hii. Kwa kweli katika miaka mingi sijapata kusikia maneno mazuri kama haya, yaliyotoka kwa Mhe. Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Lakini baadhi ya mambo yanayo mwelekeo mzuri na mengine yanaelekea kumkwaza. Kwa hivyo, labda Mhe. Spika nianze ule ukurasa wa mwisho mwisho kwenye muhtasari wa bajeti wenyewe ukurasa wa 70 katika kitabu cha Mhe. Waziri.
Mhe. Spika, tunaingia wasi wasi, kwa sababu kitu maendeleo na ukitizama mahitaji ya wananchi, maendeleo maana yake ni kitu kinachozidi. Sasa ukija kwenye maendeleo ukaona kinapungua, basi kidogo inatia wasi wasi kitu gani kimetokea hata ikawa maendeleo yapungue.

Bajeti ya mwaka jana ya maendeleo kwa wahisani ilikuwa ni bilioni 340.96, lakini mara hii imepungua mpaka kufikia bilioni 293.2. Katika maelezo yake Mhe. Waziri alitaja kwamba tunaanza kuondokana na utegemezi. Kutokana na hali hiyo, kidogo nina wasi wasi kwamba yalikuwa ni maneno yaliyokuwa ni sahihi au yalikuwa ni ya kujitoa tu.

Mhe. Spika, nyuma katika kupitia mapitio ya bajeti iliyopita kifungu cha *Program* ya Miradi ukurasa 45 kifungu cha 48. Mhe. Waziri alijizonga kidogo pengine alisema kweli, lakini katika ule ukweli ndipo penye hiyo *clue*. Katika mchango uliotolewa na wafadhili pamoja na serikali, katika kipindi cha miezi 9 ya mwanzo, Serikali ilikuwa imechangia asilimia 13.5 ya bajeti waliyotarajiwa. Wakati wafadhili walikuwa wamechangia asilimia 86.5. Mimi nafikiria kwamba wafadhili wamepunguza kutokana na tatizo hili. Ikiwa wafadhili wamechangia asilimia 86.5, serikali ina *leg behind* asilimia 13.5 tu ya mchango wao Mhe. Spika, hapa pana tatizo. Sisi tunawaita washirika wa maendeleo. Angalau tungekwenda sambamba au tungepishana kwa asilimia ndogo tu. Lakini sisi serikali tuko asilimia 13.5 ndani ya miezi 9 au miezi 9 imeshapita, wakati wafadhili wamechangia asilimia 86.5.

Mimi nafikiria kwamba sio kwamba tunaondokana na utegemezi, lakini hatujiwezi inabidi tubebwe moja kwa moja. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri wakati wa majumuisho yake atueleze ni kwa sababu gani baada ya miezi 9 serikali imechangia asilimia 13.5 tu ya bajeti iliyotarajiwa kuchangiwa katika programu za maendeleo, hilo la mwanzo Mhe. Spika. Ingawa kasema kwamba tunaondokana na utegemezi, lakini bado sentensi inabakia pale pale kwamba utegemezi upo.

Mhe. Spika, suala la pili ni suala la ukuaji wa uchumi. Kulinganisha mwaka mmoja na wa pili hupati *figure* sahihi ya ukuaji uchumi wako. Kwa sababu hii asilimia ambayo tayari inaambiwa ilifikiwa mwaka 2011, huko nyuma ilikuwa imeshapitwa. Kwa nini katika miaka ya nyuma kabisa hiyo asilimia hiyo imeshapitwa sasa hivi tunaambiwa uchumi unakuwa zaidi. Lakini tujiulize huu ukuaji uchumi wa Zanzibar unamnufaisha kweli Mzanzibari. Kuna mambo matatu Mhe. Spika, naomba tuyatizame.

Ukuaji wa uchumi unatarajiwa ulete ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi. Kwanza ukuaji wa uchumi huu unatarajiwa uongeze ajira. Mhe. Waziri hakueleza katika bajeti hii serikali inakusudia kuongeza ajira ngapi kwa upande wa serikali na ajira ngapi kwa upande wa sekta binafsi. Wamesema tu, mbali ya hiyo ambayo imetajwa, kulitolewa *wrong figure* kwamba asilimia 80 vijana wameshaajiriwa na asilimia 20 hawajaajiriwa, ambapo pengine ni kinyume chake, sina hakika. Lakini kwa vyovyote waliokuwa hawajaajiriwa ni wengi kuliko walioajiriwa.

Mhe. Spika, tungekuwa *very specific* tukasema kwa bajeti hii serikali inakusudia kuongeza ajira fulani za upande wa serikali na ajira fulani kwa upande wa sekta binafsi. Sasa katika bajeti inayokuja ndio tutaweza kupima kwamba serikali imetimiza malengo yake au haikutimiza. Imetimiza kwa sababu kadhaa na haikutimiza kwa sababu kadhaa. Lakini ukisema tu tutaongeza ajira wakiajiriwa watu wawili ndio umeshaongeza, walikuwa hawamo kazini eti. Lakini unatwambia kwamba mimi bajeti yangu ninaipanga kuongeza ajira 500, upande wa serikalini 150 na upande wa sekta binafsi 350. Hapo ndio tungejua kwamba bajeti hii imekusudiwa kuongeza ajira. Lakini kwa kutuachia tu hivi hivi sisi hatuamini.

Mhe. Spika, mfumko wa bei kuna mambo matatu ambayo yangeelezwa tungejua kwamba mfumko wa bei sasa utakuwa umedhibitika katika bajeti hiyo. Kwanza uzalishaji katika sekta ya kilimo, imeachwa hata haikutiwa katika miradi mikuu. Ukifungua kitabu cha Mhe. Waziri alipoeleza miradi mikuu ya kipaumbele cha mwaka huu hata kilimo hamna. Ipo katika kifungu cha 90 cha *budget speech* yake, hata kilimo hakikutajwa hapa wakati mwaka jana tuliambiwa Mapinduzi ya Kilimo ndio kipa umbele, mwaka huu hamna.

Sasa mimi nauliza ardhi zote zimeshalimwa? Matrekta yanapishana njiani kama hivi *vimeti*, hata ikawa kilimo sio kipaumbele tena. Hotelini tungule zinazokwenda zinalimwa hapa hapa? kebichi zinazouzwa na mazao yote yanayouzwa hotelini yalimwa hapa hapa? Halafu mfumko wa bei baada ya kuongeza uzalishaji tulikubaliana kuanzishwe kwa ghala ya hakiba. Moja katika kazi yake ni kuzuia mfumko wa bei. Kwa sababu duniani misimu inatofautiana, msimu huu inawezekana mazao yakawa mengi, mazuri na msimu mwengine yakawa kidogo, bei ikapanda.

Tanzania Bara huu mwaka wa ngapi wameshaanzisha ghala ya hakiba. Sisi tumeshindwa nini, mbona haikutajwa katika Bajeti Kuu ya Serikali ndio ambayo ingezuia mfumko wa bei. Hata wakulima wakiharibikiwa na mazao yao inakuwa si tatizo sana. Sasa haya mambo makubwa makubwa haya hayatajwi.

Jambo jengine ni kuwa na uzalishaji katika viwanda. Tumeambiwa hapa katika kitabu hapa Mapitio ya Hali ya Uchumi, *contribution* ya viwanda katika pato la Zanzibar ikiwa ni pamoja na kiwanda cha uchimbaji wa mawe ni asilimia 12. Tutawezaje kuzuia mfumko wa bei ikiwa uzalishaji ndani ya viwanda ni asilimia 12. Katika masuali na majibu niliwahi kusema kwamba Indonesia waliondokana na kutegemea kilimo wakenda mpaka asilimia 46 ya pato la taifa kiviwanda, ndio wapo pale. Lakini sisi viwanda vyetu ni vya maji ya kunywa na uchimbaji wa mawe hata kile cha nyuzi kimetushinda.

Halafu Mheshimiwa katika kitabu chako hiki cha kwanza au cha pili uliandika pahali kwamba moja katika sekta zinazozuia mfumko wa bei ni thamani ya pesa. Sasa sisi Zanzibar hebu tueleze kuna *control* gani ya fedha zetu tunazotumia hata iwe tunaweza ku-*control* mfumko wa bei tuna *impact* gani katika fedha hizi tunazotumia katika Wizara yako ya Fedha. Kwa mfano ni *partners* sisi katika Muungano je, kuna *discussion* yoyote inayofanywa ni wapi palipoathirika pakapewa angalau msukumo au tunaendelea kutumia shilingi ya Tanzania kwa sababu ya mazoea tu. Ikiwa tunaathirika tupe sababu za kuathirika na vipi tutaweza kujikwamua.

Lakini mbali ya *factor* hiyo mimi nimepitia katika madaftari mengine, wanasema njia zote mbili katika kukuza uchumi ni lazima uwe na *consrol* kuhusu viwango vya kodi. *(Physical policy)* na uwe na *control* kuhusu mambo

ya fedha *(monetary policy)*. Sasa hebu njoo utueleze ndani ya huu muungano wetu tulionao na sisi Zanzibar tunajenga uchumi wetu, tuna *control* gani katika mambo mawili hayo ili kuweza kukuza uchumi wetu.
Siku moja tuliuliza swali hapa kwa nini Zanzibar yamechimbuka mabenki mengi na hali yetu ni hii. Wachumi wanatwambia kukua uchumi kwa Zanzibar wanaofaidika ni watu wa aina tatu. (1) Halali (2) Haramu.

(1) **Halali:** Ni wenye hoteli, kwa biashara zao wanazozifanya, wenye benki kwa biashara zao wanazozifanya na wafanya biashara wakubwa wenye mitaji mikubwa.

(2) **Haramu:** Wale ambao wanaokaa maofisini wakamega pesa zetu.

Hawa ndio wanaofaidika, lakini mwananchi wa kawaida kwa sababu hakuna uzalishaji ulioongezeka hawafaidiki. Sekta ya utalii inahitaji huduma nyingi lakini hakuna huduma inayofanyika hapa Zanzibar inayopewa. Hakuna *bed sheet* linaloshonwa hapa akapelekewa, hakuna foronya inayoshonwa hapa akapelekewa, hakuna kikombe kinachotengenezwa hapa akapelekewa. Hata samaki wakati mwengine wanaagizia kutoka nje, maana wanasema samaki wetu tunawaburuta tukishakuwavua wanachunika ngozi.

Hapa sisi tulipitisha bodi ya viwango wakati baraza linaanza ule Mswada wa mwanzo ulikuwa ni wa Bodi ya Viwango. Mpaka hivi leo hakuna chochote tulichokiona kilichofanyika. Wenzetu hotelini wanatumia viwango, kwa hivyo mambo haya kwa sababu hatuyashughulikii ndiyo yanayotuvunjia huu uchumi.

Mhe. Spika, uchumi huu unaokuwa hauonekani kwa wananchi kwa sababu ni hao tu ndio wanaofaidika. Mimi namsifu sana katika vitabu vyake, kitabu hichi cha 2 cha muelekeo wa hali ya uchumi ukurasa wa kwanza na ndio utangulizi kasema hivi:-

> "Maendeleo mazuri ya nchi yanatagemea ukuaji wa kiuchumi unaolenga kukuza hali ya nchi na wananchi wake kiujumla"

Ndio nikasema wakati mwengine Mhe. Waziri anatuchanganya kwa sababu kuna *facts* anazijua lakini afanye vipi pengine kakwama kwenye Muungano, hatuelezi vizuri. Kwa sababu hii *fact* na hakuificha, hapo ndio ninapompa *distinction* yake sio *credit*, *fact* ieleze halafu mengine yavuke, wenyewe watajua, mwenye macho haambiwi tazama. Hili ndio swali la kujiuliza je, kukua kwetu kwa uchumi kuna lengo hapa. Mwananchi wa kawaida anafaidika na kukua kwetu kwa uchumi.

Mhe. Spika, twende katika maudhui mengine Maendeleo ya Kisekta. Kukua kwa uchumi kunahitajika vile vile ukuaji wa maendeleo ya kisekta kama kilimo lakini kipo hoi bin taabani kama kilivyo. Baada ya matrekta 9 au 10 yaliyoagizwa tokea na Mhe. Burhani Saadat, hayajaja mengine. Naomba radhi hayo sijayajua, Mhe. Mansoor kasema na yeye kaleta 10, namshukuru sana kwa kunishtua. Nyingi nasikia zinaitwa *power tillers* ambazo hazina nguvu sana katika ardhi zetu ni ardhi za mchanga mchanga na mambo mengine, tunashukuru.

Lakini bado hakijatoa tija ya kwenda katika maendeleo. Sekta ya pili ni sekta ya elimu. Juzi nilisema katika swali langu la nyongeza, si wakati tena wa kusikia katika kiriri kile pale Mhe. Waziri anaambiwa kuwa skuli yetu inavuja, umeme umekatwa, kompyuta zimeharibika, ndiyo lugha ya kuzungumza ikiwa tunataka kweli maendeleo. Tungeiona bajeti imeleta katika *quality education*.

Mhe. Spika, sote tulisoma huko nyuma kabla hatujaja hapa tulikuwa tunajua kukopia kiutaalamu. Leo wanafunzi wetu kwa sababu ya uchache wa elimu, udhaifu wa elimu inayotolewa hata kukopia hawajui. Mimi nilizungumza sana na watu wa Wizara ya Elimu, mimi nawasikiliza sana wanavyojibu masuali, kusema wazee, nini. Elimu inayotolewa siyo.

Mimi wakati namalizia kusomesha kabla sijaja katika siasa ilikuwa haya mambo ya *tuition* yaanza kuingia ingia. Mimi niliwazuia wanafunzi wangu wote niliokuwa nikiwasomesha nikawambia kama unataka kupasi basi jizuie kwenda *tuition*, isipokuwa kwa jambo moja tu. Kama unataka kwenda *tuition* kwa kujiendeleza katika lugha ya Kiingereza na nyenginezo hapo nenda, lakini kwa somo ninalokusomesha mie ukenda *tuition* unafeli.

Leo tuition imekuwa ndio kawaida kabisa, ile inaonesha kwamba bado maskulini hakutolewi *quality education*, wanafunzi waamini ile inayotolewa pale. Sasa kama tunataka kweli bajeti ilenge katika maendeleo, basi tungekwenda katika *quality education* tukaanza kujitizama tumekosea wapi.

Mheshimiwa sekta ya kiwanda ndio haisemeki kama nilivyosema mwanzo. Tokea siku tuliyoanza Baraza hili napiga kelele angalau Mhe. Spika, tusafirishe chumvi wananchi wana mashamba, wananchi wanajitolea, sisi tuka *improvise* tu mambo tukasafirisha ile chumvi, inatushinda. Hebu Mhe. Waziri aje atueleze sekta ya viwanda zile sera zinazotolewa za viwanda zinapata msukumo gani katika bajeti ya serikali, hata ikawakuta

*stagnation* kama hii iliyopo. *At least* kila mwaka ingekuwa tunapata kiwanda kipya kimoja tu. Kuna mambo gani yanayotukwaza sisi hapa tukawa hatuna viwanda?

Mhe. Spika, sekta hizi ni nyingi, uvuvi tumeshasema mambo mengi kuhusu uvuvi. Mhe. Waziri alitaja sana na akasema kwamba uvuvi umeongezeka hii ni kutokana na kuongezeka kwa vyombo na wavuvi wenyewe. Lakini je, samaki wanaovuliwa anawajua, wenzetu wanavua samaki kwa umri, umri kama haujatimia anarudishwa baharini.

Mhe. Spika, mapato ya serikali yanatokana na rasilimali na kodi. Tunayo rasilimali yetu ya mafuta lakini Mhe. Waziri hakutaja imefikia wapi. Kuna fedha ambazo za wale wanaofanya kazi Zanzibar kupitia Muungano, mwaka jana tulizikosa. Swali langu je, zile tulizozikosa mwaka jana kwa sababu makubaliano yameshapita tutapewa baada ya hiyo sheria kupitishwa.

Mhe. Spika, mwisho kuhusu matumizi ya serikali. Mhasibu Mkuu wa Serikali anasema mapato yote ya Serikali yanatakiwa kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Haya ni maneno yake aliyotupa katika semina moja wapo alizotufanyia. Mara hii kumekuja staili mpya ya kuwa kuchangwe kodi yanunuliwe madeksi. Sasa hii itaingia katika mfuko wa Serikali au watapewa watu, kwa sababu hakujaanzishwa mfuko wa madeksi kama ule Mfuko wa Barabara, hatujui zitakwenda vipi pesa hizi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa mimi sikubaliani na uuzaji wa majengo, halafu yajengwe mengine. Kwa sababu hamna ukweli ndani yake. Leo mimi nimechukua karatasi chungu nzima tulizopewa katika semina, zinafika kumi kuhusiana na taratibu za kuuza serikalini na kununua. Hamna hii kama majengo ya serikali yatauzwa halafu yajengwe mengine. Sasa ikiwa sera hiyo ni mpya wailete hapa sera mpya ya serikali tuipitishe kwanza halafu utaratibu ule wa uhakiki mali uende ukafanya kazi. Lakini unakuja kushtukizia tu keshauziwa fulani wala hujui.

Ndio maana kutokana na matumizi mabaya ya serikali zikaongezwa kodi hizi. Sisi hatukubaliani nazo. Kodi zile za watu wanasafiri kikawaida hakuna *alternative* mtu aliyekuwepo Pemba anataka kuja Unguja haji kwa ajili ya kutaka, anakuja kwa ajili ya haja fulani au anakwenda kwa ajili ya jambo fulani, halafu unamuongezea kodi. Wakati fedha za serikali matumizi yake ni mabovu. Imetajwa hapa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Hata pale Bandarini tunapata matukio mbali mbali pale. Sasa hivi karibu mwezi wa 4 Mkurugenzi Mkuu kaachishwa na hajateuliwa Mkurugenzi mwengine maana kile kitengo kimedharauliwa hasa, kimeonekana kitajiendesha wenyewe wakati ndio kinachoingiza fedha. Tunataka Mhe. Waziri aje atueleze kwa nini Shirika la Bandari mpaka leo halijapata Mkurugenzi Mkuu au hakuna.

Mhe. Spika, naomba nimalizie hapa. Ahsante sana.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Spika, kwanza kabisa sote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu. Vile vile napenda kulishukuru Baraza lako tukufu la Wawakilishi tokea kufika kwangu hapa kwa kupata mashirikiano ya kutosha kuanzia Ofisi yako mpaka Wawakilishi wote kwa ujumla.

Vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wetu, baba yetu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Al- Hajj Dokta Ali Mohammed Shein pamoja na Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, kwa hekima na busara kwa kuweza kutuongoza katika hali ya amani na utulivu.

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii, kusema kwamba hii ni mara yangu ya kwanza katika Baraza hili kuweza kusimama kwenye vyombo ndani ya Sheria hii kupata nafasi nikawa mimi ni mtu wa pili. Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wenzangu wananchi wangu wa Uzini kwa kukushukuru kwa dhati kabisa.

Mhe. Spika, nashukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa hekima na busara na usikivu kabisa kwa kutuletea hii bajeti nzuri ambayo ndiyo muelekeo wa kukidhi mahitaji ya wananchi wa Zanzibar. Lakini katika kitabu hichi Mhe. Spika, kama nilivyokuwa ni mgeni kwa vile kuna wenzangu wamenitangulia sana, nilikuwa nikae tu kimya kipindi chote hiki ili na mimi nipate kusoma zaidi. Lakini kwa kuwa kitabu hiki kimetupa nafasi sisi wawakilishi kwa kutengeneza maslahi ya nchi kuweka mbele, basi nikaona nina sababu kuweza kutoa mchango huu ambao wananchi wa Uzini walionifikisha hapa nilipofika.

Mhe. Spika, katika kitabu hichi ambacho ukurasa 57 tumeelezwa mikakati ya Serikali yetu ya Zanzibar namna ya kupata mapato ya kuondoa haya matatizo yetu yanayowakabili vijana wetu kama afya, madeski ya skuli, walemavu, kilimo na mambo mengine muhimu.

Mhe. Spika, hili mimi silioni kubwa sana lakini nataka niwaambie waznzibari nikariri maneno yangu ambayo nilikuwa ninasema kwa miaka 20 iliyopita, humu ndani leo nitakuwa ninakariri tu kwamba Mhe. Spika, ili kuondosha matatizo haya bila kutegemea mambo haya tuliyokuwa tumeyakusudia tuyapate huku kwa kuweza kujaliza hasa hivi vikalio vya skuli na afya sisi Zanzibar tumejiunga na OIC, tulipojiunga na OIC Mhe. Spika, ilikuwa suala la njaa si la dini. Na kwa bahati nzuri nchi nyingi za Afrika Mashariki na Kati na *West* Afrika kuna waislamu asilimia tano tu na wasiokuwa waislamu asilimia zaidi ya 95 na wapo wanachama wa Jumuiya hii ya OIC.

Sasa Mhe. Spika, ninakumbuka kulikuwa kuna makubaliano kati ya viongozi wetu wakuu katika nchi. Yaani Rais wa awamu ya tatu kwa upande wa Tanganyika yaani Bara na kwa upande wa Zanzibar ilikuwa na *resolution* kwa upande wa Zanzibar Rais wetu kwa awamu ya tano. Na tulikubaliana kwa kauli moja Mhe. Spika, *resolution* ipo haya yote ninayazungumza leo ninao ushahidi na niko tayari kutoa ushahidi kwa maandishi yote niliyokuwa nimeyazungumza. Kwamba tulikubaliana Zanzibar tujitoe Tanzania iingie ili tufaidike sote, matokeo yake Mhe. Spika, ilikuwa ni kiini macho. Leo majirani zetu wanafaidi na barabara za ndani, barabara kuu, *universities*, maji ndugu zetu wa Uganda, umeme mambo yote. Lakini mpaka leo imekuwa jambo kama linatafsiriwa la kiajabu ajabu.

Mhe. Spika, kwa Zanzibar ukitizama na nchi za Afrika hakuna suala hapo linalozungumza dini, wenzetu kule Bara Tanganyika kuna ubalozi wa *Vatican city* na wala halikuwa tatizo kwetu sisi. Sasa ninafikiri Mhe. Spika, huu muungano wetu ni muungano wa hiari wala tusilazimishane. Kwa sababu ni muungano wa kuvumiliana, kujadiliana na kuheshimiana. Sasa kama wenzetu Bara hawakuwa tayari watuachie sisi Zanzibar twende huko tuna njaa. Na kitabu hiki ndio inaotekeleza Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar imeelezea wazi na mimi ninafikiri kusiwe na kisingizio kwamba OIC kujiunga kwake muda umepita. Mimi Mhe. Spika, kwa heshima ya Baraza hili niko tayari kusimamia Zanzibar inapata uanachama kesho wa OIC ili kutatua matatizo yetu.

Lakini vile vile Mhe. Spika, katika mazingara haya haya ya kukua uchumi kote ndugu zetu sehemu mbili hai hoi tumekaa hapa sote kwa maslahi ya nchi, tumekaa hapa sote kwa kuwatetea wazanzibari, hili suala la Afrika Mashariki na Kati. Mhe. Spika, suala la Afrika Mashariki na Kati katika suala hili hili la kukuza uchumi wetu na kupata mapato, yapo makubaliano. Awamu ya tano ya Tanganyika Tanzania Bara walileta nyaraka Zanzibar kutwambia kwamba mnasemaje Zanzibar katika masuala ya Afrika Mashariki na ya Kati, Zanzibar tukajibu kwa wenzetu Bara kwa viongozi wa kitaifa yaani Marais, tuacheni Zanzibar tuingie kama Zanzibar kule kuna suala la uchumi. Kwa sababu nyaraka zile katika Afrika Mashariki na ya Kati, yanazungumza kilimo, yanazungumza afya, yanazungumza mawasiliano yanazungumza michezo, yanazungumza elimu.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu hili hapa lilipo leo na wenzetu leo wapo kule kule Dodoma, kwa maana kwamba kila mmoja anatoa bajeti yake ya kilimo, utalii, ya mawasiliano. Kwa hivyo Waziri wa Kilimo wa Bara au wa Tanganyika anafika mwisho Chumbe, na Waziri wa Kilimo wa hapa anazungumza bajeti yake anafika Chumbe. Sasa inakuwaje Waziri wa Kilimo atuwakilishe sisi Zanzibar kwa Tanganyika.

Sasa Mhe. Spika, mimi ninafikiri wazanzibari tuwe wakweli katika hili nasema hatujachelewa. Na katika kulizungumza hili tufike wakati Mhe. Spika, huyu maiti kwa kuogopa kilio tunamficha chumbani akienuka tutakimbia sote. Sasa Mhe. Spika, nasema uwezo kwa wazanzibari tunao. Zanzibar tunaweza kesho kukomboka bila kutozwa kodi kwa wananchi mbali mbali haya mambo madogo madogo. Na hiyo nyaraka zipo sasa watuelezee kwa sababu serikali yote iliyokuwa inaongoza ni ya CCM na haya maandishi yapo, hakukuwa na mabadiliko ya Serikali mbili hizi. Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar zinaongozwa na chama cha mapinduzi. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninafikiri tufikie pahala wenzetu wafike pahala kwamba kuna suala la nchi na nchi, na hiyo ndio tutaweza kufikia yale malengo ambayo Waziri wa Fedha na Serikali hii kuweza kufanikisha.

Lakini mbali na hayo Mhe. Spika, hali ya biashara ukitizama ukurasa 20 namba 10 kuhusu biashara. Mhe. Spika, kuna wafanyabiashara kwa ushahidi kuna China na Uingereza ambao hawa ndio nina ushahidi nao. Leo China kuna tairi *linglone* na P 38 kutoka Ungereza ni PUTI ukenda China unaambiwa kuna *agent* Tanzania. Tunamwambia bwana suala la uchumi Bara na Zanzibar mbali, anasema sisi hatuijui Zanzibar tunaijua Tanzania maana Tanganyika. Sasa Mhe. Spika, matokeo yake basi, haki ya wazanzibari, haki ya wafanyabiashara wa Zanzibar na haki ya nchi yetu tunaikosa kwa sababu hawa mabalozi si waaminifu kwa kuitetea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa sababu yeye yuko pale kuitumikia Tanganyika, na kwa sababu hiyo nina ushahidi kwamba matairi ambayo humu ndani ya Baraza wakiwemo na wafanyabiashara tairi hizi zinatumika kwa gari za michanga na kokoto, inabidi mtu akitoa China ailete Dubai, ikitoka Dubai mbio ailete Zanzibar. Kwa hivyo gharama ya yule

mpandaji wa daladala abiria na yule mwenye gari zinapanda mara mbili, ili tu kwamba wenzetu pale tumezuiliwa kupata nafasi zetu kwa Zanzibar katika uhuru wa biashara. Na muungano wetu huu kila nchi na uchumi wake. Sasa ningeliomba Mhe. Spika, haya mawili ndio ninayoyajua mimi lakini kuna mengi Mhe. Spika, haki ya wazanzibari, haki ya wafanyabiashara, kwa sababu ya huu tuliokuwa na umoja wetu nasema sipingi muungano lakini nasema tunataka muungano uliokuwa na usawa. Nchi mbili zilizoungana sawasawa. Kwa hivyo hilo katika mchango wangu na kuwasaidia hao wenye dala dala hao wenye *grade* 750/16 kupata afueni katika biashara hizo za vitendea kazi.

Lakini isiishie hapo tu Mhe. Spika, tunakuja masuala ya mapato ya ndani. Tunaambiwa katika kitabu hiki ambayo Mhe. Waziri alielezea, ukurasa 20, ukurasa 25 namba 28, namba 39 tunaambiwa humu ndani leo kwamba ndugu zetu Tanganyika wamezuia bilioni 18 yale mapato ya *pay as you earn*. Sasa nasema Mhe. Spika, mapato haya yamechelewa Mhe. Spika, ukweli Wizara ya Fedha mtanganyika mmoja kazuia hizi pesa sijui kwa kiburi gani si kama pesa zimechelewa. Pesa zishatolewa Waziri Mkuu kimekaa kikao Mizengo Pinda alikuwa haoni sababu pesa hizi kwa nini zisije Zanzibar ambayo ni haki ya wazanzibari.

Matokeo yake Mhe. Spika, hizi bilioni 18 kuchelewa kufika kwetu hapa kuna suala la *devaluation* pesa zetu za thamani zimeanza kushuka na hatujui hizi pesa zitakuja lini na zimeshaamuliwa na ni haki yetu wazanzibari hiyo ni mwaka 2010/2011. Mhe. Spika, inanipa wasiwasi huu mwaka 2012/2013 hizi *pay as you earn* kwa wenzetu walioko Zanzibar tutalipwa lini wakati hizi pesa wakati tulikuwa tulipwe 2010/2011 hazikulipwa.

Sasa nafikiri ningelipenda kwa heshima na taadhima ni kaka yangu akatupa ufafanuzi uliokuwa wazi ili Baraza hili liweze kumsaidia. Na kama kuna suala la kuwajibika wenzetu wawajibike. Lakini wasituharibie muungano wetu wasione kwamba wao ni *champion* wa kufanya hivyo, tuna haki zetu, tuna taratibu zetu.

Mhe. Spika, maamuzi ya Tume ya pamoja katika haya haya ya fedha suala la muungano. Maamuzi ya pamoja Mhe. Spika, yalianza tokea 2006 mwezi wa Agosti. Ninasikitika kusema katika Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, maamuzi haya ya pamoja yameshakaa, yameshaamuliwa kuhusu namna ya uendeshaji wa muungano wetu. Ninasikitika mpaka leo wamekaa watu 14 wanatupangia Mhe. Spika, nataka kuwaambia hawa watu 14 wanaotaka kutupangia Wazanzibari tumefanya vidonda matumbo yetu. Kwa hivyo Mhe. Spika, maamuzi haya ya Tume ya pamoja maana yake hivi sasa hivi tumekaa tuna kazi kubwa sisi watendaji humu ndani. Maana yake Watanganyika wanatwambia Zanzibar mzigo, Wazanzibari tunawaambia Watanganyika mzigo.

Sasa masuala kama haya hayawezi kupatikana ufumbuzi kama viongozi hatukuwa wakweli, je, nia ipo? Sasa haya ni mambo muhimu sana, Tume tokea mwaka 2006 yashakamilika tupeni tuchangie sote hili suala ya muungano na pesa. Mimi nataka nikuhakikishie mbele ya Baraza hili pesa hizi za pamoja za muungano zinatosha nasema nina ushahidi nasema zinatosha kuendesha muungano na bado zinabakia katika pesa zetu.

Lakini tatizo kubwa linaonekana nini hapo Mhe. Spika, kwamba haya yote yametokana naweza kusema na ubabe au ukaidi, lakini ninachotaka kusema kwamba hekma, busara ya watendaji wetu ufikie kikomo katika kuheshimiwa muungano wetu.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi lakini kutokana na muda mimi kwa kuwa Mhe. Waziri alisema kuzungumzia magari ili yapatikane mapato. Sisi magari yetu ya Zanzibar yakenda hayaruhusiwi kutumika ili yapatikane mapato tunatia TZ. Kwa hivyo ningeliomba magari ya TZ huko yahesabike kama magari ya kigeni yapate nambari ya ZNZ. Kwa sababu magari yetu ya Zanzibar yanafanywa ya kigeni yanatoka Uingereza. Sasa inakuwaje magari ya Tanganyika yakija hapa yasifanywe ya kigeni. Mkuki kwa nguruwe kwa binaadamu mchungu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, katika hali hii tunayokwenda nayo mimi ingelifika wakati nasema kwamba nilizungumza miaka 20 watu hawakunifaham, cheti cha ndoa tukachukua Dodoma na mambo mengine mengi niliyoyasema. Kwa hivyo ninachotaka kusema kuwaambia viongozi, kueni wakweli, tutekelezeeni mimi kama ni mwakilishi wa Jimbo la Uzini, naunga mkono bajeti hii, naunga mkono muungano uliokuwa wa kuheshimiana hatujalazimishana wala tusilazimishane.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kushukuru kwa jumla na imani yangu kwamba kama kutahitajika, nyaraka zote, msaada wowote katika hali hii na ningeliomba viongozi wakuu, wakae kututolea matatizo haya, ili tuendeshe muungano wetu huu uliokuwa umeleta faida kwa pande zote mbili. Narejea tena jamani msitupangie tumechoka kupangiwa miaka nenda rudi. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi ya leo kunipa ruhusa kuweza kuchangia bajeti ya Mhe. Waziri wetu mpendwa, shemeji kama alivyoeleza katibu wake kipenzi na mimi nasema hivyo hivyo katibu wetu kipenzi kwa maelezo mazuri Mhe. Spika, kitabu hiki walichotuletea. Lakini kuna mambo tunawaomba radhi waweze tuwasaidie na wao katika kuleta.

Mhe. Spika, niliwahi kumuuliza Mhe. Waziri katika Wizara yako kuna mtu wa uchumi akanambia yupo, lakini mmoja tu nikaoneshwa katibu kipenzi akasema yupo huyu hapa. Mimi nilifurahi sana na mtu wa uchumi wenyewe mwanamama maendeleo ninashukuru sana lakini peke yake ana dhima kubwa sana ya Zanzibar kuitafutia uchumi lakini peke yake. Na ndio maana nikakiona kina kasoro kitabu hichi kwa sababu yeye ni mmoja tu.

Mhe. Spika, hivi vitabu nimesoma kwa muda baada ya kusomwa bajeti na mimi nikatafuta lebo yangu ya kuweza kujifundisha kusoma ili niweze kuichangia kwa ufasaha kabisa. Kuna mambo mengine nimeshafilisiwa na Maalim Rashid, mengine keshanifilisi Mheshimiwa wangu Raza lakini na mimi itabidi nipige nyundo mule mule ambamo tunawajibika.

Mhe. Spika, uchumi tunao lakini tunaendelea kuukalia. Ninamuomba Mhe. Waziri kabla sijaingia kwenye hiki kitabu, tuliambiwa tutakuwa na akaunti ya pamoja, kila mtu na akaunti yake katika mgao huu wa fedha za muungano. Kwanza naomba hilo alielewe aje anambie je katika akaunti yetu ya Zanzibar tuna kiasi gani? Lakini la pili Mheshimiwa Mwenyekiti wa Wenyeviti, alinishtua na kunishtua na kunionesha na ilibidi nivae miwani bila ya kutaka, tulikubaliana katika muungano masuala ya gesi asilia, lakini humu katika kitabu chako neno gesi sioni humu Mhe. Waziri sasa hapo nimepata mshtuko na tumeambiwa wenzetu wameshaanza kuchimba wanapata faida matrilioni Mhe. Raza anasema tungepata fedha hizo bajeti yetu isingekuwa kandamiza.

Lakini bajeti yetu inakuwa kandamiza kwa wanyonge kwa sababu kuna fedha ambazo ni muhimu hatuzifatilii. Mhe. Spika, ndio maana hivi vitabu tunaviandika tu kuandika ni kuandika lakini maudhui ya mambo ya kiuchumi hayamo humu kabisa. Humu asilimia kubwa ni upandishaji wa kodi tu ndio kitabu hiki hakuna chengine. Kumuonea mnyonge alipe bei hii, sijui kumuonea nani, kwa hivyo Mhe. Spika, tufike pahali tuwe wakweli viongozi wetu, mawaziri wetu muwe wakweli mnapokwenda kukaa kule kwa Mhe. Rais kwenye bango kitita basi tusimdanganye kabisa. Mhe. Spika, mimi nina imani sana kubwa amefanya Mhe. Rais kwa nia nzuri kuwa unapoanza kwenda kusoma kwanza unasoma kwenye ubao halafu unakwenda kwenye *practical* yenyewe katika *visiting site*. Sasa ningemuomba Mhe. Rais ende katika zile *site* zenyewe anazoambiwa kwenye bango kitita. Mhe. Spika, nikenda kwenye ukurasa wa tisa tunaambiwa kwa upande wa mfumko wa uchumi kifungu namba 18 kwa kweli hichi kitabu mimi wewe niachie tu Mhe. Spika, leo nipige tu hapa.

Mhe. Spika, hii hali ambayo tunayoogopa ogopa ndio inatufanya sisi tuingie umasikini. Mhe. Spika, Mheshimiwa kusema kukua uchumi hatumuoneshi mtu zile njia za kukua uchumi kila leo ukikaa wafanyabiashara wanalia wanakwambia wanalipa uchumi mara mbili ukuaji uchumi wenyewe mimi hapo ndipo ninaposhangaa. Mhe. Spika, jamani haya mambo mengine tunapokubaliana hebu tuyatekeleze yasilete athari katika nchi yetu sisi tunakuwa hatukubaliani nayo.

Mhe. Spika, tuna wawekezaji wa binafsi ukurasa wa 11, waekezaji tunawaonea tunawanyanyasa, serikali hatuwalindi, tunawabugudhi wakati tunawaita. Mhe. Balozi anakwenda Ulaya kule anasema njooni muekeze, anakwenda wapi huko wakifika hapa tunawanyanyasa tunawadhalilisha hatimae wanakopa mapesa, hatimae wananunua ardhi kwa wananchi wanawatajirisha wananchi, hatimaye inakuwa tunawazungukia tunawanyang'anya.

Mhe. Spika, ndio maana nikasema uchumi tunao lakini tunauharibu hatuutekelezi ipasavyo. Sasa hivi tuna wimbi la kuwafutia wawekezaji *land lease* kinyume na utaratibu, Mhe. Spika, *lease* hizo zinafutwa hazina *notice*, hazina barua ya kumpelekea muhusika, mtu anafutiwa tu basi tu. Mhe. Spika, tunapopita kwenye kamati kwanza nikushukuru sana Mhe. Spika, ujuwe una kamati zako mara hii mahiri kweli zinakwenda kwa mujibu wa kanuni na katiba, wala hupotezi pesa za UNDP kusomesha wajumbe wako ukasema aa, siku hizi zinatekeleza wajibu. Mheshimiwa hapa alisema Mwenyekiti wa Wenyeviti kuna maeneo yanafutwa yeye kasema tu mimi nina *document*s hizi hapa, yeye kaeleza mimi nina vitu hivi hapa.

Mhe. Spika, kuna mwekezaji huyu tunamwita Dubai ukanda wa Matemwe. Mhe. Spika, kampuni ya *Nahil* imefutwa kinyume na utaratibu hakuna *notice* sasa unafikiri uchumi huo utakwenda wapi Mhe. Omar bwana unatudanganya. Pato kama hilo umeshaanza kulifuta la mwekezaji unakuja kutwambia uchumi unakua. Sasa serikali inaingia hasara huyo akenda katika sheria za *world* huko inabidi serikali ilipe kodi iwalipe gharama zao tunaukuza tunauondoa uchumi? Kuna mwengine huyu hapa kafutiwa anailipa serikali kodi ya dola 11,565

amekwenda kupewa mtu analipa dola 500 Mhe. Spika, tunakwenda wapi. Kuna mtu analipa dola 13,000 Mhe. Spika, anakwenda mtu analipa dola 3,000 Mhe. Spika, tunakwenda kuchukua kodi ya Bandari shilingi elfu moja tuwatoze Mhe. Spika, shemegi mimi sikuungi mkono hii bajeti kweli. Kwa sababu vitu kama hivi ni vitu ambavyo vya kuonesha mahiri, lakini la kusikitisha anapewa mtu raia maeneo haya yanafutwa anafanya kampuni za ujanja halafu anauza anajitilia mapato kwa mabilion ya fedha leo tunahangaika hapa tunakwenda kwa wanyonge tunakwenda wapi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naungana mkono na Mwenyekiti wangu hapa si pahala pa kuunda kamati teule lakini itapofika pahali kikubali kifungu cha 117 yarudishwe maeneo hapa serikalini, serikali iinue uchumi. Mheshimiwa amesema waziri kuwa kuna mambo ambayo ya elimu ametuonesha pale, kuwa mimi nitawasomesha watu elimu ya juu, lakini katika elimu hiyo wataalam hamna ardhi, tunawaondoa watu kwa chuki tu ni wataalam wa ardhi wawili tu hakuna zaidi na akaniletee mwengine lakini katika kitabu hichi hawamo Mhe. Spika, kasahau Mhe. Waziri kusomesha wataalam wanaohusiana na mambo ya ardhi hawamo kabisa. Kama uwezekano upo Mhe. Waziri warejeshe wale hakuna tatizo chuki ya nini tusimuadhibu mtu kwa jambo la ubinafsi, tunapoteza hiba yetu, tutapoteza utajiri wetu. Mhe. Spika, kwa hilo suala mimi nasema hapo nitakuwa mkaidi au nilitewe kwa maandishi ili shemeji yangu niweze kumsaidia katika masuala kama haya.

Mhe. Spika, tunasema tunategemea mambo ya karafuu tegemezi, Mheshimiwa mimi naomba zao la karafuu tuliweke kama tegemezi la moja kwa moja. Mhe. Spika, sasa hivi nchi za wenzetu mipira sasa hivi ni biashara kubwa sana. Miche ya mipira tuipe kipa umbele kwa kuipanda katika ardhi yetu ni tija kubwa kuliko karafuu yenyewe. Lakini kwa kuwa watu hawatembei hawajui faida zake. Mhe. Spika, mimi ningeomba nalo hilo alione Mhe. Waziri alipe kipa umbele wapo waekezaji tayari na wapo tayari kutaka kutuletea neema hiyo.

Lakini Mhe. Spika, amesema humu kuwa sasa hivi umefika wakati imefanyika *study* ya watu wa umeme na kweli umeme kama alivyosema mheshimiwa wangu unapanda bei lakini utaratibu wa kupanda bei mpaka sasa hivi wananchi hawajaelimishwa, upandaji wake ukoje huo. Kwa hivyo mimi ninachoomba Mhe. Spika, tayari kampuni zimeshajitokeza ili kwa kuweza kufanya umeme huo.

Kwa mfano kuna kampuni imejitokeza suala la kuleta umeme wa taka. Sasa hivi taka zimezagaa katika nchi yetu na hawa watu walivyokuwa wazuri Mhe. Spika, hawataki hata pesa mbili za serikali. Mhe. Spika, sioni sababu sasa hivi tuna usiri wa viongozi wetu kutokuamua. Mhe. Spika, umeme tegemezi tusiutegemee, umeme wa ndugu hautufai sasa hivi imefika pahali hautufai kabisa tuwe na umeme wetu. Na umesikia hapa Mhe. Spika, mabilioni ya fedha hawataki kutupa, kodi hizi za umeme kila siku kukicha wanatuongezea tu wenzetu *TANESCO*. Kesho Mhe. Spika, watakuja kutuzimia tutafanya nini Mhe. Waziri wakati tumeshazimiwa na zogo kama hili lililokuwepo la masuala ya muungano.

Wananchi wanadai haki zao kwenye muungano. Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili suala la umeme hii kampuni tuikubalie haraka. Mimi ninakujua Mhe. Waziri huna mchezo wa mbali kwa jambo kama hili. Unawatakia mema wananchi wako.

Kampuni hii imeshafanya *study* imeshamaliza, imeshapata baraka za *ZIPA*, imeshapata kwa Mhe. Waziri Mwinyihaji Makame yupo hapo, aiangalie vizuri. Taka taka hivi sasa hazikai tena. Tuna usiri wa mambo yetu kuamua ndio maana tunafika pahali kunazuka zogo kwa sababu Mhe. Spika, hatuwi wakweli viongozi. Tunatoa mwanya kwenye vitabu, katika utendaji tuna-*delay*.

Mhe. Spika, kampuni hii hapa. Mimi nimeingia katika uchumi ndio maana nikasema Mhe. Spika, kitabu hiki utashangaa siingii sana kwa sababu ninakwenda kwenye masuala ya uchumi. Amesema maalim Rashid tuwe na viwanda, tuna chetu cha sukari kile pale mpaka leo kinadaiwa mamilioni ya fedha, kinadaiwa umeme wa mamilioni ya fedha, kile pale kimekaa tu baraka tu ya kupeleka watu mahakamani.

Mhe. Spika, tutafute mwekezaji aliyekuwa anaweza kutetea uchumi. Leo tunakuwa kwenye masuala ya ajira tunampa kazi Mhe. Haroun Ali Suleiman atafanya nini yeye peke yake? Hatumpi nyenzo kwa sababu Mhe. Haroun tukimwambia kiwanda kipo kinafanya kazi Maalim Haroun anapeleka watu, samahani kwa kutumia jina lako ninalipenda jina lako.

Sasa hiyo ndiyo hali Mhe. Spika, kuwa ni lazima hivi sasa tufufue uchumi kwa kupitia viwanda, sio tufufue kwa kupandisha kodi. Kodi Mhe. Spika, tunawaonea wanyonge. Mhe. Spika, kiwanda hiki kikija hapa, hakikisha usafi utakuwepo, huoni chupa chafu, tairi mbovu utakuwa huzioni na kiwanda chake basi hiyo nyumba yake inakaribia na Ikulu kwa uzuri wake, wala asikudanganye mtu kuwa inaharibu mazingira si kweli. Ukiambiwa

hasa eeh! Bwana kiwanda chenyewe ndio hiki basi utasema aah! Mshimba muongo hii Ikulu bwana! tena ya Marekani.

Sasa Mhe. Spika, watu watapata ajira, watapata kuuza hizi chupa kama zinavyouzwa hivi sasa, gari wanakuja nazo wao wenyewe. Sasa mambo kama haya namuomba sana Mhe. Waziri kuwa ni lazima tuyape kipaumbele ili Waziri wa Biashara aweze kusaidia ili aweze kumiliki.

Lakini Mhe. Spika, tuna viwanda, nilisema siku moja hapa kiwanda kile cha kutolea kuku Maruhubi sijajibiwa vizuri, kinatiwa mule maghala ya saruji. Namuomba Mhe. Spika, hivi viwanda jamani serikali ivirudishe katika ile mantiki iliyokusudiwa. Saruji na utengenezaji wa chakula cha kuku ni vitu tofauti. Hebu tupewe sababu hasa Mhe. Waziri, sababu gani inayopelekea kugeuza mazingira ya kile kitu ambacho tulichokikusudia.

Mhe. Spika, kwa hivyo naomba sana kwa sababu naona kama unataka kuniweka, lakini usiniweke naomba kidogo muda wangu nimalizie.

Mhe. Spika, kwa kuendelea tena kama nilivyokwambia hapa kuwa bajeti hii kwa inaongeza umaskini haipunguzi umaskini. Lakini mheshimiwa amesema kama kuna vitu amevipeleka *ICU*, mimi ninakubaliana naye Mhe. Spika, umepeleka kwa macho yangu, *fitting* tayari ile ya *oxygen*, ile mashine ya kucheki damu hapo kwa hapo tayari ipo lakini *theatre* Mhe. Spika, sikubaliani nayo. Kuna nguo mbovu.

Mhe. Spika, nikwambie kule ni roho zaidi pamoja na *ICU*, halafu tunakwenda katika masuala ya *scheme of service*, Mhe. Waziri umetwambia utakwenda katika mambo ya kada lakini mheshimiwa mpaka lini? Wafanyakazi wanaumia Mhe. Spika, hawapati haki zao, *ma-nurses* hawapati haki zao lakini madaktari wanapewa, kama wapo hapa wananisikia hapa.

Mhe. Spika, *nurses* ni wafanyakazi pamoja na *ordelies* kuliko huyo daktari. Daktari anapigiwa simu kwake ni mzuri, siwezi kukataa kwa sababu ni muhimu lakini tunapokwenda kuwasaidia na wao tuwaone na ma-*nurses* anaanza *treatment* kabla ya kufika daktari lakini hana *night allowance* hapewi kwa nini.

Mhe. Spika, pamoja na kusema tunatoa kipaumbele kwa hospitali bado Mhe. Spika, kwa sababu leo daktari wa *specialist* wa mifupa hawapo hivi sasa. Nendeni maana nyinyi hamutembei hospitali, ndio ninakwambieni munamndanganya Rais. *Wallahi* kwenye bango kitita munamdanganya sana Mhe. Rais.

Mhe. Spika, kule sehemu ya *laboratory* kuna mashine ya kuchekia kensa, aah! *Old model*, pale tumepigwa changa la macho. Mashine hazifai ng'o pesa chungu nzima zimeshapotea. Hebu undeni tume wenyewe Mawaziri mukaangalie kile kitu kule? Halafu leo munakwenda kumwambia Mhe. Rais tumenunua mashine *model* ya kisasa. Mhe. Spika, pale watu wamechakachua pale, ukweli tuuseme.

Mhe. Spika, mashine haziendi na wakati kule tutauwana, mtu ataambiwa ana kensa kumbe hana kensa. Hilo ukweli tuambizane Mhe. Spika. Kwa kweli bado hospitali hatujawatendea haki, bado wafanyakazi wote Wazanzibari hatujawatendea haki kwa sababu fedha tunazo, nimesema mimi tuna 4.5 tungeipata ile tu, basi mshahara wetu ungekuwa katika hali ya juu. Lakini ile sijui inapitapita vipi na wala hatujapewa taarifa kwenye kitabu jinsi tunapewa aidha kwa mwezi au kwa mwaka.

Lakini Mhe. Spika, kwa kumalizia inakuwaje wizara si ya muungano lakini kuna jambo la muungano wana-monitor wao, mimi hapo inanishangaza sana. Wizara za muungano zipo lakini kwenye gesi imepelekwa kwenye wizara sio. Hivi kweli unategemea utapata mapato hapo? Ndio maana tukashindwa kupata mapato, kwa nini Mawaziri munashindwa mukenda kule kwenye hoja hizo kulisema hilo suala, nipelekeni mimi tukaliondoe.

Mhe. Spika, kule hakutaki usomi. Halafu mimi kuna kitu ninataka nikiombe Mhe. Waziri wa Sheria aniunge mkono. Tujaribu kutafuta chombo cha Mahakama kitakachoweza kuwasaidia hawa wawekezaji wa kizungu wanaokuja, iwe *independent* na Mahakama hii kwa sababu moja, maana ya kukwambia hivyo, ina-*delay time* kwenda katika Mahakama hii, mpaka hivi sasa kuna kesi mpaka si chini ya 18 za *land lease* zilizofutwa.

Lakini ikiwa *independent*, wale katika Mahakama yao tayari inakuwa ni tatizo dogo tu na hili uliangalie Mwanasheria. Hili Mhe. Spika, naomba nalo liangaliwe nalo, kuwe na *independent* za sheria ili kuwasaidia wawekezaji kwa sababu kila siku ina-*increase* in *numbers* yanaendelea kufutwa tu Mhe. Spika. Nikikuonesha utalia machozi hapa Mhe. Spika, haya hapa kibao yamefutwa kinyume na utaratibu, tunatoa ardhi kwa ajili ya uchumi ili wananchi wetu waondokane na umaskini, tuache hizi bajeti tegemezi kila siku tutakuwa tegemezi tu.

Juzi Waziri anataja hapa tunapiga kofi, nani katusaidia tunapiga kofi papapa! Mhe. Spika, hii tuondokane nayo, tuki-*stick* katika mambo ya uchumi tukenda vizuri basi ninaamini tutakuwa na tegemezi hata siku moja wala haitofika kupiga kelele za muungano na vipi na vipi, ndio kwanza Zanzibar tunaendelea na uchumi wetu kama ni Zanzibar. Mhe. Spika, hii ninasikitika sana.

Kwa hivyo hii ninachoomba Mwanasheria lazima mukae na Baraza lako au huko kwa Mhe. Rais mulipeleke hili. Mhe. Spika, tunanuka kuwadhalilisha wazungu, mimi ninaona vibaya sana Mhe. Rais au Mhe. Makamo wa Pili wa Rais akenda nje, huwa ninatizama televisheni, mimi mwenyewe *professor* nimekwenda huko nchi za nje Europe wanataka kuekeza ninashindwa kuwaambia kwa sababu nimeshaona mambo kama haya na mimi si nitatiwa kamba. Leo nitamleta nitamwambia njoo kesho kwa sababu nina hii miradi mitatu Mhe. Waziri wa Fedha ameshaahidi yule pale tayari, nina miradi mitatu ya kuisaidia Zanzibar.

Mradi wa kwanza ni huu, mradi wa pili ni hilo suala lililozungumzwa la mafuta watu wa Afrika ya Mashariki nzima watakuja kuchukua mafuta hapa. Ananijua yule bwana Mhe. Waziri wa Fedha, mimi sikwenda kutizama majengo, nimekwenda kutafuta uchumi kuuleta ndani ya Zanzibar na ndio maana ninaingia mpaka ndani ya sheria kuitafuta ya kuwaokoa hawa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninaomba haya tunayozungumza hapa Mawaziri muyachukue muyafanyie kazi, na ndio maana tunakuwa kwenye bajeti za mara hii tunakuwa taabu kupitisha kwa sababu munatuona kama tunapiga kelele na nini, lakini si hivyo Mhe. Spika, sasa tutazikamata wizara hadi wizara mpaka tuhakikishe yaliyokusudiwa yanapatikana.

Mhe. Spika, tumeambiwa tusiwasemee wananchi lakini kuwasemea wananchi ni wajibu wetu. Mhe. Spika, tunaambiwa gari zinatoa moshi, hebu Mhe. Omar ziachie, wawekee *condition* walete gari mpya. Hizi gari ushaambiwa zina gesi, halafu unakwenda kula mafuta halafu unakwenda kula tiba ndio utapona hivyo? Huwezi kupona. Sema hasa gari za mwaka fulani sasa Zanzibar zisiingie, ziingie za mwaka fulani au zile zile ziachie ziendelee na biashara zao usiwatoze kodi, usiwazidishie, pahala pa kupata kodi tunapo pakubwa.

Sasa haya Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Kitope ninawasemea ninaambiwa nisiwasemee lakini hapa ndio pa kuwasema, sisemi pengine popote, nikisema pengine nitaambiwa kosa lakini hapa ndio pahala husika. Wanachosema haki zao kwa mujibu wa Katiba wapewe. Suala la ajira, mara hii lazima ajira ziendane na mikataba tujielewe.

Ninawashukuru watu wa ZIPA Mhe. Spika, wana utaratibu pale hivi sasa wameweka *registration book*, wanajua hivi sasa wamewahudumia wangapi, wa ndani wangapi na na wa nje wangapi, Sasa na wao ofisi husika wanapokuwa tayari wanatengeneza mikataba watuekee *data base*, tuhakikishe.

**Mhe. Spika:** Umebakiwa na dakika tano tu kumaliza hotuba

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Hapo umenipa nyingi Mhe. Spika, ninakushukuru sana. Watueleze mara hii tumeajiri wangapi, wa nje wangapi na wa ndani wangapi, ili iweze kutusaidia wananchi kukaa na umaskini, kila siku kukicha wakalia kwenye vibaraza na serikali yao ipo, viongozi ndio sisi wasemaji wao. Tutawasemea wananchi.
Mhe. Spika, lakini nimalizie suala la ukurasa wa mwisho ambalo Mhe. Waziri ameligusia, suala la mambo ya muungano.

Mhe. Spika, hili suala hivi sasa hakuna asiyejua watu wanapiga makelele, watu wanazozana. Mimi ninataka kuwaambia watuachie wenyewe. Madhali wametuchagua sisi tunaona Mhe. Raza kaonesho mfano tu hapa na ndiye wa juzi tu, mwanafunzi kawa mwalimu leo. Sasa na sisi walimu tutakuwa walimu ndani ya walimu, watuachie sisi wana siasa wakongwe tutalimaliza hili suala wala wasiwe na wasi wasi watulie. Kwa sababu kuna mambo ambayo njia zipo ameshazieleza Mhe. Raza *automatically*, mtu akuambie hili anatia *brief case* anakimbia, ndio maana nikakwambieni mukenda katika kero zile musiende wasomi watupu tuchukueni chakaramu kama sisi tutalimaliza mara moja.

Mhe. Spika, si masikhara kwa sababu pale mimi utaniambia nini, panakwenda kusomeshwa *what is biology* pale, wapi na wapi na pale, tunakubaliana jamani tumesema hivi biashara ilipwe kodi moja TRA basi mchezo umekwisha. Lakini sikubaliani kwenye *table* twende *physically* kabisa katika ile ofisi husika, ndipo manyago yanapofanyika. Nyinyi mukishakubaliana mukiondoka pale mushachukua *allowance* zenu munakwenda zenu, wahusika wazunguka wanakataa kutekeleza yale yanayohusika.

Lakini tukiwa na mfumo mzuri, tumeshakubaliana pale na saini, Mhe. Spika, haiwezi kuwa namna hiyo na wala isingefika zogo namna hivi. Isifike watu wakataka kudai haki zao kwa mabavu. Jamani haki itatoka kwa utaratibu tutulie kwa sababu leo mabilioni ya fedha tunayadai katika Serikali ya Muungano haiwezi kutuletea. Sasa ikiwa kama haiwezi kutuletea tena!

Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa hayo niliyoweza kuchangia na kunipa muda mrefu. Watu wamenisikia na kama nilivyosema kitabu chetu hiki kimebeba sana masuala ya kodi, mambo ya uchumi Waziri wangu atafuatilia na ataeleza ipasavyo.. Lakini na haya tuliyoyasema kwenye vitabu hivi tunawangojea wenye wizara zao husika kwa sababu kuna mambo mengine mpaka leo Wakuu wa Mikoa hawajaapishwa fungu hili wamo, naona tabu mimi Mhe. Spika, tuwaapisheni wale wale, twende kwa mujibu wa Katiba yenyewe.

Leo Mkuu wa Mkoa akiapishwa anaingia kwenye fungu hili, lakini leo Mkuu wa Mkoa hajaapishwa niseme ninaunga mkono asilimia mia kwa mia. Mhe. Spika, ninaona pana utata hapo. Hili si tatizo ni sheria tu. Wakuu wa Mikoa wamo ndani ya Katiba, tuwapishe tuwapitishie fungu lao wakatumie fedha zao kwa mujibu wa utaratibu lakini leo hawamo humu.
Kwa hayo machache Mhe. Spika, ninaunga mkono (Makofi).

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla**: Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuweka tukiwa hai na wazima mpaka tukafika siku ya leo tukiwa tunajadili mipango yetu ya nchi.

Lakini pili naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu sana na mimi kuweza kutoa mawazo yangu japo machache katika mipango hii ya nchi.

Mhe. Spika, mimi ninataka nianze ukurasa wa 47 wa kitabu cha hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Mhe. Waziri katupa mwelekeo mzima wa bajeti utakavyokuwa katika mwaka huu wa fedha 2012/13. Mhe. Waziri ametueleza kuwa makisio yote yatakuwa ni Shilingi mia sita na arobaini na nane nukta tisa bilioni, ambapo mapato ya ndani yatakuwa ni shilingi mia mbili na thamanini nukta saba bilioni, lakini kuna bakaa ambalo halikutumika, na hili naomba sana aje anieleze kwa nini halikutumika mwaka uliopita ambapo tumefanya makisio kwamba yatumiwe lakini hakutumia.

Lakini ukichanganya na bakaa hilo tunakuwa na mapato ya ndani shilingi milioni mia mbili na thamanini na sita na nukta sita. Lakini mahitaji yetu ni shilingi mia sita na arobaini na nane nukta tisa bilioni, kwa hivyo nakisi ya bajeti ni shilingi mia tatu na sitini na mbili bilioni nukta tatu ndivyo alivyoeleza mwenyewe na ndivyo ilivyo.

Sasa kati ya nakisi hii washirika wetu wa maendeleo wao watachangia mia mbili na tisini na tatu bilioni. Sasa kuna nakisi hapa ambayo imebakia ya shilingi ninadhani hamsini na tisa nukta mbili bilioni.

Hizi serikali inatafuta pahali pa kuzipata. Sasa *proposal* ya Mhe. Waziri yeye kaona njia nzuri ya kuzipata ambayo mimi siiungi mkono ni kuzidi kuwakamua wananchi wetu. Kwa hivyo wananchi wetu kwa mwaka huu wabinywe mpaka watoe shilingi hamsini na tisa bilioni.

Mhe. Spika, unapojaribu kuongeza kodi basi ile azma yako nzima ya kuwapunguzia ukali wa maisha unaipoteza. Kwa hivyo badala ya kupunguza ukali wa maisha, mimi ninatafsiri bajeti hii sasa ni kuongeza ukali wa maisha kwa wananchi.

Mhe. Spika, nchi inapokuwa inahitaji pesa inatumia njia ya kodi ya wananchi na kwa kweli ndio mapato ya serikali yanapotoka. Lakini nilisema siungi mkono kwa sababu zangu. Siungi mkono kwa sababu mimi bado ninaamini vyanzo vyetu vya mapato tulivyonavyo Mhe. Spika, vinaweza kuziba karibu kwa asilimia thamanini ya hili pengo ambalo tunalo.

Mhe. Spika, tatizo linalojitokeza na ni changamoto ambayo mimi ninathubutu kusema kwamba labda serikali hii ya CCM wameshindwa kuliziba, naomba nirejee hapa kwa sababu mwalimu wangu Haroun Ali Suleiman kaniambia nirejee. Ninasema kuna pengo ambalo serikali hii ya CCM inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi inayofuata sera za ilani ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kuziba.

Mhe. Spika, ninasema hivi kwa maana yangu. Hata juzi Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha bajeti yake, alisema bajeti hii ni ilani ya Chama cha Mapinduzi, ndio mimi nikasema hivyo kwa makusudi. (Makofi).

Maana kama angesema ni ilani au ni mipango ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na mimi ningesema hivyo hivyo, lakini kasema ni  ya Chama cha Mapinduzi, kwa hivyo na mimi ninasema kwa kuwa ni Chama cha Mapinduzi basi wameshindwa kuziba. Naomba nisieleweke naanza kufanya uchochezi hapana, kaanza Waziri.

Mhe. Spika, tunaweza ku-cover hili pengo la nakisi ikiwa kutakuwa na usimamizi mzuri wa kodi, usimamizi wa kodi haujaridhisha kabisa. Kuna mapato Mhe. Spika, ya makusanyo ya kodi yanavuja bado. Kuna mwahala usimamizi ni mbovu, kuna mapato hayakusanywi mpaka leo katika nchi hii.

Kwa hivyo hii kama tutaisimamia vizuri, nimeona mipango katika mwelekeo wa hali ya uchumi, ni mipango hii, lakini mipango hii kila mwaka tunaambiwa hivyo hivyo. Lakini ukija kwenye utekelezaji hamna kitu. Kwa hivyo ni mipango ambayo mimi naisoma lakini siiamini.

Kwa hivyo usimamizi wa ukusanyaji wa kodi bado hautoshi. Mhe. Spika, vyanzo vyetu vinavyokusanya kodi havijasimamiwa vizuri na mimi ninathubutu kusema hapa uwezo wao wa kukusanya ni mkubwa zaidi kuliko kile ambacho amekusanya. Vyanzo vipo lakini la pili Mhe. Spika, tunakabiliwa sana Wazanzibari na hili ni tatizo ambalo sijui kama sisi Wazanzibari tutalipatia dawa gani, lakini tunakabiliwa sana na tatizo la kutokuwa na uaminifu wa watu wetu, yaani watendaji wa serikali kwa jumla. Kwa sababu si waaminifu basi hilo ni jawabu tosha kwamba hatuwezi kupata pesa za kutosha kwa vyanzo hivi tulivyokuwa navyo.

Mhe. Spika, taarifa tunazo kwamba watalii ambao wanaoingia hapa nchini ambapo mtalii akija hapa nchini analazimika kulipa ile kuingia katika nchi yetu tu. Kwa hivyo idadi ya watalii wanaokuja hapa nchini kwetu ni tofauti sana na idadi inayoripotiwa na watendaji wetu. Na hii bahati mbaya sana serikali inashindwa kuisimamia. Kwa mfano wanaweza wakaingia watalii mia tatu kwa siku lakini idadi itakayoripotiwa serikalini pengine inaweza kuwa ni mia mbili hamsini. Sasa hawa hamsini ambao wamelipa pesa zinakwenda wapi?

Sasa Mhe. Spika, mimi ninadhani Mhe. Waziri angeitumia hii mipango yake aliyoipanga huku, kapanga mipango mizuri ya kugawa maeneo kama wanavyogawa maeneo watu wa umeme hivi sasa. Watu wa umeme kila mtu ana sehemu maalum ya kukusanya mapato ya umeme na yeye kagawa nimeona humu. Lakini jee usimamizi utakuwepo. Mimi naomba sana hii mipango ifanyiwe kazi kwa vitendo.

Lakini jambo la pili ambao linaikosesha serikali uwezo ni matumizi yasiyozingatia uhalisia au niseme ni ubadhirifu wa pesa za serikali. Mhe. Spika, hili ninasema lipo kwa wingi sana na linaathiri na linaathiri sana maendeleo ya nchi yetu.

Siku moja Mkurugenzi akishakuwa hana pesa mfukoni humwambia hebu nipangie siku saba za kwenda Pemba, hana kazi yoyote ya maana. Mhasibu anampa mkurugenzi siku saba za kwenda Pemba leo na kesho anarudi, zile siku saba anakuja kuzitumia hapa Unguja kwa shughuli zake lakini pesa keshatia mfukoni, kwa hivyo katayarisha pesa za mara moja.

Mhe. Spika, nchi hii ina wakurugenzi wangapi, nchi hii ina makatibu wakuu wangapi? Sasa huko ndiko pesa zinakopotea. Sasa jamani achukue mkurugenzi tukamkamue mlipa kodi? Ndio hoja yangu ilipo. Mimi ninadhani si halali. Mhe. Waziri ana changamoto kubwa ya kusimamia pesa za serikali, matumizi ni mabovu. Sasa tusiwaonee watu bure.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo pia Mhe. Waziri au sisi sote kwa jumla hapa, hili si la Waziri peke yake ni la serikali nzima, kwa kweli mgao wa mapato ya muungano. Hili Mhe. Spika, halijafanyiwa kazi ipasavyo au labda wenzetu wanatufanyishia kwa makusudi. Mhe. Spika, kaeleza Mhe. Waziri mwenyewe hata ile *income tax* ya wafanyakazi wa taaasisi za muungano ambao tumeshakubaliana kwamba ziingie katika Serikali ya Zanzibar hazikuingia ni shilingi *eighteen millions* hazijaja hapa na jawabu ya msingi sisi hatujaipata.

Kuna fedha kazitaja hata Mhe. Hamza Hassan Juma shilingi mia tatu na sabini na saba bilioni za elimu ya juu, ukizigawa hizo kwa 4.5 Wazanzibari percentage tunatakiwa tupate *eighteen millions*, nazo hizo hatuzipati, ukiuliza utaambiwa suala la elimu ya juu ni mambo ya muungano? Hatutaki tunataka tutumie wenyewe.

Kwa hivyo, kuna mapato ya gesi mwaka wa kumi na mbili huu Watanganyika wanachimba gesi hebu atwambie toka Watanganyika walipochimba gesi ile 4.5 yetu

**Mhe. Spika:** Tanganyika kwa maana ya Tanzania Bara. Usione taabu kulitumia neno hilo.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla**: Tanganyika kwa maana ya Tanzania Bara.

Mhe. Spika, mapato ya gesi hebu Mhe. Waziri atwambie hii miaka kumi na mbili toka Tanzania Bara waanze kuchimba gesi ni shilingi tumezikosa katika gawio la 4.5 iko wapi, si tungezipa hii nakisi ya bajeti yetu.

Mhe. Spika, unajua Mwenyezi Mungu siku zote anapokupa neema katika nchi na Mwenyezi Mungu kwa hekma yake kila nchi kaipa raslimali, na raslimali ile tunatakiwa tuitumie. Huu ni mwaka wa ngapi toka 1963 mpaka leo Wazanzibari tumeshindwa kufaidi mafuta yetu, tusimamie hilo. Tusimamie hilo na tumebadilisha Katiba sisi hapa, wenzetu wameshindwa kwenda katika Bunge kubadilisha mstari mmoja tu wa kusema mafuta si jambo la muungano. Hivi leo tungekuwa na mafuta yetu sisi nakisi kama hii si tungeiziba. Kwa nini tunawatoza kodi wananchi wetu tunawakamua.

Mambo kama haya Mhe. Spika, ndiyo yanayosababisha *volcano* katika nchi yetu. Mimi ninaamini Wazanzibari hawakatai umoja lakini umoja wa kufaidi mmoja na mmoja akabinywa hayupo anayeutaka. Sasa mimi ninafikiri tungezungumza muungano inaonekana ni kama jambo la kisiasa, lakini katika uhalisia wake Mhe. Spika, muungano si jambo la kisiasa, muungano ni jambo la kiuchumi kwa sababu muungano huu unatuumiza sisi kiuchumi. Mimi ninadhani Mhe. Spika, Wazanzibari wana haki ya kuujadili muungano kwa nguvu zao zote.

Mhe. Spika, naomba sasa niingie kwenye ajira. Na mimi kama Mhe. Waziri alivyoandika katika kitabu chake hiki cha mwelekeo wa uchumi kwamba mipango mizuri ya kiuchumi ni ile ambayo inalenga kuimarisha ustawi wa nchi, lakini na kuimaisha ustawi wa wananchi wake. Sasa moja katika mambo muhimu sana ya kustawisha wananchi ni ajira.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amegusagusa katika kitabu chake ninafikiri ukurasa wa kutoka 37 mpaka 38, na ukisoma kitabu cha mwelekeo ya hali ya uchumi ukurasa wa 32 mpaka 40 imeelezea kwa urefu sana mipango ya ajira. Lakini tumeelezwa hapa kwamba ajira atakazozalisha kwa mipango ile aliyoipanga mule ni ajira 2000.

Kapanga mipango ya miradi 7 Mhe. Spika, ambayo itagharimu yote kwa jumla shilingi mia nane na ishirini na moja milioni na laki tatu. Sasa mimi ninachotaka kujua hapa ni kwamba ajira hizo 2000 ambazo Mhe. Waziri katwambia wananchi wanazipata kwa mwaka huu, ni ajira za aina gani. Maana ajira zipo nyingi. *Concept* ya ajira ni ile kazi ambayo anafanya kupata riziki yake, hiyo ndiyo ajira.

Lakini ajira imegawika mafungu mawili mpaka matatu. Kuna ajira serikali inaajiri watu moja kwa moja. Sasa mimi nilitaka atwambie katika hawa watu 2000 ni wangapi wataajiriwa na serikali moja kwa moja na pia atwambie kati ya hawa watu 2000 wataajiriwa katika kampuni za watu binafsi. Lakini pia atwambie katika watu 2000 hawa ni wangapi watajiajiri wenyewe kwa uvuvi, kilimo na mambo mengine ya biashara kwa sababu ni muhimu hilo.

Hasa Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninadhani katika utekelezaji bora wa majukumu tujue ilipaswa tujue hasa katika nchi yetu tuambiwe wazi wazi ndani ya takwimu ya Mhe. Waziri kwenye kitabu chake cha bajeti, ni watu wangapi katika nchi yetu hawana ajira wote tuwajue na kati ya hawa wataajiriwa wangapi. Halafu tuone ni wangapi tunawahitaji na wao kuwapatia ajira.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninataka niseme suala la ajira tumekabiliwa na manung'uniko makubwa. Katika kipindi ambacho serikali imebana kuajiri ajiri, ajira zilikuwa zinatoka katika zile sehemu ambazo serikali haina budi. Lakini tumekuwa tumekabiliwa na manung'uniko na manung'uniko mengi yanakuja kwetu sisi Wawakilishi.

Inaonekana Wawakilishi ni suluhisho la matatizo ya Wazanzibari. Lakini ni kweli kwa sababu sisi ndio tunaowasemea watu ili kuiambia serikali itekeleze yale mahitaji ya watu. Kwa hivyo wananchi hawakosei kutujua sisi.

Sasa moja katika mambo ambayo wananung'unika vijana hasa kwa ajira za serikali. Wanatwambia kwamba ajira zinatolewa kwa kujuana mno. Mhe. Spika, kama ami yako, kaka yako si waziri, si Katibu Mkuu, si Mkurugenzi, si Meneja wa shirika huwezi kupata ajira. Na ukifanya utafiti ajira zinatokea katika miaka miwili mitatu iliyopita, kila utakayemtafuta huyu kaajiriwa vipi, utakuta basi jamaa yake basi ni mkurugenzi au mtu wa aina hiyo.

Sasa mimi ninajiuliza Mhe. Spika, ikiwa mtu mlalahoi maskini wa Mungu, baba yake si waziri, si Katibu Mkuu, si Mkurugenzi hivyo jamani yeye ndio asiajiriwe. Mimi nilikuwa ninadhani, ametaja Mhe. Waziri kuna sera ya ajira, nilikuwa ninadhani sera ile ya ajira hebu ifanyiwe kazi kwa vitendo. Mtu aajiriwe kwa sifa zake.

Mhe. Spika, kuna watu wenye sifa kutokana na matangazo ya ajira yanayotolewa hasa wameachwa, wamechukuliwa watu sifa zao hata hazimo katika lile gazeti lililotangazwa, na wameajiriwa *just* tu kwa sababu kaka yake ni mkubwa. Hii inauma sana na kwa kweli ninaomba sana watendaji wa serikali wanisikie hapa, hapa mwaka huu tutakuwa wakali kweli kweli, haiwezekani bwana maskini ya Mungu asiajiriwe kwa sababu hana mkubwa mkononi bwana.

Jengine Mhe. Spika, kuna hizi ajira za muungano zinazotolewa. Ajira hizi nazo zina upendeleo wa hali ya juu. Katika vyombo vya ulinzi kama Polisi na Jeshi la Ulinzi. Mhe. Spika, kunakuwa na mgao maalum ama ni kanuni au ni sheria, mimi sijui lakini kuna mgao maalum hizi ni za Tanzania Bara na Zanzibar. Lakini mpaka leo ajira za Zanzibar wanakuja kuzichukua wenzetu wa Tanzania Bara.

Ninashukuru Mhe. Spika, kwa kuwa muda haupo tena, nilikuwa nimebakiwa na *point* moja tu lakini unisamehe na naomba niishie hapa.

**Mhe. Spika**: Nikushukuru sana Mhe. Abdalla Juma Abdalla. Muda kwa kipindi cha asubuhi umemalizika, lakini kabla hatujatawanyika basi kuna tangazo moja dogo.

Nimeombwa au nimetumwa niwatangazie waheshimiwa wafuatao wakutane katika ukumbi wa juu. Nao ni:-

1. Mhe. Salma Mussa Bilali
2. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
3. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
6. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

Mwenyekiti wa Uwawaza anataka kuzungumza na nyinyi Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe, sasa ninaakhirisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Spika, awali ya yote naomba niitumie fursa hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutupa uhai na afya ili tukaweza kuhudhuria bajeti nyengine hii ya serikali.

Pili shukrani zangu naomba nizielekeze kwako Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii angalau na mimi kuchangia katika bajeti hii ya serikali, na kuwa mchangiaji wa kwanza katika jioni hii.

Mhe. Spika, leo tunaingia katika mjadala wa bajeti ya serikali. Tunapozungumzia bajeti ya serikali, *twabaan* tunazungumzia uchumi wa nchi yetu. Hali ya uchumi ndio inayopelekea serikali kupata mapato na baadae mapato hayo yakaandaliwa utaratibu maalum wa kutumika chini ya idhini ya Baraza hili.

Mhe. Spika, tunapozungumzia uchumi, hatutoisahau miaka ya 2000, katika miaka ya 2000 nchi yetu iliingia katika mageuzi ya kiuchumi. Tutakumbuka kwamba mwaka 2002 serikali ilianzisha mpango wa kupunguza umaskini unaoitwa ZPRP na baadae serikali ikaja na mpango wa MKUZA I na MKUZA II ambao sasa hivi tunaendelea nao.

Mhe. Spika, katika kipindi kile cha tathmini kwa mpango ule wa ZPRP, uchumi wetu ulioneshea kuwa na afya yaani ulikuwa. Wastani wa kukuwa kwa uchumi kwa miaka ile minne au mitano, uchumi wetu ulifikia asilimia 6.3. Halikadhalika mfumko wa bei ukawa ni kwa asilimia 6.1. Ilivyoonekana kufeli kwa mpango ule wa serikali wa ZPRP, serikali ikaanzisha mpango huu wa MKUZA ili kufanya marekebisho ya ZPRP ambayo ilionekana kufeli.

Mhe. Spika, katika tathmini tunapochukuwa wastani wa ukuwaji wa uchumi katika mpango wa MKUZA, imeonekana uchumi kukuwa kwa wastani wa asilimia 6.1, ikilinganishwa na asilimia 6.3 katika kipindi cha mpango wa ZPRP. Kadhalika tathmini inaoneshea kuwa mfumuko wa bei uliongezeka kwa asilimia 12.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ni lazima tujiulize kwamba ikiwa MKUZA ambao imekuja kwa kurekebisha mpango wa serikali, imeoneshea ukuwaji wa uchumi ni mkubwa zaidi ukilinganisha na ule mpango ambao umefeli. Lakini vile vile hata mfumko wa bei nao unaonekana ni wa juu zaidi ukilinganisha na ule mpango wa awali wa ZPRP. Hiyo ni kuoneshea kwamba MKUZA nao haukuwa na jawabu kwa suala la kuimarisha uchumi wa Zanzibar.
Kwa msingi huo Mhe. Spika, ni dhahiri tumeona kwamba mpango wa kukuza uchumi haukufikia pahala. Sasa kwa vyovyote vile serikali italazimu kukaa tena kwa mara nyengine kutafuta muarubaini wa tatizo letu la uchumi. Kwa kuwa ZPRP ilifeli ndio maana ukaletwa MKUZA, lakini MKUZA nao umefeli zaidi kulikoni ule mpango wa awali. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni wakati sasa wa serikali kukaa na kufanya tathmini ya kina, ikiwashirikisha wawakilishi wa wananchi ili kutafuta muarubaini wa tatizo letu la uchumi.

Kwa tathmini yangu mimi Mhe. Spika, nadhani mambo manne ni muhimu sana yazingatiwe. Kwa kuwa uchumi wetu unaonekana hauendelei, changamoto zinazoukabili uchumi wetu huo ni nne. Kwanza Mhe. Spika, uchumi wetu haukuenea kwa watu waliowengi. Ni lazima tukubali kuwa uchumi wetu haukuenea kwa watu wengi. Uchumi wetu uko kwa wachache, tena hao wachache wenyewe ni wageni katika nchi. Sasa hiyo maana yake ni nini. Hiyo maana yake ndio maana ukaona kwamba kadiri uchumi unavyoambiwa umekuwa, lakini hauonekani katika uhalisia wa hali za maisha ya wananchi wetu na hata unapofika pahala ukaona kwamba kwa kugawa pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja, unapofika pahala unaangalia hilo pato kweli mtu wa kawaida anaweza akawa na kiwango hicho cha fedha katika kipindi cha mwaka, utaona kwa kweli haiwezekani, kwa sababu mtu wa kawaida hana uwezo katika mapato yake kupata katika kiwango hicho cha fedha.

Kwa msingi huo Mhe. Spika, ni suala zima kwamba uchumi umemilikiwa na watu wachache katika sekta ya mahoteli na mabenki, hao ndio waliomiliki uchumi na katika mgao wa pato la taifa hawa ndio wanaonufaika zaidi kuliko wananchi wa kawaida. Kwa hivyo, ni wakati sasa wa serikali kutafuta mbinu mbadala za kuwawezesha wananchi mmoja mmoja, ili na yeye aweze kumiliki uchumi wake, ili katika mgao ule wa pato la taifa basi kinachozungumzwa katika *data* hizi kilingane na uhalisia.

La pili Mhe. Spika, tuna tatizo kwamba uchumi wetu hauko katika uzalishaji. Mara zote Mhe. Spika, tumekuwa tukizungumza katika Baraza hili. Leo ni aibu kwamba Zanzibar imegeuka kuwa ni soko tu, ukitafuta kitu tunachokizalisha na kukiuza katika masoko ya nje utakuta hakuna. Matokeo yake tunajikuta kwamba Zanzibar hatuna uwezo wa kuzalisha na kuuza katika masoko ya nje, tumebakia Zanzibar ni soko la kung'ang'aniwa na watu waliokuwa ni wazalishaji katika nchi za Afrika Mashariki na nchi za mbali. Hilo ni tatizo la pili linaloelemea uchumi wetu.

Tatizo la tatu Mhe. Spika, ni suala la sekta binafsi. Hakuna nchi yoyote iliyoendelea duniani iliyokuwa haina sekta binafsi iliyokuwa ni *powerful.* Leo Zanzibar sekta binafsi inachukuliwa kama ni mshindani wa serikali, haijapewa nafasi zake. Tunaposema kwamba sekta binafsi haina uhai, ni kusema kuwa ajira nazo zitaleta matatizo, kwa sababu sehemu kubwa ya ajira katika nchi yoyote huitegemea sekta binafsi. Vile vile sekta binafsi ndio inayokuwa na vianzo vingi vya mapato katika uchumi wa nchi.

Katika hotuba ya Mhe. Waziri imezungumza kwamba sasa kutakuwa na sera na nini. Kweli wafanye kadiri watakavyofanya, lakini bado tunasema sekta binafsi Zanzibar bado inahitaji kupewa nafasi yake maalum na isichukuliwe sekta binafsi kama ni mshindani mkubwa wa serikali. Tunapofanya hivi Mhe. Spika, tunafikia pahala kwa kweli uchumi wetu hauwezi ukaendelea.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza hayo kwa muhtasari sana mambo yanayohusiana na uchumi pamoja na changamoto zake. Mhe. Spika, sasa naomba uniruhusu angalau kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana.

Mhe. Spika, bajeti iliyopita ililenga kukusanya jumla ya bilioni 613, ambapo kwa mujibu wa ripoti ya Mhe Waziri katuambia kwamba utekelezaji wake hadi mwezi Juni ni kuweza kupata bilioni 463. Hiyo ikiwa itakuwa na upungufu wa asilimia 23 kwa mujibu wa ripoti. Lakini vile vile bajeti ya matumizi ya kawaida ilipangwa bilioni 234, ambapo hadi mwezi Juni serikali imetuhakikishia kwamba itakuwa na uwezo wa kutumia bilioni 228, hapa kidogo hali ni nzuri kwa sababu ni mambo ya serikali yanakwenda vizuri, hapa tutakuwa na upungufu wa asilimia 3. Lakini katika bajeti ya maendeleo katika fedha iliyotengwa bilioni 378, serikali hapa imejiwekea hadi kufika mwezi Juni kukusanya jumla ya bilioni 235 ikiwa ina upungufu wa asilimia takriban 38.

Mhe. Spika, huo ndio muhtasari wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana kuanzia Julai hadi mwezi Juni. Ni dhahiri kwa vyovyote vile picha inayojijenga hapa kwamba serikali haikuweza kulinganisha vile ambavyo ilikisia katika bajeti ya mwaka jana. Kwa msingi huo ni dhahiri kusema kuwa Mhe. Spika, tumeshindwa kufikia

malengo tuliyojiwekea katika bajeti. Kwa hivyo, ikiwa mpaka mwezi Juni fedha hazikutosha au hazikukamilisha na huku tunaambiwa kwamba kuna 5.9 bilioni ambazo zitakuwa- *carrying forward* katika bajeti hii.

Mhe. Spika, hoja yangu kwa nini fedha hizi hazikutumika katika kipindi cha bajeti kilichopita, fedha hizi zinatokea wapi maana yake unapoi-*carrying budget* mbele maana yake ni kusema matumizi yalikuwa ni kwa asilimia 100. Lakini leo huku fedha haikutosha na huku kuna fungu ambalo litaingizwa katika bajeti ya mwaka huu, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kulikuwa na sababu zipi, chakula akapewa jirani wakati watoto ndani ya nyumba hawajashiba.

Mhe. Spika, baada ya kufanya tathmini fupi sana katika utekelezaji wa bajeti iliyopita, naomba sasa nije katika bajeti hii tunayoizungumza sasa ya mwaka 2012/2013. Makisio yanatuonesha kwamba mara hii serikali imepanga kukusanya jumla ya bilioni 649, kazi za kawaida zitatumia bilioni 307 na makisio ya maendeleo ni bilioni 341.

Mhe. Spika, bado hoja inakuja kwamba ikiwa hatukuweza kufikia malengo ya mwaka jana, kwa nini serikali mwaka huu ikisie zaidi. Maana ndio ile aliyoisema Mhe. Subeit, mkongwe miujiza. 'Leo una chanja huliwezi wachukua jengine wajielemeza' mambo haya ni vipi. Kwa hivyo, hili ndio tatizo letu katika uandaaji wa bajeti.

Kwa hivyo, hoja yangu katika hili naomba Mhe. Waziri anieleze kwamba ikiwa hatukufikia malengo katika bajeti ya mwaka jana kwa nini mara hii tukakisia zaidi, kwa nini hakufikiria kwamba kile kile tulichokikisia mwaka jana tukakiweka kuwa ni kile kile tu, ili tukavuta soksi kama ambavyo tulifanya mwaka jana.

Lakini Mhe. Spika, bajeti ya shughuli za serikali na bajeti ya maendeleo inavyoonekana iko sawa. Mhe. Spika, hili haliko sahihi. Nasema inawezekana likawa sahihi kwa sababu hatuna uwezo, lakini kwa nchi iliyojikita kujielekeza katika maendeleo, inategemewa kwamba bajeti ya maendeleo fungu lake liwe ni kubwa zaidi kulikoni bajeti ya serikali. Sasa inavyoonekana kwamba bajeti ya maendeleo na bajeti ya shughuli za kawaida za serikali *almost* iko sawa. Mhe. Spika, nasema tena hili sio sahihi, kwa sababu angalau basi bajeti inayokusudiwa katika shughuli za kawaida za serikali, angalau iwe ni asilimia 40 kwa asilimia 60 katika bajeti ya maendeleo. Tunapofika pahala tukaweza kutengeneza bajeti yenye sura hiyo, hapo ndipo unapoweza kuona sasa nchi imejikita katika uwekezaji katika suala zima la maendeleo.

Mhe. Spika, hoja yangu ya tatu katika hapa naomba niulize. Kwa nini mara hii bajeti ya maendeleo ishuke. Maana yake ya mwaka jana hatukuweza kuifikia, lakini kwa nini mara hii bajeti ya serikali ishuke. Maana yake ikiwa kwa asilimia 100 mara hii ni asilimia 90 katika bajeti tuliyoifanya mwaka jana, inawezekana tukafika pahala tukasema kuwa inawezekana ni wahisani wamepunguza misaada yao. Kama ni hivyo, jawabu litakuwa rahisi au lakini kama itakuwa sababu sio hiyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelimishe tujuwe kwa nini badala ya kwenda mbele katika suala la kuwekeza katika maendeleo sisi tunarudi nyuma.

Mhe. Spika, baada ya kufanya tathmini fupi ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu, sasa niende kwenye sura halisi ambayo imeiona, sura halisi ya bajeti ya mwaka huu. Mhe. Spika, bajeti ya mwaka huu ni bajeti tegemezi, tunaendelea kuwa ni wategemezi na tunaendelea kuwa ni watu watembeza bakuli. Makusanyo hayakufikia kabisa au hayafikii makisio yaliyowekwa. Mathalani katika makisio ya 649, inaonekana kwamba serikali itakusanya 280 tu, katika 600 serikali huwenda ikakusanya bilioni 280 tu. Bilioni 333 ni misaada na mikopo kutoka nje, lakini ndio kama ninavyosema kwamba ni misaada pamoja na mikopo. Hili linakuwa ni tatizo zaidi, maana yake sasa tunakopa zaidi kwa ajili ya kufidia bajeti yetu. Ni sawa na kuwa pahala unadaiwa ukalipa kwa ajili ya kukopa, maana yake ukenda kukopa pahala pengine kisha ukenda ukalipa kule unakodaiwa, kwa hivyo bado hujafanya kitu tatizo ni lile lile tu ni kujidanganya wewe mwenyewe tu.

Kwa hivyo, na hii nakisi ya bilioni 29 Mhe. Spika, ujazo wake basi serikali itajaza nakisi hii kwa kukopa katika vyanzo vya ndani. Kwa hivyo, katika hali hii Mhe. Spika, inaonekana dhahiri kwamba bado tuna tatizo kubwa sana la utegemezi katika bajeti yetu. Kwa msingi huo tunahitaji kubadilisha mwelekeo, tunahitaji serikali ya awamu ya saba ikae iinamishe kichwa na ione ni namna gani tunaweza kuondoka hapa. Sio vizuri hata kidogo baada ya kupata utulivu. Tulikuwa Mhe. Spika, tunajisifia kwamba hakuna matatizo, wala fujo. Lakini leo hakuna sababu kwa nini serikali isiendelee kukuza uchumi, kwa sababu ile tunu ambayo tumeitafuta kwa muda mrefu ya amani, leo tunayo. Sasa ikiwa tunayo, kuna sababu zipi zinazopelekea uchumi usikuwe katika nchi yetu. Kwa hivyo, sura ya kwanza ya bajeti yetu hii inaonesha kwamba kuna utegemezi wa hali ya juu.

Lakini sura nyengine ya bajeti yetu inaonekana kwamba bajeti haikulenga kuanzisha vianzo vyengine vya mapato, Mhe. Spika, hili ni jambo la kusikitisha sana. Tulitegemea kwa vyovyote, kwa sababu tuna muelekeo

wa kujenga uchumi, kwa vyovyote vile bajeti ingelizungumzia namna gani serikali imejipanga katika kuanzisha vyanzo vipya vya uhakika vya mapato.

Kwa mfano, kilimo chetu kwanza hapa Zanzibar sisi ni bahari, serikali ituambie na mara nyingi sana tumekuwa tukilizungumza hili kwamba kilimo chetu sisi ni bahari, tumezungukwa na bahari, suala la uvuvi wa bahari kuu serikali imelipa mtazamo gani, ni kiasi gani cha fedha ambacho kimeekeza katika kuona kwamba tunaondokana na uvuvi huu tuliozowea na tunaingia sasa katika uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Spika, tuna suala zima la mafuta ambalo tulilizungumza katika baraza hili. Mafuta na gesi ni kitu cha kusikitisha sana kuona kuwa serikali haikuzungumza chochote katika bajeti hii, ni kitu cha aibu sana kuwa serikali haikuzungumza namna ambavyo tutajipanga katika kuitafuta na kuichimba rasilimali hii.

Mhe. Spika, wenzetu kule Tanzania Bara sasa hivi wanakwenda mbio sana katika suala zima la mafuta na gesi. Mimi katika hili naomba niseme kitu kimoja, kwamba hii kwa sasa ni rasilimali ya Muungano. Mhe. Waziri katika mengi ambayo atakuja kutueleza hapa, basi atuambie kwamba Zanzibar itajipatia kiasi gani, kwa sababu watu wanasema kwamba sisi tususie maana yake tusidai; aah, hizo ni hadithi za alinacha mimi sizitaki, nataka tulichonacho tukipate leo. Wenzetu kule wanapata pesa nzuri sana katika suala la mafuta na gesi, wameshaanza katika gesi.

Kwa hivyo, ikiwa ni suala la Muungano katika bajeti hii mbona mimi sijaona kifungu kwamba kuna kiasi ambacho kitakuja Zanzibar kama ni pato ambalo linatokana na gesi, inawezekana kwamba mimi sikufahamu kwa sababu hilo tabu kubwa sijalipitia, lakini Mhe. Waziri kwa sababu bajeti hii ni yake, atakapokuja hapa na katika mengi ambayo atakuja kutueleza ni serikali yetu katika bajeti ya mwaka huu tutapata kiasi gani kutokana na rasiliamali hii ambayo ni yetu pamoja.

Lakini Mhe. Spika, mbali ya suala la mafuta, kwa nini hatuzungumzi masuala ya viwanda. Hatuwezi tukaendelea, hatuwezi tukajenga uchumi kama hatuna viwanda. Hatuzungumzii viwanda vikubwa vya kuunda madege, magari na mameli hapana, tuko katika viwanda vya kati na kati, tuna uwezo navyo Mhe. Spika. Hii hadithi imefikia pahala gani. Basi angalau ndani ya kipindi cha miaka mitano au miaka mitatu hatuoni angalau viwanda vitatu au vinne vimesimama viwanda vya uhakika vya kuongeza mapato katika serikali. Ukiachia mbali vile viwanda tunavyoambiwa viwanda vya kutengeneza chapati au viwanda vya kutengeneza viatu vya makubadhi. Mhe. Spika, tunahitaji viwanda, serikali itupe jawabu katika hili, itakujakuwa ni aibu sana katika Serikali ya Awamu ya Saba kuondoka katika madaraka katika kipindi hiki kama angalau hatukuwa na viwanda japo vitatu au vinne, japo vile vile vya zamani vya viatu vya mwendo na sigara za mchujo, hatuna haja ya viwanda vingine Mhe. Spika, ni lazima tuvizungumzie vitu hivyo ndio ambavyo vinatuwezesha sisi kuuza nje na kujipatia fedha za kigeni, bajeti hii imezungumza nini katika hili.

Jambo la tatu Mhe. Spika, bajeti haikuangalia kuongeza kipato cha wananchi. Mhe. Spika, mwanzo nilisema kwamba tatizo kubwa la bajeti yetu uchumi umedhibitiwa na watu wachache tena wageni, wananchi waliowengi ni hohe hahe hawana uwezo wa aina hiyo. Kwa vyovyote vile mimi nilikuwa nina matumaini sana kuanzishwa kwa wizara ile ya uwezeshaji nikidhani kwamba serikali itaitumia wizara ile kuwawezesha wananchi, tulitazamia hivyo. Kuwawezesha wananchi maana yake ni kwamba unafika pahala wananchi unawaelimisha na walioelimika unawawezesha na kuwawezesha duniani kote utakakokwenda ni suala la kuwapatia mikopo, kote duniani wanafanya hivyo wananchi wao kuwapa mikopo. Leo tunazungumzia diaspora na vitu vyengine. Diaspora wote wale hupewa mikopo na serikali zao.

Kwa hivyo, hapa tulitazamia kwamba suala hili serikali katika bajeti hii italizungumza, tuachane mbali na ile mikopo ya AK na JK. Mhe. Spika, mikopo ya AK na JK ni usanii tu hakuna chochote kile, utasikia tu hapa kuna bilioni ngapi, ukizitafuta katika jimbo wilayani hakuna. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba suala hili Mhe. Waziri atueleze, ili mikopo iwe na nafuu na tija kwa wananchi, hao wananchi wanaoipata hiyo mikopo riba inawaumiza. Mhe. Spika, mabenki ya Uingereza kule huwakopesha watu wake kwa asilimia 11 tu. Leo hapa mabenki yetu huyo anayepewa mikopo huenda mpaka asilimia 21 au asilimia 20, huwasaidii, mtu mnyonge kumkopesha kwa asilimia 20 au 21 humsaidii. Mhe. Spika, Oman kule sasa hivi imefikia katika asilimia 8 kuwakopesha wananchi wake, unapomkopesha mwananchi katika kiwango hicho unamsaidia, kwa sababu kiwango hicho unaki-*afford* kuweza kulipa na wewe ukapata faida.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linaonekana katika bajeti hii kuna suala zima la serikali imepanga miradi na programu ambayo haina tija kwa wananchi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, dakika tano zimebakia.

**Mhe. Omar Ali Shehe: M**he. Spika, tutakuja kuzozana sana katika bajeti za mawizara. Hizi fedha zilizoainishwa kwamba zitakwenda kwenye sijui kujenga nyumba za ofisi. Mhe. Spika, nakumbuka tangu mimi niingie katika Baraza hili, Ikulu hizo zinajengwa na wala huzijui zinajengwa wapi. Ikulu hiyo Mhe. Spika, kila siku inaimarishiwa mawasiliano hujui mawasiliano ya aina gani.

Mhe. Spika, halikadhalika kuna miradi mingi katika mawizara ambayo inaingiziwa fedha ambayo huioni tija yake. Mfano, Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuna miradi mingi sana ya mabilioni ya fedha, unapoziulizia pesa hizi zinatumika wapi, utaambiwa maana yake hizi tunafanyia semina na hizi tunazifanyia safari, ni namna tu ya watu kugawana fedha zile. Mhe. Spika, hili halikubaliki.

Mwisho Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako naomba niingie kwenye mapungufu ya bajeti. Mhe. Waziri bajeti yako haikueleza namna ya uvujishaji wa mapato na vipi utadhibiti uvujishaji wa mapato. Mhe. Spika, kuna suala la ukusanyaji wa kodi, bado hatujawa na mfumo mzuri wa ukusanyaji kodi, vipi mbona bajeti yako haikuzungumza kitu, huwezi kuzungumzia uchumi na udhibiti wa mapato kama hujazungumzia namna gani utaimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Waziri katika bajeti yako hukuainisha namna utakavyozipa nguvu sheria zinazosimamia fedha katika nchi. Mhe. Spika, humu sikuona chochote.

Mhe. Spika, pungufu la pili ambalo ni kubwa la bajeti yako, bajeti haikuzungumzia chochote kuhusiana na misamaha ya kodi. Tuna tatizo kubwa sana misamaha ya kodi. Naomba niseme hivi, mwaka 2008/2009 jumla ya bilioni 22 zilisamehewa kama ni msamaha wa kodi. Mwaka 2009/2010 jumla ya bilioni 27 Mhe. Spika, zilisamehewa kupitia misamaha ya kodi. Mwaka 2011/2012 jumla ya bilioni 18 zilisamehewa. Mhe. Spika, hili mimi sikubaliani nalo. Kodi zinasamehewa kiholela, kunakuwa na mambo ya uholela holela, lakini zaidi hapa kuna kitu rushwa kinachotokea hapa. Hatuwezi leo tukawakamua wananchi na tukawasamehe watu wenye pesa zao wasitupe kodi. Naomba sana serikali itupe jawabu kamili juu ya namna ilivyojipanga. Sasa Baraza hili tuliangalie sana hili na ifike pahala kwa kweli tusikubali suala hili kumpa mtu huyo kwa sababu kunakuwa na mianya ya rushwa katika kusamehe kodi.

Mhe. Spika, bajeti haikuzungumzia suala la gesi na mafuta kama nilivyozungumza, lakini naomba nitangaze, kwa sababu serikali ilikuwa na nia ya kuleta mswada hapa, suala la kuunda shirika la mafuta na tulikubaliana katika Baraza lililopita, kwa kweli wenzetu wanakwenda mbele kupitia TBC.

Mhe. Spika, natangaza kwamba tukijaaliwa naandaa mswada binafsi kuunda Shirika la Mafuta katika Baraza la Wawakilishi. Ni matumaini yangu kwamba kwa kuwa serikali walikuwa na nia hiyo na wawakilishi walikuwa na nia hiyo, basi nitapata *support* kubwa ya kuupitisha mswada wa kuunda Shirika letu la Mafuta.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nakusudia kusema, mbona Muungano hukuuzungumza, tuna matatizo katika Muungano wetu. Muungano ndio unaodhoofisha uchumi wetu na katika Muungano kuna mambo mengi sana ambayo yanasababisha sisi tusiendelee. Kama alivyosema Mhe. Mohamed Said juzi kuzungumzia Afrika ya Mashariki namna Tanzania itakavyoingia katika uchumi wake, kwa vyovyote na wewe ungezungumzia vipi Wazanzibari tujitayarishe katika mchakato huu, katika yale mambo ambayo kwa kweli yanaleta udhia katika uchumi wetu.

Mimi napendekeza moja, suala la sarafu na benki ni lazima tukijaaliwa tuwe na sarafu yetu na ni lazima Zanzibar tuwe na benki yetu, kwa sababu kadiri tutakavyojinasua kiuchumi kama hatuna uwezo wa kuzi-*regulate policy* za fedha hatuna uwezo wa kufikia popote.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa kwa sababu ya muda wako, naomba niseme tu kwamba ili uchumi wetu ukuwe ni lazima tuwe na utawala bora na utawala bora ni lazima tufikie pahala tuwe na suala la uwajibikaji, hatuwezi kuwa tunapiga kelele katika Baraza hili. Baraza na kamati zako Mhe. Spika, tuibuwe mambo ya ubadhirifu, lakini mwisho wa siku tukaja tukamaliza, tutakuwa hatulitendei haki Baraza na hatuwatendei haki wananchi. Suala la utekelezaji wa ripoti ya kamati teule ambayo tayari imeshapitiwa na Baraza lako, naomba serikali ije na jawabu. Serikali ituambie vipi itatekeleza au lini itatekeleza mambo yaliomo katika ripoti ya kamati teule, ili na sisi tujenge imani

Kwa hivyo, suala la utekelezaji wa Ripoti ya Kamati Teule ambayo tayari imeshapitishwa na Baraza lako, basi naomba serikali ije na jawabu na kwamba serikali ituambie vipi na lini itatekeleza mambo yaliomo katika Ripoti ya Kamati Teule, ili na sisi tujenge imani pamoja na matumaini kwamba sasa tunaweza kuidhinisha fedha nyengine na watendaji wakatumie.

Mhe. Spika, kabla ya hapo, mimi nasubiri kauli ya serikali juu ya utekelezaji wa Ripoti ya Kamati Teule pamoja na mambo mengine, ili baadae niunge mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha na Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwanza nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa uwezo wako mkubwa katika kukiendesha Kikao hiki cha Bajeti. Pili nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta hotuba yake ya bajeti pamoja na watendaji wake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu kwenye kitabu hiki niende moja kwa moja kwenye masuala ya kuimarisha elimu. Kwa kweli elimu ni msingi wa maendeleo.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu kwa ajili ya kumsikiliza Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Spika, elimu ni kitu cha msingi kabisa. Kwa hivyo, nimeona kwenye kitabu hiki kwamba kumewekwa misingi au Mhe. Waziri alielezea kwa upana sana juu ya kuchangia katika suala hili la elimu kwa mwaka huu wa fedha. Mhe. Spika, ni kweli tunaona kwamba hapa Zanzibar tuna ukosefu wa wataalamu. Kwa maana hiyo, ni jambo la msingi kabisa Mhe. Waziri kutoa kipaumbele kwa masuala haya ya elimu.

Vile vile niende kwenye suala la kuimarisha ustawi wa wazee. Mhe. Spika, tunajua kwamba wazee ni watu muhimu katika nchi yetu hii, pia nimeona katika mwaka uliopita alitenga fedha, yaani alisema kwamba katika kipindi hiki cha bajeti atawatizama zaidi wazee na kwenye kitabu hiki amejitahidi kuwaelezea namna ya kuwasaidia wazee wetu.

Vile vile suala jengine ninaloliona kwenye bajeti hii ni ajira kwa vijana. Mhe. Spika, ni kweli ajira kwa vijana ni muhimu sana, kwa sababu tunawaona vijana wetu hawana ajira ambazo ni rasmi, na hali hiyo inapelekea watoto wetu hao kujiingiza katika mambo mbali mbali ambayo hayana faida kwao wao.

Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Waziri, lakini itakuwa tathmini hiyo si sahihi kwamba katika kila watu watano mtu mmoja hana kazi, yaani hiyo tathmini yake kidogo haiko sahihi, kwa sababu tunawaona vijana wetu ni wengi ambao hawana kazi na wanazurura.

Jambo jengine ambalo naliona Mhe. Waziri amelipa kipaumbele kwenye bajeti hii ni kuhusu ujenzi wa Skuli za Kisasa za Ghorofa. Kwa upande huu niseme skuli za ghorofa lakini zimezingatia kwamba sisi katika jamii zetu kuna makundi tofauti ya watu hasa hawa walemavu. Kwa hivyo, ni lazima Mhe. Spika katika ujenzi huu wa skuli hizi za ghorofa uzingatie makundi kama haya ya walemavu.

Kwa kweli hotuba ya Mhe. Waziri kwa kiasi fulani nzuri, na amejitahidi pamoja na wafanyakazi wake, lakini kuna mapungufu na hasa kwenye matatizo kuhusu masuala ya kodi pamoja na mambo mengine. Mhe. Spika, ukiongeza kodi katika mambo mbali mbali ni kwamba unawaongezea mzigo wananchi wako.

Kwa maana hiyo, lazima hizi kodi zitazamwe vizuri, ingawaje tunaambiwa kwamba kabla ya wewe hujataka nchi yako ikufanyie, lakini na wewe ujitizame kuwa nchi yako utaifanyia nini. Kwa hivyo, ni lazima kama tunataka maendeleo, basi kuna mambo ni vyema sisi wenyewe tujipinde na tuone kwamba kuna umuhimu wa kile tunachokitaka na sote tushirikiane kwa pamoja, ili tupate yale maendeleo tunayoyataka.

Mhe. Spika, kuhusu mambo ya kodi na kama walivyosema wenzangu wafanyabiashara kwamba wanalipa mara mbili na hili limekuwa ni tatizo kwa wafanyabiashara na hata kwa maendeleo ya nchi yetu. Kutokana na hali hiyo, labda niseme kwamba na wenzetu wanasema kuwa muungano unakuwa unapigiwa kelele sana, kwa kweli muungano ni kitu kizuri sana kwetu sisi na lazima tuwe pamoja, lakini hizi kero nadhani sasa tukae pamoja, ili tuone namna gani ya kuzitatua hizi kero, kwa sababu ikiwa kitu unakipenda, basi ni lazima ukitafutie njia, ili kiwe kinapendeza zaidi.

Kwa hivyo, haya yamekuwa ni matatizo na wala tusishikane mikono wakati wa kula, wakati sisi tunasema Zanzibar ni ndogo na tunao ndugu zetu wa damu, kwa hiyo tukifanya uchoyo, kwani nina hakina kwamba

tukifanya mambo yetu vizuri na tukaachiliwa muungano, yaani ukatupa nafasi ya kuamua mambo yetu mengi tu.

Kwa maana hiyo, itafika wakati tutashiba na wala hatutokimwaga kwa sababu ya ule utamaduni wetu Wazanzibari, basi tutawasaidia na wenzetu, pale tutakapofika kwamba sisi tumeshatosheka na maendeleo au maendeleo yameshafika kiasi fulani sisi hatutokuwa na haja ya kuvimwaga na tutawasaidia na wenzetu ambao ni ndugu zetu wa damu na lazima kwenye udugu muhurumiane.

Kwa hiyo, suala hili la mambo ya muungano, ni vyema kuyatatua sisi wenyewe tukikaa Viongozi Wakuu huko juu wayaone na hao watendaji, mimi nasema kwamba si serikali hasa isipokuwa ni watendaji ambao hawafanyi ule wajibu wao ambao unakusudiwa.

Mhe. Spika, ningependa kuwaomba wale viongozi au watendaji kwa sababu hizi kasoro zimeshakua, kwa sababu kero mwisho wake hugeuka ikawa balaa. Kwa mfano, tumeona nchi hivi sasa vijana wanaokua hivi sasa ambao ni tatizo kwa sababu wanapashana habari kutokana na hii mitandao ya kijamii na inakuwa ni kero kubwa. Hivyo, ni lazima turudi na tuone namna gani tutaondosha haya matatizo, ili lengo letu pamoja na madhumuni yetu ni kupata maendeleo ya nchi zetu hizi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika nimesoma vitabu vyote hivi kama vile nimesoma hiki cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na nimeona mambo ya kipaumbele ambayo yametiwa humu na ndiyo hayo ya kuimarisha vijana, ajira, wazee, elimu ya lazima ambapo ni lazima tuelimishane kuhusu masuala haya.

Vile vile kuna mambo ambayo ni lazima yatatukuta kwa sababu tumo kwenye ulimwengu wa kipamoja, basi lazima kuna mambo yatatukuta kutokana na mambo haya ya kilimwengu. Kwa mfano, kuna suala likitokea ulimwenguni kama vile kuna *crisis* yoyote, basi na sisi linatuhusu huku chini ingawaje sisi huku ni watu masikini na wala hauwakolezi wenzetu, yaani mataifa mengine, lakini sisi tukitizama na kulingana na bajeti zetu na yanapotokea mambo huko ulimwenguni na sisi yanatuhusu.

Kwa hivyo, ni lazima pia serikali itizame kutokana na hali hizi za mambo ya mfumko wa bei, yaani mambo mengi yanatokana na mabadiko ya huko ulimwenguni.

Mhe. Spika, pia kuna tatizo la mafuta kwamba tukisema kuwa tunapandisha kodi ya mafuta, kwa sababu ukipandisha kodi ya mafuta maana yake mafuta yatapanda bei na matokeo yake vitu vyote vinapanda bei. Kwa kweli ni jambo ambalo ni kero au tatizo la ulimwengu mzima, yaani ni matatizo ambayo yanatukumba ulimwengu mzima, vitu vikipanda bei na sisi kwa sababu ni sehemu ya ulimwengu basi ni lazima mambo kama haya yatatukumba na sisi.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema uiangalie serikali yetu kwa macho mawili, yale waliyoyakusudia kuyafanya basi tuwape nafasi, ili wayafanye kwa moyo wa kusaidia taifa letu.

Mhe. Spika, bila ya shaka kila mmoja anataka maendeleo ya nchi hii na kwa yale yaliyokuwa ni kero, basi serikali kama walivyosema wenzangu kuna mambo haya ya hoja zile maalum zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, kwamba kuna matatizo ambayo yalishughulikiwa hapa, basi angalau tungeyafanyia usahihisho na tukajua kuwa ile kazi tuliyoifanya ni kazi ambayo Baraza lilitutuma kufanya kazi hizo, ni vyema kuyaona yanafanyiwa kazi.

Kwa hayo machache Mhe. Spika niseme kwamba kwa upande wangu nimechangia kiasi hicho cha kuiona kwamba bajeti hii inayo mambo ambayo ni muhimu, na serikali imejitahidi na pia kuna mambo ambayo yatakuwa yenye kasoro kama walivyosema wenzangu, basi serikali ikae na iyazingatie pamoja na kuyafanyia masahihisho.

Mhe. Spika, kwa hayo machache niseme nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia ingawaje ni mambo ya bajeti na mengi kwenye vitabu hivi yanakuwa yanachanganya, yaani yanahitaji ukae kwa utulivu na utulivu wenyewe haupo, ukienda huko jimboni kuna mambo mengi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni lazima tukae tuyaone haya mambo ni yetu na sote ni watumishi wa watu huko majimboni kwetu, kwa maana hiyo ni lazima tuyachangie pamoja na kuyasimamia kwa nguvu zote. Kwa maana hiyo, niseme kwamba nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kusema machache mbele ya Baraza lako hili tukufu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, ahsante sana kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyenijaalia jioni hii kuwa katika hali ya uzima na afya njema na kuweza kusimama katika Chombo hiki cha Kutunga Sheria, ambapo tunajadili shughuli za nchi yetu.

Vile vile nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi Mhe. Spika kwa utulivu ulionao katika kutuongoza kwao, namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima na busara.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika uwasilishaji wake wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali. Kwa kweli Mhe. Waziri aliingia kwa mbwembe kwa ajili ya kuwasilisha kitu kizito kama hiki. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kojani, naomba na mimi nitoe machache katika kuchangia bajeti hii adhimu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu aniwezeshe niwe na niweze kuchangia vizuri.

Kwa kweli bajeti hii ukiiangalia kwa ndani kabisa, basi ni bado ni mzigo kwa wanachi wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika, bajeti hii haikuzingatia ugumu wa maisha katika mfumko wa vyakula na dawa za kibinadamu.

Kwa maana hiyo, bajeti nzuri ni ile inayowapa wananchi wake unafuu, kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi lazima tuwasemee wananchi wetu na hapa ndipo mahala pale na wala hatuna sehemu nyengine pa kuwasemea. Kwa hivyo, bajeti hii imejikita sana katika masuala ya kuboresha serikali, lakini wananchi wako chini sana, jambo ambalo halifurahishi kabisa.

Mhe. Spika, katika bajeti hii kuna ongezeko la kupanda kwa mafuta senti hamsini, ukilinganisha kwa kutamka ni ndogo, lakini mafuta yanapopanda bei, basi kila sehemu inapanda bei. Kwa mfano, kwenye usafiri kutakuwa na bei, vyakula na chanzo ni hii kupanda kwa mafuta.

Mhe. Spika, bajeti hii ingezingatia kwamba ingesimamia vizuri katika usimamizi wa mapato, hili lingekuwa jambo zuri sana, kwa sababu kama Mhe. Waziri alivyozungumza kwamba uchumi umekua kwa asilimia 7.6, lakini inasikitisha sana kwani hatuoni umekua kwa namna gani. Kwa maana hiyo, kama uchumi umekua basi ajira za wananchi zingeongezeka, pia masuala ya afya yangekuwa mazuri pamoja na masuala ya mfumko wa bei yangepungua.
Mhe. Spika, alizungumza hapa Mhe. Omar Ali Shehe, ili uchumi wetu ukue basi japo viwanda viwili vitatu tuwe navyo, kwa sababu tukiwa na viwanda vinasaidia wananchi wetu kupata ajira. Kutokana na hali hiyo, basi kama uchumi wetu umekua vile viwanda vyetu tulivyonavyo vidogo vidogo kama vingefufuliwa tungesema *Alhamdulillah* tumefikia malengo.

Haitoshi Mhe. Spika, kuhusu ushuru wa bandari umepanda tena kwa safari za Unguja na Pemba ni shilingi 1,000/= na kwa upande wa Unguja na Dar-es-Salaam shilingi 2,000/= na mzigo wetu huu umebebeshwa wananchi si mfanyabiashara wala mtu wa serikali haathiriki na chochote, isipokuwa mzigo wote huu umemwelemea mwananchi wetu.

Mhe. Spika, ongezeko la vyanzo vya mapato hivi kama tungesimamia vizuri, basi yangetosha kabisa kuliko kuongeza hivi. Kwa kweli mapato ya serikali yanavuja sana, kuna sehemu kadhaa yanavuja na hapa wenzangu wameainisha na vielelezo vyote vipo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunaiomba serikali hapa tunapozungumza basi isiwe tunazungumza tu na kuishia hapa, isipokuwa yale tunayoyapeleka yanayotokana na wananchi wetu pamoja na taifa letu la Zanzibar, basi yafanyiwe kazi vya kutosha.

Wakati tunapomkuta mtu ni mbadhirifu basi tusimuonee aibu na tumuwajibishe, na kufanya hivyo itakuwa fundisho kwa mtu mwengine yeyote, lakini tukimuachia kila siku kuendelea na mapato yetu kuvuja na wala hatuwezi kupata maendeleo hata siku moja.

Mhe. Spika, imetajwa Sekta Binafsi hapa na Uvuvi wa Bahari Kuu umetajwa hapa. Kwa hivyo, tunaomba hii isiwe ni msemo tu, kwa sababu hata bajeti ya mwaka jana ilizungumzia kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu, lakini mpaka bajeti hii inaelekea ukingoni hatujaona wavuvi wetu kupata hatua ya kunyanyuka, isipokuwa ni ukandamizaji mtupu wa kuwabana zaidi.

Kwa kweli hali hii hatutawasaidia chochote kwa kupanga mipango ya kuwabana wavuvi na nchi hii ya visiwa, badala yake tupange mipango ya kuwaboresha wavuvi na wafike Bahari Kuu, na samaki Zanzibar hii wamejaa, na tunayo Sera hii ya Utalii kwa Wote, kwa sababu watu wa hotelini wanahitaji sana samaki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Sekta Binafsi ya Uvuvi ni sekta ambayo imeajiri watu wengi sana, na ninawaomba mufanye tathmini kuona kwamba sekta hii imeajiri watu wengi sana na inatusaidia kweli pamoja na mapato kwenye serikali, kwa sababu wavuvi wanakata leseni na tunapata mapato.

Mhe. Spika, serikali ingefikiria kuondosha kodi za vyakula, ili tuwe na unafuu kwa kweli wananchi wetu wana matumaini makubwa na Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa, lakini inafika wakati wanapoteza hata malengo kwa sababu siku zinakwenda bado unafuu haupo na hili ni tatizo kubwa sana.

Nikiendelea na mchango wangu, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la Kero za Muungano, ambazo hazitatuki na wenzangu wamezizungumzia hapa na wala bajeti hii haikutaja. Kwa hivyo, sisi kama Wazanzibari tunaheshimu wenzetu wa Bara, lakini sisi kidogo tunakosa kuheshimiwa, kwa sababu gani niseme hivyo, kwani kero ikizidi kuzaa matatizo na matokeo yake ni ugomvi.

Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe ambaye alizungumza wakati wa asubuhi hapa Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali alisema hapa kwamba, tulijiunga na *OIC* na tukakemewa hapa na tuliona tumefanya kosa na tulirudi hapa, lakini kila siku kuna Kamati ya Kuzungumzia Kero za Muungano na wala hazipati ufumbuzi milele. Kutokana na hali hii nadhani mwisho tutafikia hatua mbaya na kuja kuwalaumu wananchi wetu na ikawa wamekata tamaa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba serikali suala hili lilizingatie kwa uyakinifu kabisa na wala lisidharauliwe kabisa kwani muda umefika na siku zinakwenda mbele, kwa sababu tunataka tujikite Wazanzibari, na sisi *Alhamdulillah* na tupo watu wachache tu hapa kiasi cha watu milioni 1.5, ikiwa rasilimali zetu tulizopewa na Mwenyezi Mungu tutazihifadhi vizuri, basi *Wallahi* hakuna mtu wa kuwa masikini hapa.

Mhe. Spika, sisi wenyewe tunajidharau na hatima yake tutakuwa masikini milele na kwa nini tusiwe huru, kwa sababu muungano huu tuliungana kwa nchi mbili zilizo huru, ndio maana kukawa na kitu muungano na wala mtu mmoja hawezi kuungana. Kwa maana hiyo, hivi sasa umefika wakati na sisi tupatiwe fursa ya kujiamulia mambo yetu yanayotuhusu, hivyo ni vyema kabisa.

Mhe. Spika, taarifa hii ya kujisifia kupanda kwa uchumi kwa asilimia 7.6 ni jambo la kujivunia, lakini kama nilivyoeleza mwanzo hapa haioneshi taswira nzuri kwa maandishi tu, isipokuwa tunataka kwa vitendo kwa sababu ikiwa kwa vitendo itakuwa tumefikia hatua kweli, lakini ikibakia kwenye maandishi hatuna lolote wala chochote tutakachokifanya.
Mhe. Spika, kwa mchango wangu huu mdogo naomba niishie hapo na ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Azza Wajalla* kwa kutujaalia neema zake zisizo na mwisho, ikiwemo neema ya uhai na uzima tukakutana tena kupokea bajeti ya pili ya Serikali ya Awamu ya Saba ambayo tumeanza kuijadili leo hii.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa maoni yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe, ambao ndio ninaowawakilisha hapa kuhusiana na bajeti hii.

Mhe. Spika, kabla ya kuingia kwa undani katika baadhi ya mambo ambayo ningependa kuyagusia, nataka nitumie fursa hii kwanza kumtanabahisha rafiki yangu Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha Bajeti ya Serikali, alituambia anawasilisha Hotuba hii ya Bajeti pamoja na vitabu ambavyo alituambia anataka virikodiwe pamoja katika *Hansard*, ambavyo vilikuwa ni kitabu cha kwanza, cha pili na hili buku kubwa la makisio.

Sasa Mhe. Spika, hii ndio miongozo yetu katika kupitisha bajeti, lakini nasikitika kusema kwamba watendaji wake Mhe. Waziri wamemuangusha, kwa sababu vitabu hivi vina matatizo makubwa ya nambari na hesabu kiasi ambacho ingelikuwa si heshima kwake na kusema kwamba tuvikatae na akatuchapishie vitabu vipya na kuja kupitisha bajeti hapa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, ili nifahamike naomba nitoe mifano michache. Kwanza ukitizama vitabu hivi viwili, yaani kitabu hiki cha bajeti na hiki cha kwanza vina-*contradiction* ya nambari kubwa sana. Kwa mfano, michango ya washirika wa maendeleo ukiangalia ukurasa wa 18 wa kitabu cha bajeti unazungumzia, Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kitabu cha bajeti 2012/13 ukurasa wa 18 unaeleza hivi:-

> "Mhe. Spika, hadi Machi, 2012 jumla ya shilingi 199.0 bilioni sawa na asilimia 53.6 ya matarajio ya mwaka zilipatikana, zikiwemo shilingi 24.1 bilioni za Misaada ya Kibajeti sawa na asilimia 79.7. Aidha jumla ya shilingi 174.9 bilioni zilipatikana kupitia programu na miradi mbali mbali ikiwa ni sawa na asilimia 51.3 ya matarajio".

Lakini Mhe. Spika, ukilinganisha hiyo na kitabu hiki cha Mapitio kwenye ukurasa wake wa 43 kuhusu mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kitabu cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2011/2012 ukurasa wa 43 unaeleza hivi:-

> "Katika mwaka wa fedha 2012/2012 ndivyo walivyoandika wao Serikali ya Mapinduzi imepokea Misaada ya Kibajeti (4.5%) yenye thamani ya shilingi 24.0 bilioni hadi Machi, ambao mwanzo ndio walitumia pia, ambazo ni sawa na asilimia 79 ya makadirio ya mwaka wa fedha 2011/2012 ya shilingi 30.3 bilioni. Aidha Ruzuku na Mikopo iliyopokelewa kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo imefikia 170 bilioni sawa na asilimia 50.06 ya matarajio ya mwaka ya shilingi 340.95 bilioni".

Mhe. Spika, kuna mapungufu kule kuna asilimia 53 na hapa 50. Sasa Mhe. Spika, katika hesabu za serikali milioni 1, 2, 3 mpaka 5 si fedha kidogo kwa wananchi masikini wa Zanzibar. Kwa hivyo, tunapata wasi wasi kwamba kipimo kinafanywa kwa miezi ile tisa kutoka Juni hadi Machi, kwa nini vitabu vinakuwa na *contradiction* na watayarishaji wa vitabu hivi ni sehemu moja ni Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa sababu ya kuokoa muda naomba nisisome nyengine lakini naomba vile vile mtu alinganishe ukurasa wa 25 wa Bajeti na ukurasa wa 47 kitabu hichi cha kwanza. Vile vile alinganishe matumizi ya serikali ukurasa wa 21 kitabu cha Bajeti, na kilivyoandikwa ukurasa wa 44 wa kitabu cha kwanza kinachozungumzia mapitio ya hali ya uchumi.

Mhe. Spika, si hali nzuri chombo kikubwa kama hichi kuletewa mambo ambayo Wizara ya Fedha haikuwa makini kabisa, inatuletea hesabu ambazo zinapingana katika vitabu vyake vyenyewe vinavyokuwa vinawasilishwa juu ya meza.

Lakini kama hilo halitoshi Mhe. Spika, kama nilivyosema naokoa muda, lakini ningelivisoma vingi sana hapa. Hivi ndio tunavyovipitishia bajeti sisi, kitabu hiki Mheshimiwa kina matatizo makubwa sana. Kwa wenzetu Bungeni kuna utaratibu kwamba huwa kinatolewa kitabu hichi ambacho ni *draft estimates* halafu baada ya kupitiwa na Kamati kinapofanyiwa marekebisho na kamati vinatolewa vitabu vipya, kwa hivyo zinakuwa vitabu vitatu, kuna cha mashirika mbali, cha *local Government* mbali na cha Serikali Kuu mbali. Sisi tuna kimoja tu hapa lakini hata hichi kinakuwa kinajaa makosa.

Mhe. Spika, ili nifahamike nukta yangu naomba niseme kwa ufupi tu. Ukiangalia fungu la matumizi, ukenda kwenye fungu la matumizi kimafungu na fungu la matumizi kikasma, kuna sera thamani tofauti zilizoombwa Baraza hili kupitisha, tofauti na yaliyokuwemo katika hotuba ya Waziri. Naomba niseme Mheshimiwa ukiangalia ukurasa wa 58 wa kitabu hichi kikubwa ambacho pana muhtasari wa makadirio ya matumizi kimafungu. Sera iliyooneshwa jumla pale chini ni shilingi mia tatu na mbili bilioni mia nane na tano milioni, mia sita na sabini elfu (302,805,670,000).

Lakini ukifungua ukurasa 60, ambapo sasa kuna jumla ya Muhtasari wa Makadirio ya matumizi kikasma, kuna shilingi mia tatu na tano bilioni, thalathini na nne milioni, mia sita na sabini (305,034,670,000), huku kuna mia tatu na mbili, huku kuna mia tatu na tano. Najiuliza sasa Wizara ya Fedha hapa inatufanyia nini Mhe. Spika.

Isitoshe ukenda katika fungu la Wizara ya Fedha ambao hawa ndio wakusanyaji wakubwa wa mapato, ukenda katika ukurasa wa 23 matumizi takriban yote makubwa ya serikali yamewekwa chini ya Wizara hii.

Mhe. Spika, katika kitabu hichi kikubwa ukurasa wa 22 ambayo ni *consistency* na maeneo mengine inasema Wizara hii inakadiria kukusanya shilingi mia tatu hamsini na sita bilioni, mia mbili na hamsini na moja milioni (Sh 356,251,000,000). Lakini ukija ukurasa wa 23 kwenye mafungu kuna ziro mwanzo mpaka mwisho. Sasa

najiuliza Wizara ya Fedha haikusanyi kitu. Bahati mbaya hatujaletewa marekebisho mara hii tulivyokuwa tumezowea kupewa. Sasa nasema hakujakuwa na umakini kabisa katika kuandaa kitabu hiki.

Vile vile Mhe. Spika, nataka kueleza *concern* yangu kwamba Baraza lako hili linakuwa linajaribu kuburuzwa na hili sio jambo sahihi. Kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika? Baraza hili ndilo linalowawakilisha wananchi, linalopitisha matumizi kwa niaba ya wananchi ambao wanalipa kodi. Lakini kuna ujanja tunafanyiwa humu ndani. Ukilitizama hili ukenda katika fungu la mapato ukurasa wa 5-9, utakuta hakujawekwa ile nambari ya fungu moja kwa moja tu, kuna nambari ya fungu halafu kuna na fungu dogo ya kila kifungu ambacho kimetajwa hapa cha mapato. Kwa hivyo unapotaka kuja ku- *trace* mapato, unayaona sawa sawa, lakini njoo katika muhtasari wa matumizi kikasma, katika ukurasa wa 59.

Mhe. Spika, ukiliangalia buku hili ukurasa wa 59 muhtasari wa makadirio ya matumizi ambayo kawaida yawe mengi kuliko mapato, utakuta yapo katika ukurasa mmoja tu na kidogo yamemalizia ukurasa wa pili. Kilichofanyika ni kwamba tumewekewa fungu la jumla jumla la kila fungu. Najua ndani ipo wizara moja moja wapo, lakini hapa katika muhtasari ilitakiwa tuoneshwe. Kwa mfano tujue fungu la posho maalum wote walipata kiasi gani katika bajeti nzima. Fungu la posho za vikao ni shilingi ngapi katika mwaka mzima, posho la viburudishaji. Yapo kwa jumla lakini zile *break down* ambazo huku kwenye mapato tumeingiziwa vizuri, kwenye matumizi hazipo vizuri Mhe. Spika. Sasa hii haitendi haki kwa wawakilishi wa wananchi ambao wanakuja kupitisha bajeti hapa. Inatupa wasi wasi kwamba hapa ndio tunavungwavungwa panapo michezo ya watu.

Hii inanileta katika sehemu ya pili katika mchango wangu na kutaka kuzungumzia kidogo kuhusu muelekeo wa bejeti yetu. Mimi binafsi napata wasi wasi mkubwa sana na fungu hili la bajeti ya kawaida. Mhe. Omar hapa alipokuwa akitoa mchango wake kasema kwamba hafurahishwi na ile hali ya kwamba bajeti ya maendeleo takriban zinalingana na bajeti ya kawaida. Mimi naamini hali haingekuwa hivyo ingekuwa tuko makini katika kuchunga matumizi. Namuomba sana Mhe. Waziri, simlaumu yeye lakini hapa ndio anayewajibika kwetu ndani ya Baraza la Wawakilishi. Awatizame sana watendaji wake na watendaji wa wizara nyengine kwa ujumla Mhe. Spika. Ayaangalie sana maeneo yafuatayo:-

- Katika bajeti ya *stationery* katika matumizi ya kazi za kawaida.

- Atizame sana katika posho za safari za nje na za ndani.

- Atizame sana katika posho maalum. Tunashangaa tunaambiwa mishahara ime – *consolidate*, hili posho maalum linatokea wapi tena. Watu wana mishahara yao wanaingiziwa kila kitu na bado wana posho maalum kwenye Idara na Wizara wanatumia wanavyotaka.

- Atizame sana katika posho la vikao.

- Aangalie sana kwenye mafuta, vilainisho na vipuri vya magari.

- Aangalie sana viburudishaji, kuna mafungu yanatisha. Tunapokuja katika Wizara moja moja hatutawaachia Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nasema kuna haja ya kutizama sana bajeti yetu ya *recurrent*, kwamba hizi fedha tunazoziweka si fedha halisi, kuna fedha nyingi zinapotea mbali ya zile ambazo zimetajwa hapa katika fedha za misamaha ya kodi na mambo mengine. Jengine katika muelekeo wa bajeti ambalo halifurahishi, ni kwamba bado tuna bajeti tegemezi mno kama alivyosema Mhe. Omar. Ukiangalia utaona kwamba bajeti yetu vyanzo vya ndani havitoshelezi hata kukidhi bajeti yetu ya kawaida. Hiyo maana yake ni kwamba bajeti yetu hata ya mishahara na kuendeshea serikali nayo inategemea ifidiwe na sehemu ya bajeti inayotoka kwa washirika wa maendeleo.

Mhe. Spika, *summary* hii inaonesha kwamba vyanzo vya ndani vitatupa 294.1 bilioni. Lakini bajeti yote ya *recurrent* ya shughuli za kawaida ni 307.8 bilioni, pana nakisi kubwa tu hapa. Mimi siamini kwamba tungepaswa kutegemea bajeti ya wahisani, tungekuwa tunaichunga vizuri bajeti ya *recurrent* na kwenye mapato mimi naamini tungeweza kutafuta dawa ya tatizo hili.

Mhe. Spika, jengine ambalo linanipa mashaka ni kwamba kuna maeneo hayaonekani mapato yake katika bajeti hii. Nataka nitoe mfano *specific* nayo ni Mamlaka ya Usafiri Baharini kuna 00000. Ukinambia kwamba ni mamlaka inayojitegemea, zipo mamlaka nyingi humu zinazojitegemea na mapato yake tumeoneshwa humu. Hii

najiuliza halina mchango wowote serikalini, hayo mapato yake yanakwenda wapi? Tunajua kuna mapato mengi yanaingia pale. Vile vile kwa mfano pia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, kulikuwa kuna mapato humu ilipokuwa Idara ya Anga inaonesha, nimeyatafuta buku zima hili nimeshindwa. Mhe. Waziri labda leo utanisaidia utanionesha Mapato ya Mamlaka yako wapi? Na kuna mapato mengi tu pale hayaonekani. Kuna maeneo bado tunajiuliza mchango wake katika serikali iko wapi.

Vile vile katika matumizi kuna miradi mingi Mhe. Spika, ambayo nitakuja kuyahoji ikifika katika wizara yake inatupa mashaka. Mwaka jana nilionesha mashaka makubwa sana na mradi huu wa E-*Government*. Moja katika *concern* yetu kubwa katika bajeti hii ni kuongezeka kwa deni la taifa. Niliwahi kutahadharisha nilipokuwa nikichangia katika ripoti za kamati kikao cha mwezi wa Machi/Aprili kwamba, haya madeni tunayokopa kwa wingi kugharamia miradi mikubwa, kweli tunajiridhisha kwamba fedha zinazotajwa pale ndio fedha halisi zinazotakikana katika mradi ule. Nikasema tuwe na tahadhari sana na Wachina, tunawapenda sana, rafiki zetu tangu 1964 mpaka leo. Lakini ulimwengu wa leo kila mmoja anavutia kwake, huu ni ulimwengu wa biashara huu. Kuna mambo mengi tutakuja kuyataja tutakapofika katika bajeti ya wizara husika. Utakapokuja kukaa Mhe. Spika, itakubidi uweke *Ambulance* nje hapo wengine tutawatoa kwa *Ambulance* hapa, kuna matatizo makubwa sana.

Mhe. Spika, Kamati yetu sisi iliomba *break down* ya mradi wa *E- Government,* mpaka leo hatukupewa. Kunafichwa nini hapo? Mimi mwaka jana nilieleza *concern* yangu kwamba tukiutizama mradi huu unatutia mashaka kama kweli kiwango kilichotajwa pale takriban 18 milioni dola, kweli fedha ile inahitajika kwa *E-Government*, kuna nini hapa? Kwa hivyo nasema kuna mambo ya mapato hayaonekani, lakini kuna matumizi nayo vile vile yanatia mashaka makubwa nadhani waziri anapaswa ayatizame sana.

Mhe. Spika, jengine kwa ufupi naomba nigusie, nasema kwamba bajeti zetu zina matatizo zimegeuka ni *balance sheet*, bajeti zetu bado hazina *vision*, miaka nenda miaka rudi imekuwa bajeti yetu tunapata kiasi hichi, tutakuwa na nakisi hii, tutakitafuta vipi, kutakopa vipi, tunatumia na hadithi imekwisha. Lakini bajeti kama taswira ya dira ya nchi katika maendeleo, haionekani Mhe. Spika. Katika hili mimi napata mashaka kama tutafika katika suala hili. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu muelekeo wa bajeti zetu umekuwa sasa unakwenda kwa *ceiling*, inajulikana mapato inakuwa ni kiasi gani, kila wizara inapewa *ceiling* yake. Kakae upange *priority* yako.

Mhe. Spika, katika hali kama hiyo ile *role* ya Tume ya Mipango iko wapi? Kwa sababu tulitegemea kama *priority* za mwaka huu katika Wizara zote zilenge katika kukuza kitu fulani basi kuwe na uwiano, kuwa na uratibu katika masuala haya. Lakini anapokuwa kila mmoja anapewa fungu lake, halafu akaambiwa akakae ahesabiwe *priority* zake, najiuliza kweli katika hali kama hiyo kweli tutajenga uchumi wa nchi ambao utafika kuzalisha mapato ya kawaida katika nchi na kuwafikia wananchi kama walivyosema wengine. Mimi napata mashaka makubwa sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nahitaji Mhe. Waziri aje atusaidie, karibuni atatuletea Mswada hapa, tukaiunda upya Tume ya Mipango, tumeipa idara chungu nzima, tulitegemea tuanze kuona muelekeo wake. Hizi bajeti zionekane kama kweli ni *reflection* ya mipango ya nchi. Tunaambiwa tuna dira ya 2020, imezaa MKUZA, kuna CLUSTER tatu, kuna mambo chungu nzima. Nilikuwa nategemea kwamba hayo yaonekane yanatafsirika. Ndio maana matokeo yake kila mwaka tunaahidi mambo chungu nzima halafu hatuyaoni hapa.

Mwaka jana tulipewa matumaini makubwa hapa. Kwa uchumi tulikuwa tunategemea ndio iwe muelekeo, lakini kwa sababu hakuna pale panaporatibiwa mipango yote inapotea. Mwaka jana hapa tuliahidiwa na viongozi waliporudi safari kwamba tutaliona Shirika la Meli la Zanzibar, unakatika mwaka na hata dalili hauna na hautajwi tena mradi ule. Tuliambiwa kwamba kuna muwekezaji wa nje, keshaonesha muelekeo, ataingia katika mazungumzo na serikali hajaonekana tena. Kulitajwa hapa kuna mradi mkubwa wa Uvuvi wa Bahari Kuu, tukaambiwa kuna Kampuni inakuja hapa ya TAWASUL na itawekeza, tutaanza kupata ajira hapa takriban 4,000 lakini matokeo yake hakuna kitu. Kuna mambo mengi tunatajiwa lakini nadhani kuna upungufu katika pahala ambapo panaratibu masuala haya na kuweka muelekeo wa bajeti ya nchi.

Mhe. Spika, yako mengi, tutaingia katika wizara naomba haya niachie hapa. Lakini haya nahitaji kupewa maelezo kwa nini bajeti zetu bado zinakosa muelekeo ule wa kuwa na *vision* ya nchi.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo linatuathiri sana katika uchumi wa nchi yetu. Hili mimi silionei haya wala aibu ni suala la muungano huu ambao hauna haki baina ya Tanganyika na Zanzibar. Tungelikuwa tuna udhibiti wa uchumi wetu kwa sawa sawa, leo Waziri wa Fedha asingehangaika kutuletea marekebisho hapa ya kodi katika kuwatoza wananchi wetu, kuwaongezea gharama ya usafiri baina ya Unguja na Pemba ambayo ndani ya

nchi yetu. Maana kutoka Unguja na Pemba ni kama kutoka Mjini kwenda Makunduchi na kwenda Nungwi, tupo ndani ya Zanzibar. Lakini leo tunaongeza kodi kwa sababu tuna nakisi ya bajeti. Tunawaongezea wananchi wetu mzigo wa kodi kutoka hapa kwenda Dar-es-Salaam kwa sababu tuna nakisi ya bajeti.

Mhe. Spika, tunaongeza kodi katika mafuta hata kama ni shilingi 50, tayari hiyo itazaa mfumko wa bei mkubwa sana katika nchi yetu katika uzalishaji na kila eneo. Haya Mhe. Spika, yasingewapata wananchi wetu ingelikuwa tunasimamia kudai haki zetu, hata muungano huu usiokuwa wa haki kwa Zanzibar. Hili na tuonekane wabaya sana lakini tutalisema mpaka mwisho wa tone la damu yetu.

Naomba Mhe. Spika, niongeze dakika chake katika hili nilifafanue kwa kina kwa sababu hili ni suala muhimu sana kwa Wazanzibari. Bajeti yetu itaendelea kuwa bajeti, tutadanganyana tu hapa. Kwa sababu niliwahi kusema na Waziri wa Fedha namshukuru aliwahi kukiri juu ya kiriri kile pale. Kwamba Waziri wetu wa Fedha Zanzibar ni Waziri pekee duniani wa Fedha aliyekuwa hamiliki uchumi wake. Utakuwaje Waziri wa Fedha wakati huna udhibiti wa sera za uchumi, fedha na sarafu ya nchi yako. Wala sio tatizo kuwa na taasisi moja mkawa mna *share*.

Mhe. Spika, huko nyuma ilikuwepo Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki kabla haijaja BOT. Lakini nchi zote wanachama zilikuwa zina kauli sawa sawa. Leo tunaambiwa tuna BOT lakini sio ya Muungano ambayo inaratibu sera hizi. TRA mimi nasema sio ya Muungano inayodhibiti sera za kodi. Tutizame mjengeko wake, tutizame muundo wake, tutizame waliokuwemo ndani katika Bodi za Wakurugenzi, Wazanzibari wangapi na vyombo hivi visitizame ukubwa wa nchi, hizi ni nchi mbili sawa sawa mbele ya sheria za kimataifa. Zilipaswa ziwe na idadi sawa, lakini sio hivyo Mhe. Spika. Kwa hivyo hawajatutendea haki.

Matokeo yake wanasema kwa jeuri kabisa katika Baraza hili hili tumegaiwa kitabu hichi hapa kwamba kinasema. Katika kuadhimisha miaka 50 ya uhuru wa Tanganyika Benki Kuu inatoa ripoti ya miaka 50 ya shughuli za Benki Kuu. Mimi Mhe. Spika, najiuliza 1961 – 2011 wakati Benki Kuu imeundwa mwaka 1966 wakati tayari kuna Muungano Benki Kuu lini imekuwa ya Tanganyika hata itoe ripoti kwamba inaadhimisha miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika. Hivyo tunataka tudanganyane kwamba ikifika miaka 50 ya Mapinduzi tutatolewa ripoti ya Benki Kuu ya kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi hapa. Hata siku moja hawafanyi Mhe. Spika.

Lakini hili ndio tunaoneshwa mwenye Muungano huu nani? Ni Tanganyika Mhe. Spika, sisi ni wageni waalikwa. Hili Mhe. Spika, alilisema Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Pius Msekwa wakati alipokuwa Spika mwaka 1994. Aliandika *paper* yake maarufu akasema Zanzibar katika Muungano huu ni Mgeni Mualikwa. Semina ilifanyika Tanga na sasa leo haya tunayaona.

Mhe. Spika, tunahangaika kwa sababu hatupati haki zetu ndio maana tunawakamua wananchi wetu kwa kodi hizi zilizokuwa hazina sababu. Leo sisi tunatumia sarafu shilingi ya Tanzania. Tunasema kwamba inatuathiri katika mfumko wa bei kutokana na kuendelea kuporomoka. Mimi namuomba Waziri wa Fedha akija aje anisaidie, hivi sababu zinazopelekea kuporomoka kwa thamani ya shilingi ni za uchumi za Zanzibar au ni za uchumi wa Tanganyika? Sasa mpaka lini sisi tutaendelea kuumia kwa sababu ya mapungufu ya uchumi wa ndugu zetu?

Mhe. Spika, nawaomba Wazanzibari wakati ukifika wafanye maamuzi magumu ikija tume ya Katiba hapa. Wakati umefika tuwe na Benki Kuu ya Zanzibar na tuwe na sarafu ya Zanzibar na inawezekana kabisa tusidanganyane. Juzi Mhe. Spika, ulinipeleka Sychelles pale nikenda nikafanya kazi ya Baraza. Nimefika pale uchumi wa watu thamanini na saba elfu (87,000) nachenjisha dola 100 pale naambiwa *rate* ya rupia ya Sychells ni rupia 12 kwa dola moja. Leo hapa dola moja ni Shs 1,600/= kwa sababu ya uchumi wa Tanganyika tunaathirika hapa, kwa nini tuendelee kuwa hivyo.

Mhe. Spika, sio hilo tu kuna mapato yetu katika BOT, namuomba Mhe. Spika, akija aje atusaidie hapa. Kuna kipindi kirefu tumepata matatizo ya *balance of payment* ikawa IMF inatupa *balance of payment support.* Nina hakika kwa vile alikuwa Naibu Waziri wa Fedha wa Muungano anayajua hayo. Tulikuwa tuna fungu mpaka katika mwaka 1999 wakati ule Wawakilishi wetu katika BOT, walileta hoja hapa kwamba Zanzibar ikifanya hesabu ilikuwa inadai takriban bilioni 18, tuambiwe Mhe. Spika, fedha zile tulizipata na kama hatukuzipata kwa nini tusizidai.

Mhe. Spika, hata katika bajeti hii tunaambiwa gawio letu katika BOT ni bilioni moja, hivi ni haki kwa Mshirika wa Benki Kuu ambaye alitoa asilimia 11.02 ya hisa kuendesha Benki Kuu, mpaka lini tataendelea kunyanyaswa Mhe. Spika. Lakini namuomba akija Mhe. Waziri anisaidie. Naambiwa kuna Benki hii ambayo inaitwa *Afrexim*

ambayo Makao Makuu yake yapo Cairo, na Zanzibar ni mwana hisa kupitia PBZ, iliwekeza mbali ya kwamba ni Mshirika wa Muungano. Lakini tunaambiwa katika vikao tunakwenda pale mwenye vote ni BOT. Tunataka kujua Zanzibar inanufaika nini katika *Afrexim* katika *share* alizoziweka na tulikuwa tunapata faida gani kutokana kuwa hisa hizo.

Vile vile katika mfumo wa Muungano pasiwe tunawatolesha wananchi wetu kodi nyingi. Lakini tumepekuwa vitabu vyote hivi najiuliza liko wapi gawio letu kutoka kwa TCRA ambayo ipo chini ya Wizara ya Mawasiliano. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inakusanya fedha chini sana kutokana na Kampuni za Simu. Leo moja katika sekta kubwa ambayo inachangia bajeti ya Muungano ni Mapato yanayotokana na sekta ya Mawasiliano ya Simu. Tunapaswa tudai haki yetu sisi, hatuoni kitu.

Mwaka jana nilimuuliza Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu hapa, hana jawabu na mwaka huu hamna kitu katika bajeti yetu. Kwa nini tunaendelea kunyanyaswa mpaka leo katika mfumo wa Muungano huu hatunyamazi kimya Mhe. Spika. Hatunyamazi.

Mwaka jana nilionesha Uvuvi wa Bahari Kuu kwamba gawio tulilopewa hapa ukilinganisha na gawio liliripotiwa katika Bunge kule kuna tatizo katika kugawana asilimia 40 ambayo tuliyoambiwa sisi ni haki yetu. Twende tukalitizame vizuri, serikali isiridhike na habari tunazopewa tu na wenzatu, ikajiridhishe mapato yale hasa yapo vipi.

Mhe. Spika, nipo katika mapato yanayotokana na visa. Hapa nikiangalia ukurasa wa 7 buku hili kubwa linaloonesha mapato ya visa ni kama bilioni 3.598. Lakini tunajua kuna visa nyingi zinatolewa kwa watalii wanakuja Zanzibar wageni wanalipa katika Ofisi za Kibalozi nje kule, haziingii Zanzibar zinaingia katika hazina ya Tanganyika. Mimi nasema Tanganyika maana mfuko wa pamoja haujaundwa mpaka leo kwa mujibu wa ukurasa wa 132 na 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, pesa zinaingia kwao sisi hatupati kitu.

Mhe. Spika, hapa zimetajwa Kodi ya Mapato ya Wafanyakazi wa Muungano ambao wanafanya kazi Zanzibar, wanatumia huduma zetu. Tunawaendeshea huduma zao kutokana na kodi zetu sisi wananchi wanyonge wa Zanzibar. Wao kodi zao zinaruka zinakwenda upande wa pili, mwaka jana tuliambiwa sheria ilikuwa haijarekebishwa kwa hivyo hatukuweza kuzipata bilioni 15, mwaka huu tunakisiwa bilioni 18. Lakini kuna matumaini tu, tunaishi kwa matumaini tumekuwa kama vile wagonjwa wa ukimwi. Kwamba mwaka huu itarekebishwa sheria tuzipate, lakini hatuna uhakika. Lakini Mh. Rashid kauliza pale kwamba je, tukishazipata zile za mwaka jana tutazipata bilioni 15 tunazowadai. Kwa sababu hawa watu miaka yote walikuwa wakitumia huduma zetu hapa.

Mhe. Spika, naomba nimalizie katika nakisi. Vile vile kunaonekana kuna tatizo la fedha zinazotokana na washirika wa maendeleo. Mimi naamini kwamba tunaweza kupata zaidi ya hizi ingelikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, kalifanyia kazi wazo ambalo nimelitoa katika vikao hivi si mara moja wala si mara mbili wala si mara tatu. Mwaka jana pia aliniahidi kwamba atalifanyia kazi na kwamba mwezi wa Oktoba ingeanza mwaka jana mpaka leo halijafanyika. Nilipendekeza kwamba ukizungumza na Washirika wa Maendeleo wako tayari kuanzisha *consulative group meeting* ya Zanzibar peke yake. Ili misaada inayotokana na kuisaidia sekta mbali mbali tuwe tunakwenda kuomba wenyewe pale. Mhe. Waziri aliniahidi wakati ule kwamba mwezi wa Oktoba ingeanza mwaka jana mkutano wa mwanzo, mpaka leo hatujasikia kitu. Naomba unisaidie nani kakwamisha? kama ni uzembe wetu tuambiwe kama ni ndugu zetu wa damu pia tuambiwe.

Mhe. Spika, haya niliyoyataja ni mambo mengi. Mimi naamini haya yakifanyiwa kazi yanatupa vyanzo vya kutosha vya mapato hatuhitaji kuendelea kuwakamua wananchi wetu masikini. Naiomba serikali ya awamu ya saba, namuomba sana Rais wetu mpenzi Dokta Ali Mohammed Shein nawaomba makamo wake wawili, nawaomba Mawaziri wa serikali hii Mhe. Spika, wasijikunyate. Watoke kifua mbele wasimamie haki za Zanzibar. Kama wanataka himaya, himaya ni ngome ya wananchi Baraza la Wawakilishi lao liko hili.

Mhe. Spika, awamu ya sita ilifanikiwa pakubwa na imeondoka na heshima kubwa sana, kwa sababu ililitumia vyema Baraza la Wawakilishi kama ni ngome ya Wananchi kusimamia maslahi ya Zanzibar. Naomba sana Mhe. Spika, Rais, Mawaziri, Makamo wa Pili humu ndani, tunaonekana tunawakilisha kisawasawa maslahi ya Zanzibar.

Mimi naamini tukifanya hivyo wananchi watakuwa na sisi, na katika hilo niwaombe wananchi vile vile kwamba hizi ni haki zetu. Nataka niwahakikishie viongozi wao tupo makini, wawakilishi wao tupo makini tutazisimamia. Niwaombe katika hili wasikubali kutumika kufanya vitendo vya vurugu, fujo na kutumia maneno ya matusi katika kuzidai haki hizi. Hivyo Mhe. Spika, inaweza kutudharaulisha na ikatuondoa katika hoja.

Wazanzibari hatuhitaji kufanya ghasia wala fujo wala kutumia matusi kama nilivyosema. Hapa nilitoa mifano michache tu, tuna hoja lukuki za haki zetu.
Mhe. Spika, niwaombe sana Wazanzibari wakubali kufuata taratibu, Tume ya Katiba inakuja wakatoe maoni yao, wayazungumze haya na mengine, tupo tayari kuwasaidia, tudai haki zetu.
Mhe. Spika, mimi nasema hapa, mimi naamini katika haya niliyoyazungumza na kwa niaba ya wenzangu wote ndani ya Baraza hili, kwa sababu sisi tumechaguliwa na wao, tutasimamia wanachokitaka. Nawatoa wasi wasi wananchi wa Zanzibar, Baraza hili litawasimamia haki zao na wanachokitaka.
Tuwaombe wao ikija tume wakatoe maoni yao, walichokuwa hawakitaki wakaseme hawakitaki, wanachokitaka wakaseme wanakitaka. Sisi tutasimamia maamuzi yao yoyote hata yakiwa magumu kiasi gani, tutayasimamia. Lakini hayo yatakuja ikiwa kwanza tumetumia fursa ambayo ipo. Ikiwa fursa hii itakwama kwa sababu wengine wana wasiwasi. Ikiwa fursa hii itakwama Baraza hili lipo, Serikali yao ipo, Rais wao Dokta Sheni yupo, Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif yupo, Makamo wa Pili Balozi Seif yupo, watasimama kidete kuhakikisha sote kwa pamoja tunayasimamia maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo nasema nitaiunga mkono hoja lakini baada ya kupata maelezo ya kutosha juu ya hoja nilizozitoa hapa. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Azza wa Wajalla kwa kunipa afya njema na sasa hivi kuweza kusimama hapa kuweza kuchangia bajeti hii ya serikali kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, katika hilo basi kwanza nianze kwa kutoa pongezi za dhati kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuwasilisha Bajeti nzuri yenye matumaini mazuri kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, pia niwashukuru wenzangu wote waliochangia kwa namna moja au nyengine, lakini pia nianze na mimi kwa kuchangia kwenye ukurasa wa 35 juu ya uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa kuweza kukuza uchumi kutoka asilimi 7.5 kutoka asilimia 6.8 mwaka 2011/2012. Niipongeze serikali kwa dhati kabisa katika kukuza uchumi kwa kuangalia kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu Zanzibar. Ila natoa angalizo katika hili kwamba zao la karafuu hivi sasa, hivi duniani limeanza kuwa ushindani mkubwa sana na soko la dunia halina uhakika wa kudumu, linaweza likapanda linaweza likashuka. Lakini ushindani ambao upo unaweza ukatupunguzia zile nguvu ambazo tunazitarajia. Ni vyema serikali ikaona kwamba kuna haja ya kuangalia vyanzo vyengine vikuu ambavyo vinaweza kutusaidia katika kukuza uchumi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, ninataka kuzungumzia suala jengine. Katika kuangalia kitabu hiki Mhe. Spika, kuna mambo ambayo ni muhimu sikuweza kuyaona na hususan katika suala la bahari kuu kwani suala hili linaweza kukuza uchumi mzuri wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sasa Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja ninafikiri atatueleza ni sababu zipi za msingi ambazo hakuainisha suala la bahari kuu katika suala la kukuza uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba niendelee kwa kuangalia ukurasa wa 37. Mhe. Spika, katika vipaumbele ninafurahi kuona suala la vijana kupewa kipaumbele, lakini kwa masikitiko makubwa sana, naomba kwamba Mhe. Waziri hakuainisha basi ni namna gani vijana watanufaika na vipaumbele ambavyo yeye amevikusudia.

Kwa sababu katika ukurasa huu Mhe. Spika, sehemu mbili tayari zimeelezwa wazi wazi, ukiangalia wazee wameelezewa kwamba wao wataimarishwa kwa kuongezewa kipato kutoka shilingi kumi na tano elfu hadi shilingi arobaini elfu. Lakini kwa upande wa akina mama na wao wameelezwa wazi kwamba serikali itachukua jitihada ya kuondosha malipo katika suala la uzazi, lakini katika suala la vijana halikuelezewa hasa nini serikali inategemea kuwatengenezea vijana ili kuwaondoshea matatizo yanayowakabili katika maisha ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, katika kuendelea kuna suala ambalo pia linanipa mashaka. Serikali Mhe. Spika, imejipanga vizuri sana na imeelezea jinsi ya kukuza uchumi na matumaini waliyokuwa nayo, lakini kubwa mimi ninataka kulichangia leo ambapo wengi wamechangia kwa namna mbali mbali.

Mimi zaidi ninazungumzia katika suala la matumizi kwa sababu tunaweza tukakusanya vizuri, tunaweza tukapata mambo mazuri lakini matumizi hayakuwa na udhibiti mzuri basi Mhe. Spika, hali itakuwa ni ile ile. Na

hili silizungumzi kwamba ninalipigia kelele tu Mhe. Spika, ninalizungumzia kwa kulitolea ushahidi wa kutosha na ninasubiri bajeti za wizara zitakapokuja basi nizikabe koo katika hali hii.

Mhe. Spika, mapato ya serikali hii yanatumiwa katika hali ya kutisha kabisa. Hata mtoto mdogo hawezi akafanya Mhe. Spika. Mhe. Spika, nina ma-*documents* haya ya baadhi ya wizara ambazo nimekuja nazo, na ninapitia moja baada ya jengine. Kama utaangalia basi Mhe. Spika, sijui utahuzunika namna gani.

Leo watendaji wa serikali katika kazi za kawaida Mhe. Waziri anatembelea kuangalia kazi za serikali katika wizara, basi watu wanakaa wanapanga posho kwa kutembelea kazi zile zinazowahusu. Hiyo ni hatari na posho ukiangalia basi mtu anapewa shilingi laki kwa kufuatana na Rais kwenda kuangalia kazi za wizara katika hali ya kawaida.

Mhe. Spika, kweli tunaweza tukafika kwenye hali kama hii. Hatuwezi kufika. Hiyo ni sehemu moja tu Mhe. Spika, kwamba watu Rais anatembelea wizara, watu wakishatoka pale wanagawana mapato. Kuna *commitment* nyengine waziri anakwenda kuzungumza na wafanyakazi wake katika vikao vya kawaida, ndio haki yao ya msingi hupanga posho. Hii ni hatari.

Mhe. Spika, hii ni wizara moja tu. Sasa wizara moja wanafanya mambo kama haya mapato yanateketea katika hali kama hii, sijui hizo wizara zipo katika hali gani Mhe. Spika. Hatari kubwa ipo katika hali hii. Ninasema tunaweza tukakusanya mapato mazuri, tukapanga mipango mizuri, maendeleo mazuri lakini tukashindwa kutekeleza kwa sababu pesa zinatumika ovyo.

Mhe. Spika, hali kama hii basi na sisi tungepata ingekuwa *alhamdulillah*. Huku kuna posho tumejiwekea siku hadi siku. Kila mtu anapewa shilingi milioni moja. Watu wanafika muda wao maalum ukifika, watu wanapewa pesa kwa ajili ya sera za kazi.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninataka kugusia hili. Wenzangu wamezungumza mengi tukirudi mule kwa mule basi itakuwa ni hayo hayo. Kweli tuna vyanzo vingi vya mapato kama wenzetu walivyozungumza, tunadhulumiwa na ndugu zetu. Kama wenzetu wanavyosema tuna haki ya kupambana ili kuona haki zetu kama Wazanzibari zinapatikana.

Kuna gesi asilia hii hapa hatujasikia hapa, bado halijatoka katika muungano Mhe. Spika, na kuna pesa nyingi zinapatikana katika gesi asilia watu wamezungumza, kuna bahari kuu au TCA na mambo mengine mengi tu kwa sababu tutarejea hayo hayo. Lakini kama tunavyosema wananchi wametuchagua kuja kusaidia haki za Wazanzibari, tutazisimamia kwa nguvu zote lakini na wale watendaji ambao ni wakorofi, ninasema kwa wale watu ambao tumewapa dhamana za mawizara hawatumii kazi zao ipasavyo, muda utakapofika kwa wizara zao basi wajiandae lakini kazi ipo katika bajeti hii Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kukaa na ninaunga mkono hoja, ahsante (*Makofi*).

**Mhe. Shawana Bukheit Hassan:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kunipa afya ya kuweza kusimama kwenye hadhara yako hii, ili kuweza kuchangia hotuba ya bajeti hii ambayo ipo mbele yetu.

La tatu Mhe. Spika, nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa wizara husika aliyewasilisha bajeti yake hapa kwa nguvu zake zote, katumia takriban masaa yasiyopungua mawili kwa kweli kawasilisha hotuba yake nzuri na safi, na kwa kweli ina mwelekeo mzuri kwa mustakabali wa wananchi wetu. Tunampongeza sana yeye pamoja na watendaji wenzake aliowataja hapa siku ambayo amewasilisha, wote tunawapongeza kwa sababu ametuletea kitu ambacho kinawapa matumaini wananchi wetu. Hongera sana Mhe. Waziri (*Makofi*).

La tatu Mhe. Spika, nichukue nafasi hii pia adhimu, muhimu na maalum kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi anavyosimamia maendeleo ya wananchi wetu, na jinsi anavyojitahidi kuona anaondosha kero mbali mbali ambazo zinawakabili wananchi. Ninasema ninamshukuru sana, ninampongeza na tunasema hongera sana Mhe. Rais (*Makofi*).

Mhe. Spika, katika hotuba ya bajeti iliyowasilishwa, kuna masuala ambayo muda mrefu kwa kweli ilikuwa ni kero, ni tatizo na shida kwa wananchi wetu. Mhe. Rais kayatolea tamko kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Dole tunampongeza Rais.

Masuala yenyewe ni kama haya yafuatayo. La kwanza suala la kuchangia mama mjamzito katika kujifungua ya kawaida, na hasa yale ambayo yaliyokuwa mama inabidi afanyiwe operesheni. Hili lilikuwa ni tatizo na kwa kweli lilikuwa halijapata maamuzi ya uhakika kuweza kupatiwa ufumbuzi jambo hili.

Mhe. Rais Mhe. Spika, ametoa hii kauli kwa kweli ni tatizo ambalo lilikuwa wananchi wetu wanapata mambo ambayo hawayategemei kwa sababu kiwango kilichokuwa kimeekwa kimepindukia mara mbili, na kwa kweli imefikia mahali hali ni ngumu kwa yeye mjamzito anayekwenda kujifungua kufanyiwa lile jambo, lakini hata wale jamaa zake. Mhe. Rais tunamshukuru kwa hili.

Lakini jengine suala la kuweza kuona na wazee wa Sebleni nao wanapata stahiki zote za kusaidiwa kwa hali zote kwa aina baada ya kile kidogo walichokuwa wanapewa kwa ajili ya kujisaidia wao wenyewe. Sasa hali kama hii kwa kweli kama ilivyokuwa na sasa imejirejea, tunashukuru sana katika suala zima la kuwatunza wazee wale. Na imani yetu kuwatunza wazee wale kwa hali na mali, tunaamini imani ya nchi yetu na uradhi wa watu wetu wale hali itakuwa nzuri katika nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo katika bajeti hii limezungumzwa na hilo limo katika shukurani na pongezi. Kukushukuru kabisa Mhe. Rais katika kuona hasa kuna haja ya suala la dawa kulibeba sisi wenyewe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni suala zuri, kwa kweli tunasema mtegemea cha ndugu hufa maskini.

Kwa kweli tulikuwa tunadhalilika, tunasononeka kwa suala muhimu kama hili kuwa bado tunategemea wahisani ndio suala liende. Kwa kweli ilikuwa ni tatizo Mhe. Spika, na ndio maana kukawa na ile hofu ya kuona kuwa tusipotoza hii asilimia ambayo ya kuchangia waja wazito kwenye suala la operesheni, litafikia mahali itakuwa wengine watashindwa kufanyiwa. Kwa sababu vile atakavyokuletea mtu kukusaidia tunasema sio kukufikisha safari. Atakayekuletea atakuletea yeye anachoona akuletee.

Lakini inawezekana hali Mhe. Spika, ikawa haitokidhi. Sasa kwa pale inabidi lazima wachangie watu ili kuweza ku-cover ile hali ili na wengine wakija waweze kupata ile huduma. Pale ndio tatizo lilipokuwa. Lakini serikali leo imeamua na imesema kabisa kwa kuwa sasa hivi wafadhili hatutowategemea moja kwa moja, kutakuwa na fungu maalum la kutoa dawa sisi wenyewe katika serikali yetu. Hongera Dk. Shein Mwenyezi Mungu akupe kila la kheri na sisi tupo pamoja na wewe. Nimefurahishwa Mhe. Spika, na kufarijika na imani imenipata zaidi na sasa kweli ile ilani aliyoisema Mhe. Waziri, ilani ya CCM inasema kuna maisha bora kwa kila Mtanzania, au maisha bora kwa kila Mzanzibari yeyote ni sawa, lakini sasa tunahisi kwa kweli yale mambo ambayo walikuwa wanahisi watu hapa maisha bora hayapo, sasa kuna dalili ya kurudi maisha bora. Na suala la kusema mapinduzi daima pia linajirudia. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo na pongezi hizo, sasa nianze kuchangia bajeti yetu. Mhe. Spika, nianze kuchangia bajeti hii, nikianzia mchango wangu kwenye ukurasa wa nambari 7, 8 na 9. Katika suala zima la ukuaji wa uchumi Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi ninapongeza kwa jinsi hiki kitabu kinavyoeleza ukuaji wa uchumi ulivyo. Kuna namna zote zimetajwa lakini Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi pamoja na yaliyozungumzwa humu, kuna dhana tofauti na ukuaji wa uchumi una dhana pana. Mwengine anasena ukuaji wa uchumi ziwe kila dakika mfukoni ziwepo, lazima apate nyumba za ghorofa tatu au nne, na kila mmoja ana dhana yake ukiacha na haya yaliyoelezwa humu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kasema na katamka wazi wazi kwa kuwa ukuaji wa uchumi ukoje. Kati ya hayo kasema, ukuaji wa uchumi kutokana na soko letu la karafuu limekua sasa, ongezeko la idadi ya watalii, sekta ya viwanda, ujenzi wa barabara, ukuaji wa pato la taifa na sekta ya viwanda, tunapongeza na mengi mengineyo kayataja. Lakini nimeyataja hayo mimi machache, tunapongeza kwa sababu kwa kweli dira inaonesha kuwa hali ni nzuri.
Lakini Mhe. Spika, pamoja na hii hali ambayo tumeelezwa, na hasa katika suala la ongezeko la mapato yetu ya ndani. Kuna haja kuona kwa kuwa tunatafuta na vianzio vyengine vya mapato ili uchumi wetu uweze kuongezeka.

Mhe. Spika, suala la karafuu limekuwa si jambo lione la kulitegemea kabisa. Suala la karafuu kwa bei kupanda na kushuka, kama vile wale wanaosema presha inapanda na kushuka, leo imepanda na kesho imeshuka.

Watalii inategemea na mazingira yalivyo, mazingira mukiyachafua tu kidogo, juzi tu ninasema wanasema wanafika airport tuje tusije. Sasa kuna mambo ninahisi inawezekana yakawa yanatuongezea mapato na uchumi

ukapanda, lakini hapo hapo tusipokwenda vizuri nayo inawezekana tukafikia hali ya uchumi ukashuka na mapato yakashuka.

Pia akazungumzia kuna sekta ya viwanda, pamoja na jitihada iliopo ya wenzetu kuanzisha hivyo viwanda vyao walivyovianzisha, lakini kama serikali na kushirikiana na wananchi ambao wanao uwezo, kuna haja ya kuongeza viwanda. Hivi vilivyotajwa havikidhi kuwa ni uchumi wa nchi yetu.

Mimi si mtaalamu sana wa nchi ambazo wenzangu wametembea na kuona, lakini kwa taarifa tunazozisikia ya kwamba uchumi unakua endelevu katika maeneo au katika nchi ambazo zina viwanda vingi. Kwa hivyo kama hilo ni sahihi, Mhe. Waziri awashajihishe wenzetu ili na sisi hapa waje waelekeze na tuweze kuwa na viwanda vingi, ajira zipatikane na vijana wetu waweze kuajiriwa na uchumi wetu uweze kukua na pato letu la nchi liweze kuongezeka.

Mhe. Spika, ninataka kuungana na wale wote kwa sababu azma ya serikali, Rais na viongozi kuona ya kwamba wananchi wake wanaishi kwa raha, bila ya shida. Kitabu kinasema hiki ni kitabu cha kuhusu mpango wa maendeleo na makadirio ya mapato na matumizi.

Mhe. Spika, nataka kuungana na wale wenzetu wote au wenzangu wote walioanza kuzungumzia suala zima la udhibiti wa mapato lakini na udhibiti wa matumizi. Mhe. Spika, bado mapato yanazidi na hili tunasema kila siku sijui litapata lini, mapato yanavuja. Hapa ilifikia mahali. Mimi ninakumbuka katika awamu hizo za nyuma kwenye vikao hivi vya Baraza. Tukasema jamani kama *TRA* wanakusanya vizuri waongezeni.

Mhe. Spika, taarifa ziliopo kwa kuwa pamoja na mapato na posho tulizowaombea lakini bado mapato yanavuja, rushwa ipo. Kumetolewa mfano na sio mfano ameelezea humu hivi sasa bandarini ataweka *scan* ya kuangalia mizigo, wafanyabiashara na vitu gani, sasa hivi kodi zitapunguzwa lakini mimi naona bado Mhe. Spika, hawa wafanyabiashara kodi watapunguziwa na bei zake pale pale na kuzidi.

Lakini hata hivyo Mhe. Spika, hizo *scan* zitakazoekwa huko, vitu vitaonekana kwani sio kuwa havionekani, vitu vinaonekana lakini rushwa imekithiri na dawa yake haijulikani ni kitu gani. Kwa hivyo suala hili litafutiwe dawa kwanza. Mapato yanayopatikana si kidogo. Hayo makisio yanayopewa wizara waweze angalau kujikimu kwenye wizara huwa maisha hayatimii au kukamilika kwa sababu nini? Fedha hazikusanywi kikamilifu.

Na wengine wamesema hapa hata zikikusanywa kikamilifu Mhe. Spika, ulafi na ubadhirifu, kila mtu anataka kujaza tumbo lake, kila mmoja anataka aonekane yeye ndiye ndio yeye, hatufiki na Mwenyezi Mungu atatuhukukumu kwa hili. Kwa sababu tujue kuna watu wana dhiki, wanalala na njaa na shida mbali mbali.

Mhe. Spika, kuna wakati ililetwa ripoti hapa, tukawahukumu, ni taarifa nisamehe lakini kwa kweli ni taarifa ambayo inayosema kuna baadhi ya viongozi wetu wameonekana hali si nzuri katika matumizi labda na hali ya mambo mengine.

Mhe. Spika, hao inawezekana ikawa ndio ndivyo, na kama vyenginevyo basi imeshapelekwa ripoti ilipo, itachunguzwa halafu baadae tutakuja kuambiwa lipi ni kweli. Lakini hao kama kweli, si kweli, ni wachache na baadhi ya hao wanaofanya hayo Mhe. Spika, au waliokisiwa kufanya hayo, lakini hayo wanayapata kwa niaba ya watendaji wao.

Mhe. Spika, mawaziri wakati mwengine utawakuta yanawakuta mambo ambayo hawayaelewi. Watendaji wanakuwa wana nguvu, kuna neno linalosema wapambe huwa na nguvu kuliko mwenye shughuli. Sasa hili lipo linatokea.

Suala linalosemwa la kuwa watendaji, wanisamehe kama hapo juu wapo, kama Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, sijui Mameneja na nani, huko Mhe. Spika, mimi ninaamini kwa kuwa huko ndio maeneo yanaumia pesa za wananchi. Waziri wakati atake asimamie lakini aliyepewa *authority* ya kusimamia ni Katibu Mkuu, Waziri mwengine anapewa taarifa na wakati mwengine hapewi.

Sasa utakuta hali inakuwa ngumu. Sasa huko ndiko wanagawanagawana ndio wakapigiana mafungu, waambie basi warejeshe marejesho jinsi zilivyotumika, huyu kaingilia huku, huyu nitaleta kesho, huku keshokutwa. Hili lipo na Mhe. Spika, Mhe. Waziri na mawaziri wote na Makamo wa Pili wa Rais watafute jinsi ya kulitafutia dawa fedha zinaliwa kiholela.

Sasa mimi nilikuwa ninataka nitoe rai Mhe. Spika. Mhe. Spika, tumestahamili vya kutosha wananchi wetu wanalipishwa kodi kiasi cha kutosha, lakini hali bado inakuwa ngumu. Hapa tumelalamikia mapato mengine hatupati na nini na mapungufu chungu nzima yamesemwa, inawezekana kweli hayo yapo lakini ije OIC, OIL, OIZ vyote vije lakini kama usimamizi si mzuri hali zitakuwa hivi hivi.

Mhe. Spika, kwa hivyo tunachoomba na mimi ningeshauri hasa ikiwezekana kama Mhe. Shein atanisikia naomba anisikie, sasa umefika wakati kuundwa tume ya kuchunguzwa viongozi, watendaji, wakurugenzi, na hali kuonekana kwa kuwa hali alipoingia kazini na hivi sasa walivyo. Hatusemi watu wawe maskini lakini sio wale mpaka matonge yanachuruzika, nini maana yake.

Kwa hivyo hilo ninaliomba na wateule ningeomba sana Mhe. Rais na anisikie, wateule wa Rais, kuanzia mawaziri, manaibu mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi na ngazi zote, kabla ya mtu hajaanza kazi aidhinishe mali zake. Nchi yetu ndogo hii. Hata ukisema kile cha mjomba au cha shangazi au mtoto wa nani itaonekana tu.

Mhe. Spika, mheshimiwa mmoja kasema hapa yanayomkera, katika moja linalomkera ni hilo kwa nini tunakwenda hivi? Marehemu Karume alisema hicho hicho kidogo kiliopo basi tugawane kidogo kidogo lakini kwa nini wenzetu wakomba.

Mhe. Spika, naomba kwa hili lifanyiwe kazi na waheshimiwa wote mulifanyie kazi kuwasimamia watendaji wenu, muwe wakali. Tena ninampongeza sana Dk. Shein kwa sababu wakati mwengine mawaziri wanaambiwa wanamdanganya Rais, lakini na wao ndio walivyoambiwa na watendaji wao, lakini ule mtiririko wa kuwa sasa njooni nyote hapa, haya wewe sema ulilolifanya na fedha ulizochukua kwa quarter hii, hii inasaidia. Mhe. Spika, mimi ninampongeza kwa hilo, akinambia anasema maana yake anafuatilia sana, kazi za mawaziri anafanya yeye, ndio siku hizi hakuna uaminifu kiasi hicho.

Mhe. Spika, nimesema kwa kuwa katika suala la mapato wenzetu waangalie zaidi hali ya ukuaji wa mapato. Kwa mfano *ZRB*, kila siku tunapiga kelele ya kuwa wafanyabiashara unajua kila siku wanahitaji wao wapate zaidi, hawafakirii kwa kuwa nipate thawabu na nini, wanasema hivyo ni vitu vya baadae bwana, bora kupata.

Kwa hivyo, tukija kwenye masuala ya madukani, tumeshasema mara nyingi. Jamani kuandaliwe utaratibu. Kuna wakati, niliwahi niliona kama zowezi lilifanyika sijui mwaka gani. Unatoka nje ya duka unaambiwa risiti, mtu akikamatwa na kitu hana risiti rudi ndani umeiba, ndio. Lakini siku hizi hakuna, unanunua kitu bila risiti kiasi fulani, kama unataka risiti kiasi fulani, nini maana yake, tunakwenda wapi. Sasa kwa nini tunakwepa kodi.

Itafikia mahali huu uhisani utakwisha, kwa sababu wao huko wanalipishwa mambo chungu nzima, maji wanalipa, umeme wanalipa, ardhi wanalipa, nyumba wanalipa kila kitu wanalipia na wanacholipa ni nini, ni kodi na humo ndani ya kodi ndio wanapopata misaada ya kutuletea sisi. Sasa sisi tunakwepa kodi, tena utakuta sisi wakubwa ndio wakwepaji wa kodi kweli kweli, lakini na hao wakusanyaji wa kodi, kazi iko hapo Mhe. Spika, kodi ya milioni 5 mtu anaambiwa toa 500,000/- , anapewa na siku mbili anatia mfukoni kazi imekwisha, tunakwenda wapi. Yeye anataka mshahara huyo, anataka kusomesha wanawe huyo, anataka kutibiwa wanawe huyo, mama yake yuko kijijini anataka mbolea na mbegu, yeye kachukua laki 500,000/- na simu mbili kwa milioni 5, wapi tunakwenda ni hatari. Tuache tutauwa watoto wetu kwa tamaa zetu.

Mhe. Spika, pamoja na yote niliyoeleza bajeti ni nzuri kwa maelezo hayo, lakini usimamizi ndio kitu ambacho kinahitajiwa, bajeti ni nzuri pamoja na mapungufu yaliomo kuwa sehemu gani ilizidi mwaka jana na sehemu gani imepungua na kuonekana labda miradi ya maendeleo imepanda kidogo. Mimi nasema unashona nguo kwa mujibu wa maungo yako. Kwa hivyo, mimi nadhani hii nguo imeshonwa kwa mujibu wa maungo yetu, lakini fedha zipatikane. Kuna kashfa zimeanza kutoka kwa wenzetu, fedha za wahisani nyengine zinaliwa, mahesabu hayaji na mambo hayaendi. Tukipewa mikopo nusu kuna asilimia 10 nasikia, lakini sio utaratibu mzuri tuache.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza Mhe. Waziri alilizungumzia katika suala zima la ajira kwa vijana, ukurasa kidogo nimeusahau lakini Mhe. Waziri mwenyewe na watendaji wake wataukumbuka. Lakini ile idadi aliyotupa imetushangaza, ile idadi ya kati ya 24 sijui mmoja tu ndiyo hapati ajira. Hee; Naona huko majumbani wengi tunao hawana ajira. Sasa kama hatukufahamu basi atufahamishe na kama hatukuelewa basi atuelimishe. Huu ndio wakati wetu tuko hapa wa kuweza kuuliza na tuweze kupata majibu.

Mhe. Spika, nitalirejea, naomba wanisamehe wenzangu, wasione kuwa labda hakuna, maana ndio tunaweka sawa mambo. Kuhusu wahasibu yeye mwenyewe kawataja hapa, kafanya marekebisho na kila kitu. Pamoja na ma-*internal auditor* mimi naongezea. Suala la kukaa muda mrefu mahali ni tatizo. Wenzetu wameshabadilisha

utaratibu, wahasibu miaka miwili miwili tu inatosha, toka nenda mahali fulani, ikizidi mnajenga urafiki na ushoga, mkishajenga urafiki na ushoga basi tena mambo yamemalizika. Kwa hivyo, utaratibu wa kuwekwa wahasibu miaka 5,10,15,20 uachwe.

Mhe. Spika, bajeti ni nzuri mimi naikubali pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Dole, kwa sababu wamesikiliza na wameisikia, imewagusa wakulima, imewagusa wafanyakazi, walemavu, vijana, wakulima wa mambo ya kupatiwa pembejeo, mbegu na kadhalia. Pia imehusiana na mambo ya barabara ambayo nayapongeza kwa sababu suala la barabara linawasaidia sana wakulima wetu kuleta bidhaa zao mjini, maeneo ambayo bidhaa zilikuwa hazifiki na hapo nao ukuaji wa uchumi unakuwa kwa upande wao.

Mhe. Spika, mwisho niseme kuwa mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Dole tunaunga mikono hotuba hii, lakini tunachoomba yale ambayo tumewasilisha yafanyiwe kazi na tuone bajeti ijayo ime-*improve* vipi katika matumizi na tuone hali halisi ya yale yaliyopangwa yametekelezwa, mambo mengine ya Muungano na mimi sitaki kuyagusia leo, hotuba nyengine zinakuja tutapata nafasi tutazungumza vizuri. Leo nilitaka kuzungumza hili tu ambalo na mimi lilikuwa linanikera ninapoyaona yananiudhi, kwa hivyo na mimi nikasema leo ni hapa hapa niyaeleze.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache niliyochangia, narudia tena kusema, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Dole, tunaipongeza bajeti hii na tunawashukuru viongozi wetu, tunamuomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na afya, yale yote tuliyoyazungumza hapa yaweze kufanikiwa kwa mustakbali wa nchi yetu na wanachi wetu kwa jumla. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii ya ghafla kutaka kuchangia mswada huu wa bajeti ya mapendekezo ya bajeti yaliyo mbele yetu.

Pili nikushukuru kwa kuniona kusimama kwangu ghfla kwa hilo. Nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa lugha yake nzuri, yenye ufasaha katika kuwasilisha mapendekezo hayo.

Mhe. Spika, mimi nianze pale Mhe. Waziri alipotoa masikitiko madogo kwa uzamaji wa kile chombo ambacho kiliuwa mamia ya Wazanzibari. Chombo ambacho kilizama tarehe 10/09/2011. Mhe. Spika, chombo kile kimetuachia msiba na huzuni katika visiwa vyetu, kwa kuwapoteza ndugu, kaka, mama zetu na kadhalika. Serikali sijui baada ya kutoa huduma zile za kuwafariji watu, imechukua hatua gani nyengine ya kuhakikisha kuwa tunapata chombo cha uhakika cha kusafiri kutoka visiwa vyetu hivi viwili vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa kuwa bado serikali haijajitoa moja kwa moja katika suala la biashara na ndio maana ikawa wanalo Shirika la Meli, ningeomba watuambie ni lini watatuwekea chombo cha uhakika kabisa, sio cha mtumba ambacho tutaweza kutumia kutoka katika visiwa vyetu hivi viwili ambavyo hivi sasa havina usafiri wa uhakika.

Mhe. Spika, baada ya kuzama chombo kile, huu mwezi wa 5 tu uliopita, mimi nimerikodi matukio matatu ambayo yalikuwa karibu yasababishe msiba kama ule. Tarehe 03/05/2012 Meli ya Kalama nayo ilikuwa bado kidogo ipoteze maisha ya Wazanzibari tena. Tarehe 05/05/2012 Sea bus one nayo katika safari zake lilizima moto njiani. Tarehe 12/05/2012 *Seagull* kadhalika nayo ilizima moto njiani. Matokeo yote haya yanayotokea serikali ipo, wanaona kuwa Wazanzibari wanachungulia kaburi, lakini bado haijachukua hatua madhubuti ya kukubaliana na jambo hili.

Mhe. Spika, kama CDF iliyokuwa Mtambile ingekuwa inaweza kununua meli basi mimi ningenunua meli, kwa sababu tumeambiwa tutumie fedha hizi na mawaziri, lakini sisi hatununui meli.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ningeiomba serikali ituonee huruma au iwaonee huruma raia wake kwa kuwapatia chombo cha uhakika kabisa, vyenginevyo mimi pendekezo hili kwangu mimi litabakia ni pendekezo la bajeti, sitothibitisha. Mhe. Spika, pendekezo limezungumzia kupanda kwa uchumi na hii inatokana na sekta mbali mbali ambavyo Mhe. Waziri kazitaja. Lakini ni kweli uchumi unakuwa kama ulivyotajwa kwa kupitia mahoteli na sekta nyengine, hoteli nyingi ni za wageni, kwa hivyo kile ambacho kinapatikana zaidi hakitumiki ndani ya nchi hii, kinakwenda kwa wenyewe wanaokimiliki. Kwa hivyo, uchumi unaongezeka, lakini kinachopatikana hakitumiki hapa. Hivyo, Mzanzibari bado anabakia duni kama alivyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katuambia kwamba mwaka 2010 pato la wastani la mtu lilikuwa ni TShs laki 782,000/- kwa mwaka. Hizi ni sawa na TShs. 65,166.66/- kwa mwezi ambazo ni sawa na TShs. 2,172.22/- kwa siku, pesa ambazo wastani wake hazinunui hata kilo moja ya mchele, pamoja na kuwa uchumi umekua, lakini

pato la Mzanzibari halinunui kilo ya mchele, sijui ukuaji huo umekua huko lakini mwananchi bado anadidimia. Kwa hivyo, ni ukuaji wa kiajabu ajabu.

Mhe. Spika, mwaka 2011 umekua zaidi kufikia Shs. 960,000/- kwa mwaka, sawa na Shs. 80,000/- kwa mwezi na ni sawa na Shs. 2,696.66/- kwa siku, bado hazijakidhi mahitaji ya lazima ya mtu mmoja katika jamii yake na ile ambayo Mhe. Waziri kaifanya kuwa ni ilani ya CCM ifikapo mwaka 2015 pato la Mzanzibari liwe Shs. 884,000/- ambapo ni sawa na Shs. 73,600 na kidogo na Shs. 2,455/-. Hii kama chama kimepanga ifikapo mwaka 2015 iwe hapo ndio Mzanzibari alipofika, kwa hivyo taswira ya chama katika ilani yake ilikuwa ni ndogo mno, nilitarajia kuwa itampangia Mzanzibari iwe kapanda zaidi, lakini imemfanya bado yuko chini mno.

Mhe. Spika, hii ndio hali ya kuwa uchumi umekua, lakini Mzanzibari kadumaa. Pamoja na kudumaa huku bado katwikwa mzigo mwengine mzito. Kwa sababu unapoongeza kodi ya aina yoyote hata iwe ndogo kiasi gani, basi mtu wa mwisho anayelipia kodi hiyo ni mlaji wa mwisho, mwananchi wa kawaida. Kwa hivyo, bei ya mchele ilivyo leo, keshokutwa itaongezeka. Tayari waziri kaongeza usafiri baina ya Unguja na Pemba, hiyo iliopo hatuiwezi na bado serikali inatutwika mzigo mwingine. Kwa hivyo, chochote ambacho kimeongezeka katika kodi basi hicho kinamuendea mtu wa kawaida ambaye hana uwezo wa kumudu hilo ongezeko. Kwa hivyo Mhe. Spika, hii hali ni ngumu na ni tete kwa mtu wa kawaida kuweza kumudu maisha yake na bado serikali inamuongezea mzigo.

Mhe. Spika, katika bajeti hii Mhe. Waziri vipo vitu ambavyo amevipa kipaumbele, moja wapo ni ajira kwa vijana na nyengine kuwahudumia wazee. Lakini nimeona kwa mtazamo wangu mimi serikali itakuwa na wazee wa aina mbili. Kundi la kwanza nione hao wazee ambao serikali itawatunza, ambapo kitabu kimoja cha bajeti kimewataja wa Sebleni tu, na kitabu cha pili kimetaja Sebleni na Welezo. Sasa sijui ipi ni ipi ambayo imekusudiwa. Kwa hivyo, hawa niliwafanya ndio wazee haswa na kuna wazee wengine mimi niwaite ndio wazee wa mitaani, kama vile kuna watoto wa mitaani, kwa sababu wazee hawa ambao serikali imekusudia kuwatunza ni wachache sana ukilinganisha na idadi ya wazee tulionao Unguja na Pemba. Lakini wale ambao wanapatiwa matunzo na serikali ni wachache mno, je wale wengine ambao hawamo katika vituo hivyo wao sio wazee wa Zanzibar, je, wao serikali inawatizama katika jicho lipi.

Mhe. Spika, wako wazee wengine wanapewa Shs. 5,000/- huo ndio mchango wa serikali kuwasaidia wazee hawa. Mhe. Spika, unampa mtu Shs. 5,000/- unamwambia kuwa ajiendeshee maisha yake. Hii ingekuwa na maana sana pale ambapo miaka ya 1960 mwanzo wa Mapinduzi, lakini sio leo kumpa mtu Shs.5, 000/-.

Jengine Mhe. Spika, katika kitabu cha mwaka jana cha bajeti kilitaja kuhusu Muungano na hili suala la mafuta ambalo Mhe. Waziri alizungumza vizuri tu. Mhe. Spika, naomba nitafute nukuu kwenye kitabu hiki cha mwaka jana. Serikali tayari ilikuwa imeshapitisha azimio lake la kulitoa suala hili katika mambo ya Muungano, serikali ni Baraza la Mapinduzi na suala hilo likatoka katika Baraza likapitishwa. Sasa kwa kuwa suala limemalizika, lakini bado serikali inashindwa kusimamia maamuzi waliyofanya wao wenyewe. Sasa hii serikali yetu tuifahamu vipi.

Mhe. Spika, jambo ambalo mwaka jana lilishaamuliwa na tukaambiwa kuwa hatua zinachukuliwa kuhakikisha kuwa tunalitoa katika Muungano, leo halijazungumzwa kamwe suala hili katika bejeti yote hii. Je, tujaalie limeshatolewa ndio likaachwa, je, limeshindikana au serikali ina mpango gani juu ya suala hili ambalo tayari lilikuwa limeshatolewa ufafanuzi huko nyuma.

Mhe. Spika, serikali ningeiomba sana isimamie maamuzi yake, isiogope, hii ni haki yetu. Mhe. Spika, kabla ya tarehe 26/04/1964 Zanzibar ilikuwa ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na ilikuwa ina kitu, uwanachama huu uliondoka na ulipotea baada ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kuungana na Jamhuri ya Watu wa Tanganyika, ambapo leo ukisema Tanganyika, kuna watu wanakuona kama unafanya kufuru. Iliyoungana ni Zanzibar na Tanganyika, haikuungana Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa hivyo, bado nchi zilizoungana ni Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa Tanganyika, ndio ikapatikana hiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuwa hizi ni nchi mbili ambazo kwa vyovyote vile ziliungana, kila moja ina haki kwa mwenzake, tuishi kwa kutegemeana kila mmoja ana haki kwa mwenzake. Lakini sisi siku zote tunabakia tuna kero kero.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katuambia kuna kero saba zimetatuliwa na nyengine zinaendelea. Mpaka lini kero hizi zitafika mwisho wake. Kwa mwendo huo mpaka kesho tutapoulizwa kero hizi hazimaliziki, kwa sababu serikali haiko tayari kusimamia maamuzi ambayo wao wenyewe ndio waliyoyafanya. Kila siku subiri subiri, itakuwa mtoto wa kuku. Kuku anamwambia mama yake mama nataka kunyonya, anamwambia ngoja kesho, nataka kunyonya ngoja kesho, mpaka anaachizwa anakuwa jogoo au mke anakuwa mke anataga mayai mengine, lakini

ziwa la mama halipati na sisi Wazanzibari ndio tunavyofanywa na serikali zetu, kero zinashughulikiwa moja moja. Kama juhudi za lazima hazikuchukuliwa Mhe. Spika, haki yetu kamwe haitopatikana.

Mhe. Spika, huku kupoteza uanachama wetu katika Jumuiya kubwa ya Kimataifa ni moja katika kero, kwa hivyo hata hili halituudhi kuona kuwa aah; sisi tulikuwa na sauti duniani, leo hatuna sauti tena, tumo ndani ya mtungi tunavuma tu.

Mhe. Spika, kabla ya hapo ilikuwa nchi hizi Afrika ya Mashariki tulikuwa na nchi nne, nazo ni Tanganyika, Kenya, Uganda na Zanzibar na zote hizi kwa wakati huo zilikuwa zinatumia sarafu ya aina moja, kwa sababu asili yake ilikuwa ni Koloni la nchi moja hivyo hivyo, zote zilikuwa zinatumia sarafu moja. Lakini baada ya uhuru kila nchi ilianzisha sarafu yake, lakini bado ule Ujumuiya ulikuwa uko. Sasa sisi leo Zanzibar tumekwama, Tanzania Tanzania hatuna letu. Mafuta yako Zanzibar hayachimbiki ya Muungano, sijui tuseme nini.

Mhe. Spika, Wazanzibari na wao ni sehemu ya watu wa dunia. Leo watu milioni moja na kidogo wanaishi kwa Shs. 2,000/- kwa siku. Uchumi kama ungeshughulikiwa, sisi tungekopeshwa, ingelikuwa hakuna deni la taifa, kama tungefikia uchumi wetu kikamilifu pendekezo hili la bajeti lingekuwa halina kitu ambacho kinaitwa deni la taifa, kwa sababu tungelikuwa tuna uchumi ambao unatuendeleza. Leo tuna deni la taifa. Mhe. Spika, naiomba serikali iwaonee huruma raia wake, isikae tu tutaongeza Shs. 1,000/- tununuwe madeski, tutowe Shs. 2,000/- tununuwe dawa, tuongeze mafuta tununuwe hiki, hapana. Hawa unaowaongezea waipate wapi na wao hawana nyenzo ya kuipata wamekaa kimpya.

Mhe. Spika, kwa kuwa nimenyanyuka tu kighafla ningeomba nimalizie hapo ili nione kuwa lile ombi langu la kupatiwa usafiri wa uhakika na wale wazee ambao wako wazee rasmi wa mitaani, ajira iliyotajwa kila watu watano ni mmoja tu ndiye aliyekuwa hana ajira. Kwa kweli niliposikia kwa mara ya mwanzo nilishtuka akaa; hivi serikali pamoja na watu chungu nzima waliowasomesha ni mmoja tu aliyekuwa hana ajira. Kwa hivyo, nilidhani amekosea kusema, lakini kumbe ndio serikali ilivyokusudia. Sidhani kama hali iko hivyo kweli.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache, niseme nakaa na ninangojea kupata majibu kuhusu maelezo yangu, ahsante sana. *(Makofi).*

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba na mimi nichangie hotuba hii ingawa nikiri kwamba matayarisho yangu yalikuwa ni madogo kwa sababu nilitegemea kuchangia kesho. Lakini naomba nianze na baadae wenzangu wapate nafasi ya kuchangia hotuba hii.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali leo kwa mchango wake aliotoa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini. Kwa kweli sishangai kwa jinsi Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali alivyochangia, kwa sababu mtu kufikia kuchukua Fomu ya Urais huwa ni mtu makini sana. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba kwa wale wenzangu wa vijiwe wasiomjua Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kumbe alikuwa na haki ya kuchukua Urais wa Zanzibar. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, hii sasa inadhihirisha kwamba Baraza hili watu watatu waliochukua Fomu ya Urais wa Zanzibar wanazo sifa za kuchukua Fomu ya Urais. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Mhe. Haroun Ali Suleiman pamoja na Mhe. Ali Juma Shamuhuna wanne ni dhahiri kwamba Wazanzibari hawa wanao uwezo wa kuchukua Fomu ya Urais wa Zanzibar. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, bila ya shaka kwamba kwa mpango huu na mwakani tukijaaliwa na kaka yangu Sheikh Mhe. Omar Yussuf Mzee atachukua Fomu ya Urais, nasema hayo kwa sababu anao uwezo wa kufanya hivyo. Kwa kweli uwezo wake ametudhihirishia kuwa ni mkubwa na bila ya shaka Wazanzibari akichukua basi baada ya Dkt. Ali Mohammed Shein tutamuachia nafasi hiyo. *(Makofi)*

Sasa nianze mchango wangu kwa kusema kwamba inawezekana Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hajui pengine thamani yake mbele ya Wazanzibari, kwa sababu mtu mwenyewe hawezi kujitathmini.

Lakini Wazanzibari wanategemea sana mbele ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wanamjua historia yake tokea alipokuwa Mhe. Naibu Waziri wa Ulinzi, baadae akawa Naibu Waziri Fedha na leo ni Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar. Kwa kweli historia yake ni kubwa na Wazanzibari wana imani naye, pengine yeye mwenyewe hajui kama Wazanzibari wana imani naye.

Kwa hivyo, nachukua nafasi kumkumbusha kwamba Wazanzibari wana imani naye na kwa hiyo hapaswi na wala asijaribu kuja kuwatania Wazanzibari, kwani wana imani naye. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza kabisa sikubaliani na ongezeko la kodi ambazo Mhe. Waziri amependekeza. Kwa kweli sikubaliani kwa sababu ni kiini macho tu, kwani unapoongeza kodi ya mafuta maana yake unaongeza kodi ya bidhaa zote, yaani humu amesema kwamba hakusudii kuongeza bei ya chakula kama vile mchele, unga wala sukari.

Lakini yeye Mhe. Waziri ni mtaalamu wa fedha, unapoongeza kodi yoyote maana yake unaongeza kodi ya bidhaa hizo muhimu kwa wananchi na wala sisi hapa hatuzalishi na kwa bahati mbaya hatujapata hata pishi moja ya *NERICA*, mchele wote unaagiziwa kutoka nje, maharage, unga na mafuta ya kula. Kwa hivyo, moja kwa moja unapoongeza kodi ya mafuta maana yake unatuongezea kodi ya bidhaa hizo muhimu za nchi.

Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri akiwa ni Mzanzibari halisi na nimesema kwamba Wazanzibari wanamtegemea, basi azingatie umuhimu wa kupunguza hii kodi kwa ajili ya kuwanusuru Wazanzibari walio wanyonge sana.

Mhe. Spika, pia sikubaliani na haja ya kuongeza kodi kwa ajili ya ada ya bandari, kwa maana kwamba mtu kutoka Unguja na Pemba achangie kodi hii kwa shilingi 1,000/=. Kwa hivyo, akumbuke kwamba Unguja na Pemba si nchi mbili ni sawa na kutoka Mjini ukenda Makunduchi au kutoka Mkoani ukenda Wete ama kutoka Mjini ukenda Nungwi, yaani Unguja na Pemba na masafa yetu hayo ni ya kimaisha. *(Makofi)*

Kwa kweli sababu ya msingi hana, kwa sababu yeye amesema kwamba itasaidia katika ununuaji wa dawa pamoja na madeski. Mhe. Spika, nataka nimuoneshe kwamba hana haja ya kuongeza hii kodi kwa sababu hatuna shida ya madeksi sisi. Zanzibar hatuna shida ya fedha isipokuwa tuna shida ya uongozi, yaani uongozi sio kama hatuna lakini tunataka viongozi wanaojiamini kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwaka jana bajeti ya Elimu ya Juu ilikuwa ni bilioni 317, kwa mgawanyo ule ambao haturidhiki wa asilimia 4.5, basi Wazanzibari tungepata bilioni 14.3 na mahitaji ya Zanzibar kwa Elimu ya Juu si zaidi ya bilioni 7 kwa maana hiyo tungesomesha wanafunzi wetu wa Elimu ya Juu kwa miaka miwili mfululizo bila ya mkopo au msaada wowote. *(Makofi)*

Sasa anaponiambia tuwachangishe kodi Wazanzibari simuelewi Mhe. Waziri, labda aniambie ameshindwa kusimamia haki yetu Wazanzibari kwa ajili ya muungano. Kwa hivyo, nimuombe asihangaike aende kule Bara atupatie gawio letu kila sekta, ili tumsamehe hii kodi Mzanzibari mnyonge. *(Makofi)*

Mhe. Spika, fedha nyengine ambazo Mhe. Waziri anapaswa kuzisimamia ni fidia ya ununuaji wa rada, kwa sababu nimekwenda kwenye mtandao nimeona, tena naomba nimkumbushe nimemuona mtu mwenye bunduki kubwa, yaani ni jeshi Mhe. Spika hawa. Tanzania imelipwa fidia ya rada milioni 29.5 Paundi, kwa gawio ambalo tungestahiki kupewa na hilo shingo upande na asilimia 4.5 basi tungepata si chini ya bilioni 4.

Kwa hivyo, labda aniambie tutapata kiasi gain, kwa nini fedha zipo unashindwa kudai na baadae uje umwambie mnyonge wa Makunduchi na kule Mwambwe ajikamue na baadae achangie madeski.

Mhe. Spika, pia Mhe. Waziri atakumbuka kwamba mwaka jana Benki Kuu ya Tanzania ilitoa msaada ikiwemo kusaidia bajeti kwa maana ya Mtikisiko wa Kiuchumi, yaani zaidi ya *trillion* moja ilitolewa na Benki Kuu ya Tanzania. Kwa hivyo, ni vyema atuambie Wazanzibari walipata kiasi gani na Benki Kuu ikitoa msamaha, maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania ni kwamba wangestahiki kupata Watanganyika pamoja na Wazanzibari, kwa *trillion* moja iliyotolewa tungepata si chini ya bilioni 7 au 8 kwa ile asilimia 4.5.

Mhe. Spika, yote haya inaonesha kwamba hakuna haja ya kumkamua mnyonge, isipokuwa ni kujipanga na kuamua maamuzi magumu na yeye uwezo huo anao, lakini labda tumekuwa na woga. Sasa kama ni woga basi tusimlaumu mtu, ikiwa tuko jasiri maana yake tuamue na kudai haki yetu, tena kwa maneno laini kisheria bila ya panga wala mabunduki. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo nataka niseme kwenye kitabu hiki ambacho Mhe. Ismail Jussa Ladhu amezungumza kwenye ukurasa wa 113, kuhusu *General Government Operation*s, fedha ambazo tumezipata kutoka nje ni trilioni 1 bilioni 379 na milioni 657 mwaka 2010 kwa gawio la 4.5, maana yake mwaka 2010 tungepata bilioni 62.

Mhe. Spika, mwaka 2010 tungepata fedha hizo na leo ndio kwanza Mhe. Waziri anatuambia mara hii anatarajia kupata bilioni 39 na hii ingekuwa tumeipata miaka mitatu nyuma. Lakini Mhe. Spika ama Zanzibar tumeshindwa kujenga hoja au ndani yetu niseme labda tunafanya unafiki. Lakini kama mahesabu haya ni mahesabu ya fedha za nje kutoka Benki Kuu na gawio lipo la *formula* ya 4.5, maana yake na mwaka juzi tungepata bilioni 62 na leo Mhe. Waziri anatarajia kupata shilingi bilioni 39.

Mhe. Spika, nadhani haya yote Mhe. Waziri asimamie tu na wala hana haja ya kumtoza Mzanzibari kodi, isipokuwa tuamue na kuamua kwenye si kwa ugomvi, kwa hoja na haki yetu itapatikana bila ya ugomvi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa *challenge* kwa sababu siamini sana kwamba Wazanzibari tunaonewa na Watanganyika kwani hawatupi haki yetu. Kwa kweli msingi wa haki SMZ watupe *document* ambayo tumeomba na tumekataliwa, kama haipo maana yake hatujaomba, kama *document* ya kukataliwa hatupewi, yaani haipo maana yake SMZ haijaomba. Kwa hivyo, Wazanzibari wanayo haki ya kulalamika, kutusuta na kuna siku watatuhukumu vibaya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi naamini kabisa kwa viongozi ambao tunao chini ya Dkt. Mhe. Ali Mohammed Shein wakiamua basi jambo hili ni la siku tatu tu. Lakini pamekuwa na usanii wa Kero za Muungano kwa ajili ya posho na safari tu. *(Makofi)*

Kwa kweli siamini kabisa kama kweli watu wazito kama kaka yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee mwenye elimu kubwa ya fedha, akavimbe kwenye kiti kwa ajili ya kudai haki yake ya mapato, hivi kweli tukose mapato, inawezekana kuna jambo ndani yake na lazima Wazanzibari walitafute na tuambiane na Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali amesema asubuhi tuambizane kwa uwazi na huu sio wakati tena wa kufanya masihara, kwa sababu nchi inakwenda na wenzangu wananiambia sio inakwenda, yaani tayari imeshakwenda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa niaba ya wenzangu niiombe sana serikali kwamba hebu na tuamue sasa kwenye kudai haki yako hakutaki ugomvi, isipokuwa ni hoja tena zipo na Mhe. Hamza Hassan Juma mwaka jana alisema ikiwa serikali ina muhali, basi wachagueni Waheshimiwa Wawakilishi wawili watatu wakajenge hoja. *(Makofi)*

Lakini serikali iliona kama jambo kubwa ambalo ni tusi na wala si tusi, pengine wewe una muhali kwa mzee wako, basi tupeleke sisi tukaseme na wala sisi hatuna muhali. Mhe. Spika, mkinipeleka Kiwani nitakuwa na muhali kwa sababu ndiko nilikopata kura, lakini ukinipeleka Tanganyika nitasema yale ambayo niliyotumwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nasema kwamba hakuna haja ya kumtoza kodi mnyonge, kwa sababu fedha zipo na hoja au tatizo letu ni usimamizi wa fedha zetu. Mhe. Spika, juzi nilimuona Mhe. Waziri wa Fedha wa Tanzania wakati akihojiwa kuhusu kodi ya *TRA* ya ushuru wa gari, alisema hili jambo lipo na serikali itakaa na kufikiria. Kwa kweli hapa tumeambiwa hii kero imekwisha, na kuna watu wanatuambia watafikiria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninayo *Hansard* ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, mtu ninayempenda sana na siku ambayo atayegombea Urais kwa sababu nitaunga mkono tu. *Hansard* yake ambayo amesema wakati wa Ripoti ya Kamati ya *PAC* iliyopita amekiri kwamba tatizo ni muhali na kuoneana haya, yaani Mhe. Waziri amekiri kuwa fedha zinapotea hapa kiholela, lakini tatizo ni muhali. Sasa ni muhali wa nani wake yeye au nani? Maana yake yeye ndiye tuliyempa dhamana ya fedha.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atusaidie kwa sababu mimi na Mhe. Ismail Jussa Ladhu huko nje tunatupiwa maneno mazito, hivi wenzetu huambiwa maneno mazito kama yale, maana mimi leo umeninyang'anya kazi yangu kubwa kwa sababu ya maneno mazito yako, sasa na wenzangu waambie maneno mazito kama haya kwamba jamani ni wazembe nyinyi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, *Hansard* hii ya Mhe. Waziri ni maneno makubwa sana, hivyo nimuombe sana kupitia kwako Mhe. Spika kwamba asijaribu kuyakiuka, najua serikali si peke yake, lakini awashauri wenzake kitaalamu kwamba jamani ee "muungwana akivuliwa nguo huchutama".

Kwa mfano, ukivuliwa nguo sokoni na ukenda mbio basi hiyo ni aibu, vyema uchutame usubiri mwenzio akupe shuka, na kuchutama kwa hapa Mhe. Spika kila ambaye anaonekana ni tatizo la fedha za umma basi aondoke na wala si aibu. Lakini Zanzibar tumekuwa na tabia ya kulindana na Mhe. Waziri amekiri kwamba watu wanalindana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, leo mimi kama Mwakilishi wa Kiwani nitaamini vipi kumpa mtu fedha wakati mwaka jana tulimkamata ameiba, na leo nimpe tena fedha na wala sifanyi mchezo huo Mhe. Spika, kwa sababu watu wa Kiwani walitegemea kwamba kila aliyetajwa kwanza ashughulikiwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa mtiifu mbele ya Bunge, kwa sababu Bunge limesema tu kwamba huyu ni tatizo na mshughulikie, basi ameondoshwa na hata siku moja Mhe. Rais asingemuondosha Mkullo, lakini ni Bunge limesema kuwa tatizo lipo hapa na pengine sio Mkullo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba mawaziri wetu sio wezi, lakini yeye ndiye aliyepewa dhamana ndani ya Baraza la Wawakilishi na "Mchelea mwana kulia, basi atalia yeye". Sasa leo watu hapa wametajwa na mambo mazito na bila ya kisisi Mhe. Waziri anatuambia basi nipeni fedha niwape tena kwa ajili ya kwenda kula ni hatari kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Kiwani nitazuia kila bajeti ambayo kuna mtu ametajwa na bado hajashughulikiwa, tena ukinuna au ukifurahi kila mtu na kaburi lake. Kwa kweli kila aliyetajwa kwamba huyu ni tatizo lazima ashughulikiwe, basi tuone ndio imani na utawala bora. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi husafiri kwa kutumia bahari, nchi kavu pamoja na ndege, hata kama zote hizo zitazuiwa nisitoke ndani basi nitasema, yaani nizuiliwe nisisafiri angani, baharini nisipite na barabarani si ruhusa nitasema humo ndani ya kizimba kama hili ni tatizo. Kwa nini Mhe. Spika? Kwa sababu watu wasifanye mchezo na Chama cha CCM, kwani ni chama kizuri sana na wala CCM haijamtuma mtu aibe, na wala CUF haijamtuma mtu aibe, isipokuwa anayeiba ni yeye mwenyewe na sio chama. *(Makofi)*

Mhe. Spika, bosi wangu yupo hapa huniambia wacha bwana maana mwenzetu, kwa sababu kwenye utawala bora hakuna mwenzetu kuna kuwajibika. Kwa mfano, kesho akiwa waziri huyu mimi nitamwambia hivyo sivyo utaiba, yaani nitamwambia, na ole wenu muje mumpe uwaziri na aje kuwaibia nitamwambia tu, kwamba unaharibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwangu mimi mtu asije kwamba ah! Tunatoka Mwambe shirika, pengine huyu mwenzetu Mpemba na mimi si Mpemba wala si Muunguja, isipokuwa ni Mzanzibari na ukiharibu nitasema na vyovyote nitasema. Mhe. Spika, mimi nilisema na wala sifichi kwamba mimi pamoja na wanangu tu ndio tuliozaliwa Pemba, baba yangu Tumbatu na mama yangu Tazari, kwa hiyo mimi peke yangu ndio Mpemba. Kwa hivyo, masuala ya kuja lugha huyu Mpemba au Muunguja muachie sikuelewi, ikiwa unaharibu basi lazima uwajibike. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nasema kwa uchungu kwa sababu hatufiki ikiwa kuna watu wanaiba wanaachiwa na kwa jeuri kubwa hatufiki Mhe. Spika. Wazanzibari kuna siku watatusuta, kwa sababu leo Wazanzibari wote akili yao kwenye muungano na kuna siku Wazanzibari wote akili yao watakuwa kwenye uwakilishi mimi nakwambieni. *(Makofi)*

Kwa kweli unapomtesa mtu na kukosa haki yake basi mtu huyo ataasi, leo Wazanzibari wamekuwa wababe kwa sababu hakuna taarifa tu, yaani Wazanzibari wamekuwa wakaidi na kukosa taarifa na wala haki yao, sasa leo wako kwenye muungano na wataumaliza na kesho wataelekea kwa Viongozi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi ndiye wa mwanzo nitakayeinua mkono kwa sababu siwawezi Wazanzibari. Kwa maana hiyo, tusiwaibie na tukafikiri hawana elimu Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi namuamini Mhe. Waziri na bajeti hii lazima tuipitishe kwa sababu hata wote waondoke lazima nchi iwe na mawaziri. Kwa hivyo, tuipitishe na baadae tuwang'owe hawa, yaani tuipitishe na baadae kila aliyetajwa tumng'oe akae mwengine. Kwa mfano, leo Dkt. Mhe. Ali Mohammed Shein amemteua Mjumbe mpya hapo mwanamke na tutampa uwaziri na akiharibu tutamng'oa.

Lakini Mhe. Spika, kamwe sisi kwa sababu mimi nilikuwa kwenye Kamati Teule ile, basi najiuliza ikiwa Kamati Teule hakuna hatua, na juzi umenichagua kwenye umeme na Mhe. Salmin Awadh Salmin amechaguliwa kwenye Manispaa je, hakuna hatua huko. Mhe. Spika, nikwambie huku kumeroa. *(Makofi)*

Sasa ikiwa juzi hatukufanya na kesho hatufanyi na mwisho wa siku itakuwa Mhe. Spika mbaya, maana yake sisi lazima uunde tume, na tukisema uunde inabidi uunde tu huna ujanja na mwisho utakuwa Mhe. Spika mbaya, na kumbe unafanya vitu vyako vizuri, lakini tatizo ni kulindana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niseme tu kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya watu wa Kiwani bajeti hii naiunga mkono kwa sharti kwamba napitisha hii, ili mawaziri husika kwenye sekta kila mmoja tumchunge kile alichokifanya. Kwa mfano, huna pishi ya *NERICA* hufai, huna barabara hufai, huna *ICU* hufai na huo ndio ukweli ulivyo na ukinuna au ukifurahi ni hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye muungano niungane na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba Wazanzibari huu ni wakati wetu wa kuinasua nchi yetu.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, tunakushukuru, kwa kweli muda unatukwaza. Sasa niahirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 19/06/2012 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi*
*tarehe 19/06/2012 saa 3:00 za asubuhi)*